WORLDWIDE BEST-SELLER

MWONGOZO WA MFUKONI KUHUSU MUHAMMAD

KISWAHILI

Mtume wa Uislamu ﷺ

# MUHAMMAD

Mwongozo wa mfukoni wenye michoro ya kumtambulisha Mtume Muhammad (na mafundisho yake matukufu ambayo yalitengeneza misingi ya Maadili ya Ustaarabu wa Kiislamu)

MU HA MM AD

MUHAMMAD

مركز أصول
Osoul Center
www.osoulcenter.com

Chapa ya kwanza

﴿ وَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ إِلَّا رَحۡمَةٗ لِّلۡعَٰلَمِينَ ﴾

الآية ١٠٧ من سورة الأنبياء

MTUME WA UISLAMU

# MTUME WA UISLAMU
# MUHAMMAD ﷺ

Mwongozo wa mfukoni wenye michoro ya kumtambulisha Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, na mafundisho yake matukufu ambayo yalitengeneza misingi ya maadili ya ustaarabu wa Kiislamu.

مركز أصول
Osoul Center
www.osoulcenter.com

**Toleo la kwanza**

MUHAMMAD POCKET GUIDE

دليل الجيب المصور للتعريف بالنبي ﷺ وتعاليمه الشريفة التي
شكلت المقومات الأخلاقية للحضارة الإسلامية

Hakimiliki imehifadhiwa
Kituo cha Osool
Hakimiliki © Osoul Center, 2024

onyo
Kitabu hiki kilitayarishwa na Kituo cha Kimataifa cha Osool, na picha zote zinazotumiwa katika muundo huo zinamiliki haki za kituo hicho au ni chanzo wazi cha Kituo cha Kimataifa cha Osool kinamruhusu kila Muislamu kuchapa na kuchapisha kitabu hicho kwa sharti la kujitolea kukijulisha Kituo hicho rasmi. hii, ikionyesha chanzo, na si kubadilisha maandishi Katika kesi ya uchapishaji, inashauriwa Kituo kinazingatia viwango vya ubora katika uchapishaji kulingana na vipimo vilivyoidhinishwa na kituo.

Kwa maoni au maoni, tafadhali wasiliana nasi kupitia tovuti zifuatazo:

osoul@rabwah.com
www.islamhouse.com
www.guidetoislam.com
muhammadpocketguide@gmail.com

Nambari ya uchapishaji ya kimataifa: 978-0-9875891-6-3
Uchapishaji wa kwanza: Juni 2024

Amesema Mtume (S.A.W):

"Hakika mfano wangu kwa Mitume waliotangulia ni mfano wa mtu aliyejenga nyumba vizuri na kuipamba isipokuwa aliwacha sehemu ya tofali moja pembezoni (hakuliweka), basi watu wakawa wanapita hapo na wakistaajabu wakisema: Mbona halijawekwa tofali hapa?. Akasema Mtume (S.A.W): Mimi ndie hilo tofali na mimi ni wa mwisho wa Mitume."

Amepokea Bukhari, Jaamii Sahih (3535)

## UBAINIFU

• Kitabu "Mtume wa Uislamu Muhammad" (rehema na amani ziwe juu yake) (ﷺ), ambacho kinajulikana kwa jina la Muhammad "Pocket Guide" ni muongozo mdogo wa mfukoni wenye picha uliojumuisha kumuelezea Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na mafundisho yake matukufu ambayo yametengeneza vipengele vya maadili kwa ajili ya Ustaarabu wa Uislamu yakawa ni mageuzi muhimu katika Historia ya maendeleo ya mwanadamu na kupiga hatua Elimu, Fasihi na Sanaa.

• Kitabu hiki kinadhihirisha maeneo ya Ustaarabu kwa mafundisho ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) yanayofungamana na mambo yanayowahusu watu kwa ujumla na Wamagharibi kwa namna ya kipekee, kama vile haki za binadamu na haki za mwanamke, na kutunza mazingira, na huruma kwa wanyama, na maendeleo ya kijamii na uongozi wa kibinafsi, na maendeleo ya kiakili,na nyendo njema, na mahusiano na Mataifa mengine pamoja na tofauti zao za makundi na tamaduni zao, dini na Ustaarabu wao.

• Lengo la kitabu siyo kunukuu visa na sira ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwa maelezo na matamshi yake kama yalivyopokewa, bali kitabu kinalenga kuonesha kwa ufupi na wepesi kufahamu bila ya dosari yoyote katika maudhui na maana yake ambayo yamekuja kwayo. Na tumejilazimisha kunukuu hadithi kwa maneno yake kama yalivyopokewa na kutegemea hadithi sahihi katika hizo kwenye kitabu hiki.

• Kimetafsiriwa kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili iliyokua nyepesi kwa lengo la kuwahutubia watu wote pamoja na tafauti ya rika, tamaduni na asili zao kwa kutumia teknolojia ya (PLTP Proactive Language and titled Paragraphs) na inamaanisha ni kule kunukuu maandiko kwa njia bora nyepesi na zilizowekewa vichwa vya habari (kila paragrafu

ina kichwa chake cha habari) kinachowepesisha kufikia kinachotakiwa kufahamika na kufanya usomaji uwe mwepesi na wakuvutia.

• Tumekiita kitabu hiki “Mtume wa Uislamu Muhammad“ (rehema na amani ziwe juu yake) kwa sababu Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kwa mtazamo wa wasiokuwa waislamu ni Mtume ambae amekuja na ujumbe wa Uislamu na ikawa ni sababu ya kuenea kwake ulimwenguni kote. Ama kwa mtazamo wa waislamu ni mjumbe wa Allah kwa watu wote ili awafikishie ujumbe wa Mola wao na awatoe kutoka kwenye giza (upotofu) awapeleke kwenye mwangaza (uongofu) naye ndiye Mtume wa mwisho katika Mitume ambao walikuja kabla yake na ujumbe wa Mola kwa watu wao.

• Limedhihiri neno Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na kulizingatia ni sifa iliyojipambanua kwa ajili ya kitabu na limesaidiwa na michoro mingi na maumbo ya kisanaa yanayotokana na neno “Muhammad” (rehema na amani ziwe juu yake) kwa wasanii na waandishi wa Khati mbali mbali ulimwenguni.

• Hakika matumizi ya neno “Mjumbe” (rehema na amani ziwe juu yake) wakati mwingine na “Mtume” linakusudiwa “Muhammad“

• Na kitabu hiki kimekusanya mlango maalumu kuhusu khati za Kiarabu na usanifu wa Kiislamu katika ulimwengu na Misikiti mashuhuri na vivutio vya utalii vyenye muonekano wa Kiislamu kama Kasri jekundu nchini Hispania, na Msikiti mkuu wa Sultan Ahmad nchini Uturuki pamoja na Misikiti na majengo makubwa ya Kiislamu ulimwenguni yenye muonekano maalumu wa kisanifu.

• Kimetoka kitabu kwa lugha ya Kiingereza mwaka 2010 na kutafsiriwa kwa lugha zaidi ya ishirini mashuhuri za ulimwenguni katika miaka iliyopita.

ⓒجمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالربوة ، ١٤٤٦هـ

مركز اصول
نبي الإسلام محمد صلى الله عليه وسلم باللغة السواحلية. / مركز اصول - ط١. .- الرياض ، ١٤٤٦هـ
١٥١ ص ؛ ..سم

**رقم الإيداع: ١٤٤٦/٩٥٨١**
**ردمك: ٠-٧٧-٨٤٣٨-٦٠٣-٩٧٨**

# UTANGULIZI

Kila sifa njema zinamstahikia Mola wa viumbe wote, ambae amemuumba mwanadamu katika muonekano mzuri zaidi, na akawapa usikivu, uoni na nyoyo, na akawafanya viongozi katika Dunia ili waiendeleze na kuisimamisha dini yake, na wamwabudu yeye kama alivyo waamrisha, na akawapelekea wajumbe kutokana na wao wawaongoze kwake na wawabainishie yale anayoyapenda Allah ili wayafanye na yale anayoyachukia wajiepushe, na akayafanya maisha yao katika ulimwengu huu ni njia ya kuelekea maisha yao ya milele Akhera, nayo ni neema na furaha kwa yule aliyefuata wajumbe wa Allah hapa Duniani. Na adhabu na mwisho mbaya kwa yule aliyepuuza uongofu wa Allah na kuwapinga wajumbe wake.

Na rehema na amani ziwe juu ya wa mwisho wa Mitume wa Allah “Muhammad” mfikishaji kutoka kwa Allah Mtukufu wa kitabu chake cha mwisho kwa watu wa Duniani, ambae ulikua mwendo wake ni kufanyia kazi kwa vitendo kwa yale aliyoyalingania kwa watu katika kumtii Allah Mtukufu na kufuata amri zake. Na vile vile rehma na amani ziwe kwa waliofuata njia yake na wakaenda katika njia yake hiyo mpaka siku ya Kiyama.

Ama baada ya hayo:

Ni furaha yetu katika Kituo cha "Al-Usuul" cha Kimataifa kukuleteeni wasomaji wote kitabu hiki chenye kumwelezea Mtume wetu Muhammad bin Abdillah (rehema na amani ziwe juu yake) na ambacho kimekusanya machache kutokana na maisha yake mema na sifa zake nzuri na vitendo vyake bora katika wakati ambao ubinadamu umefikia katika kilele cha hatari katika Historia, na imefeli mifumo mikubwa ya kibinadamu na mitizamo ya kiutu na kushindwa kuleta ufumbuzi wa matatizo makubwa ya Kimaadili, na wakaelekea wanadamu kulia na kushoto wakitafuta ufumbuzi wa matatizo hayo ambayo yalizihangaisha dhamira zao.

Na sisi Waislamu tunahakika kuwa hakuna ufumbuzi wa matatizo hayo isipokuwa kurejea kwenye maumbile ambayo Allah amewaumbia watu na ambayo wamekuja nayo wajumbe wake (rehema na amani ziwe juu yao) kwa ulinganio wa maumbile hayo, nayo ni kumpwekesha Allah kwa kumwabudu na kufuata sheria zake.

Na tunaamini kwamba hilo linatosha kutatua matatizo ya kibinadamu na kueneza uadilifu, huruma na kheri katika Dunia, na hilo ni lenye kukubaliana na yale aliyotueleza Muumba wetu mtukufu kwa kule kumsifu Mtume wetu (rehema na amani ziwe juu yake), kwa tamko lake Allah: “Na hatukukutuma isipokua uwe ni rehema kwa viumbe wote”.

Na tunaweka mbele ya wasomaji kwa dini zao utambulisho huu wa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake), na sote tunatarajia wausome na wauzingatie kwa nyoyo na akili zao na waachane na yale yaliyomo akilini mwao yaliyosambazwa na vyombo vya habari vingi madai ya uongo dhidi yake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake), au kwa uchache walinganishe baina ya propaganda hizo na kauli za Mtume wetu (rehema na amani ziwe juu yake) na vitendo vyake ili wafahamu kiwango cha dhulma inayofanywa dhidi ya vitendo na kauli hizo.

Na tunamuomba Allah Mtukufu aliyetukuka atuandikie sisi pamoja na wasomaji wote uongofu katika njia anayoipenda.

Na sifa zote zinamstahikia yeye Mola wa viumbe vyote.

مركز أصول
Osoul Center
www.osoulcenter.com

www.osoulcenter.com


ادخلوها بسلام آمنين
محمد
MAKKAH
GATE

# YALIYOMO


**1. Ushuhuda wa wanafikra kwa Mtume (S.A.W) ﷺ** **12**

**2. Sifa zake na tabia zake.** **24**

**3. Maisha yake na historia yake.** **30**

- Maelezo mafupi ya Mtume ﷺ na maisha yake ya kifamilia na ya kikazi.
- Matukio muhimu tokea kupewa Utume hadi kufariki kwake
- Nyongeza ya Picha za maeneo muhimu yanayohusiana na historia yake Mtume ﷺ

**4. Utume na Ujumbe.** **76**

- Vip ialikuwa Muhammad ﷺ ni Mtume na vipi aliupokea ujumbe.
- Uislamu unalingania kitu gani na upi uhusiano wake na ujumbe mwingine wa mbinguni uliotangulia.
- Nini amesema Mtume ﷺ kuhusiana na Mtume Ibrahim, Mussa na Mtume Issa ﷺ.

**5. Maadili na Ustaarabu.** **120**

- Vipi Mtume ﷺ aliweka misingi ya Maadili na Ustaarabu wa Uislamu.
- Vipi aliongezea Mtume ﷺ Maadilimema katika maisha ya watu.
- Mafunzo yake kwa yanayohusia nanamalezinauongozikibinafsina kuamiliana na dhati ya mtu mwengine.
- Mafunzo yake na mwenendo wake kwa yale yanayofungamana na mahusiano ya kijamii na kiuchumi na kuishi na wasio kuwa waislamu.

**6. Mwanawake.** **154**

- Mwanamke na haki zake katika Uislamu.
- Je Mtume ﷺ aliweka yeye Sharia ya kuoa wake wengi au alikuja na sheria ya mbinguni ya kuweka utaratibu wa kuoa wake wengi? Kwanini Mtume ﷺ alioa mke mmoja tu kwa muda wa miaka 25 kisha baada ya hapo akaoa mke zaidi ya mmoja?

**7. Haki za binadamu.** **176**

- Uhuru na uadilifu na kulinda haki katika Uislamu.
- Mafundisho ya Mtume ﷺ kwa yale ≠≠yanayohusiana na vita na kuishi na wengine.

**8. Mazingira.** **188**
• Kuhifadhi mazingira na kuwahurumia wanyama na ufahamu wa nyama halali. Mafunzo ya Mtume kwenye mambo yanayohusiana na kuimarisha dunia na kuongeza hadhi chanya kwa mazingira na kuzitumia vyema rasilimali.

**9. Muujiza.** **198**
• Kwanini inazingatiwa Qur-an tukufu kuwa ni muujiza wa milele? na upi ukweli wa kisayansi ambao Qur-an imeutaja kabla ya kuvumbuliwa elimu ya kisasa?
• Vipi utahakikisha kuwa Qur-ani Tukufu ni maneno ya Allah na ujumbe wake ni kwa wanadamu wote.
• Vipi umekua ujumbe wa Allah ni kwa wanadamu wote na upo kwa lugha ya kiarabu?

**10. Hadithi za Mtume.** **212**
• Miongoni mwa maneno ya Mtume Muhammad ﷺ na hadthi zake tukufu.
• Mafunzo ya Mtume kwa yanayohusiana na vyakula na vinywaji na namna ya Miujiza ya Matibabu ilivyo ndani yake.

**11. Mwisho.** **226**

**12. Sanaa za Usanifu na khati za Kiislamu.** **232**
• Kiambatanisho cha kazi za wataalamu wa Sanaa na khati za Kiislamu kutoka mataifa mbali mbali duniani.
• Kiambatanisho cha picha za Misikiti muhimu na mambo ya kale na sehemu za kihistoria za Kiislamu kutoka mataifa mbali mbali ulimwenguni

**13. Rejea.** **294**

SURA

1

# USHUHUDAWAWASOMI (WANAFIKRA)



# USHUHUDA WA WASOMI (WANAFIKRA)

## Watu wakubwa mashuhuri walioacha athari ulimwenguni.

Katika utunzi wa kipekee wa kisomi kwa watu wakubwa mashuhuri walioacha athari katika ulimwengu. Amelinganisha msomi wa Kimarekani Michael Hart kati ya watu wakubwa mashuhuri miongoni mwa watu wakubwa katika historia, na ilikua jambo la kushangaza kwamba yeye alimteuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kuwa wa kwanza katika orodha ya watu wakubwa mashuhuri katika historia.

> *Naamini uwezo wa kipekee uliokusanya baina ya athari za kidini na kidunia kwa namna iliyo wazi kabisa, yote hayo yalimuandaa Muhammad kuwa mtu mkubwa zaidi katika kuathiri katika historia ya binadamu*
>
> *Michael Hart.*

Na amebainisha Michael Hart kwamba watu wengi aliowataja katika kitabu chake walipata bahati ya kuzaliwa katika vituo vya Ustaarabu katika ulimwengu, ndani ya Mataifa yenye Tamaduni za juu na mambo makubwa. Lakini Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alizaliwa katika mazingira ya Kibeduwi yaliyoduni na katika eneo lililombali na Vituo vya Ustaarabu na Tamaduni na Elimu.

Michael Hart amesema katika kitabu chake kwamba Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) pamoja na ukuwaji wake wa maisha ya duni lakini aliasisi moja ya dini kubwa katika ulimwengu na alikuwa kiongozi wa kisiasa mwenye kuathiri sana.

---

Dr. Michael Hart ni Myahudi wa Kimarekani amezaliwa mwaka 1932, nae ni msomi wa Elimu ya Anga, Hesabu na Professor wa Kanuni na Sayansi ya Computer na Fizikia. Amefanya kazi akiwa ni mtafiti katika kituo cha Anga cha Marekani (NASA) kabla ya kuhamia mji wa Texas ili afanye kazi akiwa ni Profesa katika chuo cha Tariniti katika mji wa San Antonio. Alipenda masomo ya Historia na ametunga kitabu maarufu akakiita "Majina mia: Utunzi wa watu wakubwa zaidi katika kuathiri ulimwengu".

Na baada ya kupita zaidi ya karne kumi na tatu tokea kufariki kwake, hakika athari zake hazijaacha kuwa ni zenye nguvu na zenye kuenea kwa upana. Na naona Michael Hart anaamini kwamba kuathiri kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) katika Uislamu kulikuwa kukubwa zaidi kuliko mkusanyiko wa uathiri wa Nabii Issa na Mtakatifu Bolis katika Ukiristo, na kwamba kila mmoja kati ya Mtume Muhammad na Nabii Issa (rehema na amani ziwe juu yao) walikuwa na uathiri wa kidini wenye kukaribiana katika ulimwengu.

## Kiongozi bora mkubwa

Na miongoni mwa watu waliozungumza kwa uwazi na haki kuhusu Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ni mwandishi na mwanasiasa wa Ufaransa maarufu Alvance Delamartin, hakika ameeleza ubora wa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kuwazidi watu wakubwa wengine kwa maneno haya machache

> "Ikiwa utukufu wa malengo na uchache wa uwezo na ukubwa wa matokeo ndio vipimo vitatu vya kupimia ukubwa (utukufu) wa watu, basi nani anayethubutu kumlinganisha Muhammad na yoyote yule miongoni mwa watu wakubwa katika zama zetu na".

Na akaashiria kuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) hakukusanya silaha kwa ajili ya kuleta ufalme au nguvu ya kiuchumi lakini aliathiri Nafsi, Fikra na Itikadi. Na kutoka katika Wahyi wa kitabu cha Mungu, kila neno ndani ya kitabu hicho ikawa ndio kanuni. Alianzisha Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) umma wa kiroho uliojumuisha mataifa kutoka kila kabila na lugha katika Ulimwengu.

Na akaongeza kwamba Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amefaulu katika kudhoofisha itikadi potofu zilizokuwa baina ya Muumba na Viumbe na kurejesha utulivu na busara kwa dhana ya Uungu katika mazingira ya machafuko ya kupenda mali na kuabudu masanamu na akaleta mapinduzi ya kifikra na ustaarabu uliofikia athari zake kila sehemu ya Ulimwengu.

Muhammad ﷺ... Mtume wa zama zetu.

Ametaja mwandishi wa Kiengereza Karen Armstrong katika kitabu chake

**"Muhammad ni Mtume wa zama zetu".**

"Sisi Inatupasa tusome historia ya Muhammad kwa njia ya lengo na ya usawa ili tupate kuthamini mafanikio yake na tutoe ndani yake mafunzo na mazingatio ambayo tunafaidika nayo katika zama zetu hizi".

Hakika Mtume Muhammad ﷺ amebeba ujumbe wa mbinguni na ameweza kuyaunganisha makabila ya Kiarabu ambayo yaliishi katika vita vikali kwa muda mrefu.

Na ili tujiepushe na majanga ya vita kati ya ulimwengu wa Kiislamu na kimagharibi basi inatupasa tujifunze kuelewana na kuthaminiana baina yetu na sio kuzipuuza tofauti zetu bila ya kuzipatia ufumbuzi. Na hakuna shaka kwamba nukta bora ya kuondokea ni utu na historia ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake).

# USHUHUDA WA WASOMI KWA MTUME (S.A.W) ﷺ



## John Adair

Mtaalamu wa Kiingereza katika elimu ya uongozi na mtunzi wa kitabu "Uongozi wa Muhammad", ni mkuu wa Kitengo cha uongozi katika umoja wa Mataifa.

"Kupitia kusoma kwenu hizi karatasi nataraji mtahukumu wenyewe namna ya upeo wa Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kuwa na sifa za kiongozi wa kupigiwa mfano ambazo zinawafikiana na ufahamu wa kisasa wa Asili na utendaji wa uongozi, na zinalingana na ufahamu wa Viongozi wa kupigiwa mfano ambao walitumikia watu wao kwa ukweli na wakawa watu wa maono na malengo".



## William Montgomery

Mwanahistoria wa Scotland na Profesa wa Tafiti za mambo ya Kiarabu na Kiislamu katika chuo kikuu cha Edinburgh (1909-2006).

"Hakuna mtu katika watu wenye historia kubwa asiyefanyiwa uadilifu na watu wa Magharibi na kutothaminiwa kama inavyopasa kama Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake). Hakika maandalizi yake ya kujitoa muhanga kwa ajili ya kufikisha ujumbe, na ukweli wa Masahaba zake na kuamini kwao Utume wake, na kujipamba kwao na tabia nzuri, na uwezo wao wa kuleta matokeo makubwa ili yaakisi ukamilifu wa nyenzo za kuathiri na uongozi katika nafsi ya Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake)".



## Mahatma Gandhi

Miongoni mwa viongozi maarufu wa kiroho na kisiasa katika historia ya India (1869-1948)

"Nilitaka kujua sifa bora za Mtume wa Uislamu Muhammad, mtu ambae anatawala nyoyo za mamilioni ya watu bila ya kupata upinzani. nikawa mwenye kutosheka zaidi kuliko siku zote zilizopita, uhalisia uliopo ni kuwa sio upanga ndio umehakikisha kukubalika kwa Uislamu katika maisha ya watu zama hizo, bali hali ya kawaida ya uhalisia kwa nafsi ya Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na kwa kujiepusha na masilahi yake binafsi, na kuheshimu kwake kukubwa kutimiza ahadi, na nia yake safi kwa Masahaba na wafuasi na ujasiri na ushujaa wake na kumuamini kwake Allah na kuamini Utume wake".



## Alphonse de Lamartine

Mwanafalsafa na mshairi wa Kifaransa mtunzi wa kitabu "Historia ya Uturuki" (1790-1869) ambae amezungumzia katika moja ya mada zake kuhusiana na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake).

"Ni Mwanafalsafa, muhadhiri, mrekebishaji, muwekaji sheria na mpiganaji. Amesahihisha fikra na kunyoosha itikadi za kifikra, mtu wa ibada pasina shaka na mwanzilishi wa utawala unaosimamia msingi mmoja wa kiroho, hakika huyo ni "Muhammad", na kwa mujibu wa vipimo vya utukufu wa kiutu, mtu atakavyokuwa na malengo ya juu na uwezo wa kawaida na matokeo makubwa, hivyo ndivyo vipimo vya ukubwa wa watu. Basi nani anathubutu kumlinganisha mkubwa yeyote wa zama hizi na Muhammad".



## Willium Durant

Mwanahistoria na Mwanafalsafa na Mwandishi. Mtunzi wa kitabu: "Kisa cha Ustaarabu" (1885-1981).

"Jina lake linamaanisha "mwingi wa sifa" na imekuja maana hii katika maelezo ya Injili ikitoa habari ya ujio wake, haijafahamika kuwa Muhammad aliwahi kuandika kitu kwa mkono wake, isipokua huko kutokujua kusoma kwake na kuandika haikuwa kizuizi kwake kunukuu Qur-an ambayo ni fasaha zaidi kuliko vitabu vyote vya lugha ya kiarabu, pia kutokusoma kwake hakujamzuia kupata uwezo wa kuwaongoza watu, mambo hayo ni mara chache sana kukusanyika kwa watu wengi kielimu".



## Yohann Wolfgang Goethe

Ni miongoni mwa wanalugha na wana mashairi na waandishi maarufu nchini Ujerumani (1749-1832).

"Muhammad hakua mshairi bali alikuwa Mtume, kwahivyo ili tuwe waadilifu lazima tuichukulie Qur-an kuwa ni kitabu cha mbinguni na wala sio kitabu cha mashairi ya kujiliwaza".



## Thomas Carlyle

Mwanahistoria na mwanafalsafa wa Kiengereza na mtunzi wa kitabu "Mashujaa na ushujaa katika historia". (1795-1881).

"Iweje kwa mtu mmoja pekee kuyayusha makabila yenye kupigana, na watu wa majangwani wenye kuhamahama akawafanya umma mmoja wenye nguvu na Ustaarabu chini ya miongo miwili?".



## Mchungaji R. Bosworth Smith

Katika kitabu chake "Muhammad na wafuasi wake".

"Alikuwa kiongozi wa nchi na kiongozi wa dini, alikuwa Papa "Pop" bila ya kuutaka na alikuwa mfalme bila ya jeshi, hakuwa na jeshi wala walinzi binafsi wala Ikulu na wala hakuwa na pato maalumu. Na kama kuna mtu anahaki ya kusemwa kuwa alikuwa anahukumu kwa kupitia maamrisho ya kimungu basi huyo ni "Muhammad" (rehema na amani ziwe juu yake), alikuwa na nguvu pasi na kutumia nyenzo za nguvu wala njia za kumpatia nguvu, hakujali aonekane ana nguvu au hana, wepesi wa maisha yake binafsi unaendana na maisha yake kijamii".



## Leo Tolstoy

Mwandishi na mtunzi wa Urusi maarufu na mtunzi wa kitabu “Vita na Amani” (1828-1910)

“Hakika miongoni mwa mambo yasio na shaka ndani yake kuwa Muhammad alikuwa ni mmoja wa warekebishaji wakubwa, ameongoza umma wake na ameutoa katika migogoro mibaya na kutofautiana na kuupeleka katika amani na umoja na kutoka maisha ya kizamani na ya kawaida kuelekea katika Ustaarabu ambao ulifunguwa milango ya mafanikio na ustawi kwa umma, na hayo hayakupatikana kwa Waarabu kabla ya Uislamu. Hakika hii ni kazi kubwa na tukufu hawezi kusimamia kazi hiyo isipokuwa mtu mkubwa na mwenye kustahiki kuheshimiwa na kuthaminiwa".



## Maurice Bucaille

Daktari na mpasuwaji wa Kifaransa, maarufu na mtunzi wa kitabu “Injili na Qur-an na Sayansi”. Alisimamia uchambuzi wa mwili wa Firauni wa Misri baada ya kuuhamisha kutoka Misri kwenda Ufaransa katika zama za raisi aliyefariki Frausou (1920-1998).

“Nimeisoma Qur-an kwa kina na kwa moyo mkunjufu bila ya kuwa na hukumu iliyotangulia, kwa hakika ilinishangaza kulingana aya za Qur-an ambazo zimeelezea mada mbali mbali na vitu vinavyo endana na elimu ya zama hizi, na tukiangalia daraja ya utambuzi katika zama za Muhammad basi haiwezekani kuzingatia uhakika wa kisayansi ambao umekuja katika Qur-an kwamba ni utungaji wa mtu. Vipi inawezekana kwa binaadamu asiyejuwa kuandika wala kusoma kuweka wazi mambo ya kisayansi pasi na kuonekana kwenye maelezo hayo kosa japo dogo?”.


صلى الله عليه وسلم








اقرا باسم ربك
الذى خلق
خلق الانسان
من علق
غار حراء







Neno hili "**Muhammad**" amelichora mchoraji Farid Al-Aliy katika mkusanyo wake aliouita (**Muhammadiyyati**).

Na inadhihiri katika jina hilo herufi (haa) kama Kuba la Msikiti lilotimia kujengwa kwake kutokana na maneno "Muhammad Rasulullah".

Na unauzunguka picha ya umbo hili uzio wa pembe sita pia wenye kuundika kutokana na neno "Muhammad", limekamilika kuandikwa kwake kwa njia ya kiuhandisi mzuri na mfumo wa kisanaa unaopendeza.

Na neno "Muhammad" katika lugha ya kiarabu linamaanisha mtu

ambae watu wanamsifia na kumshukuru kwa wingi.

Yeye basi ndie ambaye wanamtaja watu kwa sifa nyingi kwa matendo yake mazuri na tabia zake zenye kupendeza

na huyo ndie mtu ambae anastahiki sifa kila wakati".

SURA

2

# SIFA ZA MTUME NA WASIFU WAKE (S.A.W) ﷺ



Picha hii Inaitwa “Al-Hilyatun-Nabawiyyah” yaani "Pambo la Mtume" ndani yake kuna sifa za Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake), na baadhi ya wasifu wake. Ni kawaida ya waandishi wataalamu wa khati za Kiarabu huandika hivyo kwa ajili ya kuonesha uwezo wao wa kuzipendezesha khati za Kiarabu. Miongoni mwa kazi za mwanakhatti wa Kihispania Nuria Garcia Masip

# SIFA ZA MTUME NA WASIFU WAKE (S.A.W) ﷺ

Waislamu wanaamini kuwa ni haramu kuwachora Mitume wa Allah Mtukufu kwa lengo la kuwatukuza na kuwaadhimisha nafasi yao iliyofungamana na Muumba wa ulimwengu, kwa hivyo hakuna kwa waislamu picha au michoro inayodhihirisha muonekano wa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ﷺ wala hakuna picha za Mitume na wajumbe wa Allah waliotangulia kabla yake, lakini historia ya Kiislamu imesheheni mapokezi ya hadithi zilizothibiti kwa njia ya "Mutawatir" (wapokezi walio wengi wasioweza kusema uongo) ambazo zimesimulia sifa za Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ﷺ za kimaumbile na kitabia kwa umakini na umahiri mkubwa.



## Wasifu wake na muonekano wake Mtume (S.A.W) ﷺ

Alikua Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ﷺ na ngozi nyeupe iliyoelemea kwenye wekundu, alikua mzuri wa sura, mtu anayemuona hutishika kwa haiba yake na humtukuza na kumheshimu, na anaetangamana nae anampenda. Uso wake ulikuwa unameremeta kama mwezi kama walivyomsifu Masahaba zake, na alikuwa na kipaji kipana na macho makubwa makunjufu.Macho yake ni meusi na nywele zake ni nyeusi ndani yake zimo nywele nyeupe hazikua laini wala ngumu zenye kusokotana na ndevu zake ni nyingi.

Hakuwa mfupi wala mrefu bali alikuwa na urefu wa kati na kati hakua mnene na hakuwa na tumbo kubwa bali tumbo lake lilikua usawa wa kifua chake, kifua chake kilikuwa kipana, mwenye nguvu za mwili, akitembea kwa nguvu na uchangamfu, akinyanyua miguu yake na wala haiburuzi ardhini, na anapogeuka nyuma kwa ajili ya mtu anageuka mwili mzima.

## Tabia na Dhati ya Mtume (S.A.W) ﷺ

Alikua mtulivu wa tabia na mwepesi katika kuamiliana na watu, hakua jeuri wala mgumu wa moyo, alimsifu Anas bin Malik (radhi za Allah ziwe juu yake) ambae alimtumikia kwa muda wa miaka kumi, Kwamba alikuwa ni mwenye tabia nzuri zaidi na hakupatapo kusema aah!. Ilikuwa kucheka kwake ni kutabasamu na akifanya mzaha kwa Masahaba wake na hakusema isipokua ukweli. Na hakuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) mwenye maneno machafu wala kujifanya na tabia mbaya, kwa maana hajikalifishi wala kukusudia kusema machafu wala kufanya vitendo vichafu, pia hakua akisema kwa sauti ya juu kwa kupiga makelele bali alikua ni mwenye kupendeza na tabia iliyo sawa. Mtume (S.A.W)z

## Sifa ya maneno yake Mtume (S.A.W) ﷺ

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) hakuwa akisema sana, lakini anapozungumza huzungumza kwa kufupisha na ufasaha, na anapotoa msisitizo juu ya jambo hurudia mara tatu alikua ni mkweli na hasemi isipokua haki, alichukia mijadala na hakuwa mwenye kutia aibu jambo wala hakuwa mwenye kusifu mambo bila ya haki. Hakuwa akizungumza isipokuwa anayotaraji malipo kutoka kwa Allah mtukufu na hataraji isipokuwa radhi za Allah mtukufu. Na amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akiwafundisha Masahaba wake:

> "Mimi ni mwenye kuchukua dhamana ya nyumba kandoni mwa pepo kwa atakaeacha mijadala hata akiwa mkweli na mwenye haki, na nyumba kati kati ya pepo kwa atakaeacha uongo hata kama ni mzaha, na nyumba juu ya pepo kwa mwenye tabia njema".
>
> Amepokea Abu Dawd (4974/4800), na Twabarany katika "Al-Kabiir" (8/98), na ameisahihisha Imam Nawawy katika kitabu "Riyadhu-Saalihiin".

## Hali ya hisia na huruma zake Mtume (S.A.W) ﷺ




Hakuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) mwenye hali ya ukali bali alikuwa mara nyingi anawausia Masahaba wake kuwa wapole na kujiepusha na hasira, isipokua kwa yale yanayofungamana na ukiukwaji wa sharia za Allah mtukufu, basi hakuwahi kukasirika kwa ajili ya nafsi yake hata kidogo. Na ameelezea Bibi Aisha mke wa Mjumbe wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) kuwa yeye Mtume hakupatapo kumpiga yeyote kwa mkono wake isipokua anapokuwepo katika jihadi katika njia ya Allah, wala hakumpiga mtumishi wala mwanamke na alikua halipizi ubaya kwa ubaya lakini akisamehe na kuvumilia.

## Muamala wake na watu Mtume (S.A.W) ﷺ

Alikuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akiwatangulia watu kutowa salamu, na akiwafundisha Masahaba wake kuwa kutabasamu mbele ya wengine ni sadaka, na hakukhiyarishwa kati ya mambo mawili isipokua akichagua jepesi ikiwa sio katika madhambi.

Alikuwa haingilii lisilomuhusu, alikua na upendo na mkweli anapoamiliana na watu, alipofanya biashara walimtambua watu kwa jina la Mkweli Muaminifu.

Akikaa vikaoni hukaa pale anapoishia mtu wa mwisho bila kusongamana na yeyote, na alikuwa anamsikiliza yule anayemzungumzisha, basi hakuwa akimkatisha mtu anayezungumza nae mpaka amalize, alikua ni mtu mwenye haya sana na hakuwahi kufanya vitendo vya kuaibisha.

## Mtindo wa maisha yake Mtume (S.A.W) ﷺ

Hakuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ﷺ mbadhirifu wala hakuwa bakhili bali alikua ni mtu wa katikati na mnyenyekevu katika maisha yake yote, hakupenda kula sana na hakupatapo kukitia kasoro chakula, na hakupatapo kushiba kwa kula mikate ya Shayiri siku mbili mfululizo mpaka kufa kwake, alikua anakula kwa mkono wa kulia, akiramba vidole vyake na akimshukuru Allah baada ya kumaliza kula.

Alikuwa kama watu wengine akijishughulikia mwenyewe akimkama maziwa mbuzi wake na akiwa nyumbani kwake akiutumia muda wake kuwasaidia wake zake.

Alipenda usafi na kuvaa nguo nzuri bila ya kujikalifisha akipenda manukato yenye harufu nzuri na akipaka wanja kwenye macho yake.

Alipenda kubakia kwenye mswala wake baada ya Sala ya Alfajiri ili asome Qur-an na kumdhukuru Allah mtukufu mpaka jua lichomoze na kupanda kidogo, akisimama usiku kila siku na ikitokea kulala na kuikosa ada yake akisali muda wa mchana.

Na imepokewa kutoka kwa Bibi Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake) amesema: "Alikuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ﷺ anasimama usiku mpaka inavimba miguu yake, nikamwambia: Kwanini unafanya hivi ewe Mjumbe wa Allah na ushasamehewa makosa yako yaliyopita na yajayo? Akasema:Basi nisiwe mja mwenye kushukuru?".

Amepokea Bukhari na Muslim.

Alikuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ﷺ mkarimu akitoa kwa kuwapa watu utoaji wa mtu asiyeogopa ufakiri, lakini hakuwa yeye wala jamaa zake wakichukua mali ya Zaka na hakuridhishwa kwa yeyote katika watu wake wa karibu kuwa ni mkusanyaji wa mali ya Zaka miongoni mwa Waislamu.

Nyumba yake ilikuwa ndogo iliyojengwa kwa udongo na kuezekwa kwa makuti ya mtende na ngozi za ngamia na alikuwa akisema (rehema na amani ziwe juu yake):

> "Wapi na wapi mimi na dunia? Naapa kwa Mola wangu haikuwa mfano wangu na dunia isipokua ni mfano wa mwenye kipando aliyesafiri siku ya joto kali akaamuwa kupumzika chini ya mti kwa muda mchache mchana kisha akaondoka na kuuwacha mti ule".
>
> Amepokea Ahmad katika "Musnad" yake (2/666) namba (2788) kutoka kwa Anas bin Malik

Picha ya kubuni ya Msikiti wa Mtume (rehema na amni ziwe juu yake) ambao ulijengwa mara tu baada ya kufika kwake katika mji wa Yathriba, na ilikua nyumba yake ipo upande wa kusini mwa Msikiti.



SURA

# 3

# MAISHA NA SIRA YAKE Muhammad (S.A.W) ﷺ





# MAISHA NA SIRA YAKE Mtume (S.A.W) ﷺ

Maelezo mafupi ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake).

| | |
|---|---|
| **Jina** | Muhammad (S.A.W) ﷺ |
| **Jina la baba** | Abdallah bin Abdul Mutwalib (inafikia nasabu yake hadi kwa Mtume Ismail mtoto wa Mtume Ibrahim (rehema na amani ziwe juu yao) |
| **Jina la ukoo** | Yeye ni Bani Hashim nalo ni kabila lenye hadhi kubwa Bara Arabu. |
| **Tarehe ya kuzaliwa** | Tarehe 20 au 22 - April 570 AD (9 au 12 Rabiil Awwal mwaka wa Tembo). |
| **Pahala alipozaliwa** | Mji Mtukufu wa Makka katika bara Arabu (Saudi Arabia kwa sasa). |
| **Tarehe ya kufariki** | June 632AD (12 Rabiul Awwal mwaka wa 11 AH- alikua na miaka 63 takriban). |
| **Pahala alipofariki** | Mji wa Madina - kilomita 400 kaskazini ya mji mtukufu wa Makka. |






## Maelezo mafupi ya Mtume (S.A.W) ﷺ

| | |
|---|---|
| **Tokea kuzaliwa kwake hadi kufika miaka 2** | Alikufa baba yake kabla ya kuzaliwa kwake, mama yake alimpeleka nje ya Makka kwa mnyonyeshaji anayeitwa Bibi Halima Saadiyya kama ilivyokuwa desturi ya Waarabu kwa wakati huo |
| **Tokea miaka 2 hadi miaka sita** | Aliishi na mama yake Bibi Amina mpaka alipokufa mwaka 576 AD |
| **Tokea miaka 6 hadi miaka 8** | Aliishi na babu yake Bwana Abdul-Mutwalib hadi alipofariki babu yake |
| **Tokea miaka 8 hadi miaka 25** | Aliishi na Ami yake Bwana Abu-Twalib, na alikuwa ni baba wa watoto kumi |

## Kujifunza Kwake Mtume ﷺ

• Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa hajuwi kusoma wala kuandika, hakuishi nje ya Makka wala haikutokea kwenda kusoma nje ya nchi.

• Alipofika umri wa miaka 40 alipokea Qur-an kwa njia ya Wahyi kutoka kwa Mola wa viumbe alimshukia Malaika Jibril (amani iwe juu yake) akamsomesha Qur-an Mtume akaihifadhi na akaifikisha kwa watu kama ilivyo bila ya kupunguza wala kuongeza.

• Yamekusanywa maneno ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na mafundisho yake katika vitabu vinavyoitwa "Vitabu vya Sunna za Mtume mtukufu" ambavyo vimetofautiana na Qur-an maneno yake na muundo wake.

## Maisha yake ya kikazi Mtume (S.A.W) ﷺ

| | |
|---|---|
| **Tokea utoto wake hadi miaka 25** | Alichunga mbuzi kisha akafanya biashara na Ami yake Bwana Abu-Twalib, Ulikua Umri wake miaka 12 wakati alipoambatana na Ami yake kwa mara ya kwanza kufanya biashara kuelekea mji wa Shamu |
| **Tokea miaka 25 hadi mwaka 40** | Alifanya biashara ya mwanamke mwema na tajiri anayeitwa Bibi Khadija bint Khuwaylid, alijulikana Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na amani ziwe juu yake kwenye jamii yake kwa ukweli na uaminifu na kupewa lakabu "Mkweli mwaminifu" |
| **Tokea miaka 40 hadi miaka 63** | Alipofikia umri wa miaka 40 (mwaka 610 AD takriban) alimshukia Malaika Jibriil (amani ziwe juu yake) na kumpa ujumbe wa Unabii hapo akajitolea maisha yake kufikisha ujumbe wa Allah na kitabu chake (kwa jamaa zake na watu wote) ili iwe ndio katiba ya maisha na yenye kuhakikisha kupatikana kwa uadilifu wa kijamii na amani na kheri kwa viumbe wote, amesema Allah Mtukufu: "Na hatukukutuma isipokua ni rehema kwa Walimwengu" |



## MAISHA YA KIFAMILIA YA MTUME ﷺ

**Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alioa mke mmoja kwa muda wa miaka 25.**

Bibi Khadija bint Khuwaylid alikuwa mjane kutoka ukoo mtukufu wa Banii Asad alikua ni mwanamke mwenye heshima katika jamii yake, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alifanya biashara ya mwanamke huyo, basi Bibi khadija alipomkuta na tabia njema, mtiifu, muwazi na muaminifu katika kuamiliana na watu alimtaka amuoe (kupitia mtu mwengine) na hapo ndoa ikatimia.

### Ndoa ya mafanikio

Licha ya kuwa Bibi Khadija alikua mkubwa zaidi kuliko Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kwa miaka 15 kupitia mapokezi mengi mashuhuri lakini walilingana kwa kutoka matabaka mawili ya kijamii yenye kufanana.

Na wala haikua tofauti yao ya umri ni kizuizi mbele ya kuanzisha familia na kuzaa watoto chini ya kivuli cha ndoa yenye mafanikio na iliyotulia na kutawaliwa na mapenzi ndani yake na uaminifu, Iliendelea ndoa ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na Bibi Khadija (radhi za Allah ziwe juu yake) kwa miaka 25 mpaka alipofariki Bibi Khadija mwaka 619 AD.

### Baba wa watoto sita

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alipata watoto kwa Bibi Khadija (radhi za Allah ziwe juu yake) wanne wanawake nao: Zainab, Ruqayyah, Ummu Kulthum, na Fatma, na watoto wawili wanaume nao: Qasim ambae alikufa akiwa na miaka mitatu na Abdullah ambae alikufa akiwa na miaka minne.

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alimsifu Bibi Khadija kwamba ni:

Bibi mtukufu kuliko wanawake wa zama zake mfano wa Bibi Maryam (juu yake amani).

Amepokea Imamu Ali bin Abi Talib (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba alimsikia Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akisema: “Mbora wao (Bani Israil) katika wanawake ni Bibi Maryam bint Imran, na mbora wao (Umma huu) katika wanawake ni Bibi khadija bint Khuwaylid".

Amepokea Bukhari (2815)

## Mume mwenye Mapenzi na Mwaminifu

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa akimpenda mke wake Bibi Khadija alikuwa mkweli kwake na kwa watoto wake, aliutumia muda wake pamoja na familia yake akiwashughulikia watoto wake na kumsaidia mke wake majukumu mbali mbali ya nyumbani.

Picha inaonesha makaburi ya Baqii ndani ya mji Mtukufu wa Madina ambako wamezikwa baadhi ya watoto wa Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) na baadhi ya wake zake na jamaa zake na Masahaba zake.



Makaburi ya Mualla ndani ya mji Mtukufu wa Makka, amezikwa humo Bibi Khadija bint Khuwaylid (radhi za Allah ziwe juu yake).

# MTUME MUHAMMAD (S.A.W) ﷺ

## ANAFIKISHA UJUMBE KWA MUDA WA MIAKA 23

### Mwaka 610 AD

### Kuanza kwa Utume.



Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ﷺ amepokea Wahyi akiwa amejitenga anamuabudu Mola wake ndani ya pango la Hiraa katika Jabal Nuur lililokuweko Makka.

Na siku hio alimshukia Malaika Jibril (amani iwe juu yake) na jambo la Mungu ili kuanza kazi ya kufikisha ujumbe wa Allah kwa viumbe wote. Allah alimtuma Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kuwa mjumbe kwa jamaa zake na kwa watu wote kuwalingania kumuamini Allah aliyetakasika ambae hapana Mola apasae kuabudiwa isipokua yeye na kuukubali ujumbe wake. Ujumbe huo ni ujumbe ambao inahitajia kuufikisha kwa imani ya kweli na ikhlasi ya hali ya juu na kulazimiana nayo kwa umadhubuti na amana iliyokamilika.

### Mwaka 610 – 612 AD

### Waislamu wa mwanzo

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliwalingania jamaa zake na marafiki zake wa karibu wamuamini Allah na ujumbe wake, basi akamuamini mke wake Bibi Khadija bint Khuwaylid na rafiki yake Abu Bakar Asswiddiiq na mtoto wa ami yake Ali bin Abi Twalib na Zaid bin Haritha (muachwa huru au mtumishi wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) radhi za Allah ziwe juu yao. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliendelea na Masahaba zake kumlingania mtu mmoja mmoja kwa ajili ya Allah bila ya kulidhihirisha jambo hilo kwa muda wa miaka mitatu,

waliamini katika kipindi hicho mafakiri na matajiri na watu bora miongoni mwa wanaume na wanawake na watumwa, na miongoni mwa watu muhimu walioamini katika kipindi hiki ni Othman bin Affan, Zubeir bin Awwam, Abdulrahman bin Awf, Ammar bin Yasir, Said bin Zaid na mke wake Fatma bint Al-Khatwab (dada yake Omar bin Al-Khatwab) radhi za Allah ziwe juu yao.

## Mwaka 613-615 AD

### Viongozi wa kikuraishi wanapambana na Uislamu



Baada ya miaka mitatu ya ulinganiaji wa mtu mmoja mmoja Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) yeye na Masahaba zake walianza kuwalingania watu kwa dhahiri kumuamini Allah pekee na kupokea ujumbe wake na kuacha kuyaabudu masanamu, lakini viongozi wa kikuraishi hawakuukubali wito wa Mtume (rehema na mani ziwe juu yake) na wakamtuhumu kuwa ni mshairi, mchawi, na mwendawazimu, pamoja na kuwa alikuwa maarufu kwao kwa sifa za Ukweli na Uaminifu na mwenye hekima.

### Hadaa na vitisho.

Viongozi wa kikuraishi walijaribu kumuondoa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwenye ulinganiaji wake wa Uislamu mara kwa hadaa na mara nyengine kwa vitisho na wakajaribu kuwazuia watu kumsikiliza na wakadhihirisha zaidi uadui kwa aliyeingia katika Uislamu, wakawatesa mafakiri na wanyonge na watumwa na kuwaua baadhi yao na wakamfanyia maudhi Mtume (rehema na amani ziwe juu yake).

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anawatia nguvu Masahaba zake

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa akiwahimiza Masahab zake kufanya subira na uvumilivu, na aliendeleza kukutana na Masahaba zake kwenye nyumba ya Arqam bin Abii Arqam Makhzumi iliyokua kama Chuo cha kuwafundishia Masahaba zake Qur-ani inayoshuka kwake kwa mfululizo, aidha aliwafundisha maadili na tabia njema na akawajaza hisia za kubeba majukumu na kulazimiana na ufikishaji wa ujumbe wa Allah mtukufu kwa watu wote.

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alipoona yale yanayowafika Masahaba zake miongoni mwa unyanyasaji na vitisho na kuadhibiwa aliwaruhusu baadhi yao kuhama kuelekea Uhabeshi (Ethiopia ya sasa) ambapo alikua Mfalme wake muadilifu anayejulikana kwa jina la Najashy

Na katika kipindi hiki waliingia katika Uislamu watu wawili miongoni mwa watu wa Makka wenye nguvu nao ni Sahaba Omar bin Khatwab na Sahaba Hamza bin Abdul-Mutwalib ami yake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na ikawa jambo hilo ni ishara muhimu katika ulinganiaji wa Uislamu.

## Mwaka 616 – 617 AD

### Kuwekewa vikwazo mtume (rehema na amani ziwe juu yake) vya kiuchumi na kijamii

Viongozi wa kikuraishi waliendelea kufanya mazungumzo na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ili awache kulingania Uislamu lakini msimamo wake Mtume ulikua thabiti kwa kua amebeba Ujumbe wa Allah kwa watu wote, hivyo ikawa hakuna namna ya kuwepo makubaliano ili aiwache haki. Baada ya hapo viongozi wa kikuraishi wakaamua kuweka vikwazo vya kiuchumi na vya kijamii kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) pamoja na waliomuamini. Hali hii ilidumu kwa miaka mitatu waliwazuia watu kuchanganyika na Waislamu na kuuziana nao, kwa hali hiyo alipata shida sana Mtume (rehema na amnai ziwe juu yake) na Masahaba zake, kilikua kipindi kigumu mno kwa Waislamu lakini walivumilia na kushikamana na dini yao.

## Mwaka 619-620 AD

### Mwaka wa huzuni

Mwaka 619 AD Viongozi wa Makka walibadili kuweka vikwazo kwa Waislamu baada ya kuona hapana faida waliyoipata kwa vikwazo hivyo, lakini mwaka huo huo alikufa ami yake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) Bwana Abu Twalib aliyekuwa akimlea, kumhifadhi, na kumnusuru, na baadae akafariki mke wake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) Bibi Khadija bint Khuwaylid ambae alikua kipenzi chake na anae mnusuru na mwaminifu kwake, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alihuzunika sana na akawa amechoka na viongozi wa Makka kwa jeuri yao, basi akaelekea Taaif mji ambao uko kilomita 80 takriban kusini mwa Makka lakini watu wa Taaif walimfanyia uadui na maudhi na kumfukuza.

## Mwaka 620 – 622 AD

### Mwangaza wa matarajio



Msikiti wa Bay'a au Akabah, upo karibu na daraja la Jamarati kwa sasa

Licha ya usumbufu na tabu aliyopitia Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na Masahaba zake lakini aliendelea kulingania kumuamini Allah na kuamini Utume wake akiamini kuwa atapata nguvu na faraja kutoka kwa Mola wake.

Basi akautambulisha Uislamu kwa makabila tofauti ya Waarabu lakini hawakukubali isipokua watu wachache walioamini na kusilimu akiwemo Abu Dharr Al-Ghiffaariy na Attufailul- Duusiy na Dhamadul Azidy.

Kisha akatokea Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kukutana na watu sita waliofika kutoka mji wa Yathrib (Madina) katika msimu wa Hijja, na wakaazi wa Yathrib ni makabila mawili makubwa ya Waarabu Al-Aws na Al-Khazraj pamoja na baadhi ya makabila ya kiyahudi. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) aliwalingania watu hawa kumuamini Allah peke yake na akawaelezea Ujumbe wa Uislamu, walikua ni kutoka kabila la Khazraj na walikwisha sikia kutoka kwa Mayahudi kutoka Yathrib kuja kwa Mtume mpya, basi wote wakamuamini na ujumbe wake na wakaafikiana kwenda kuwalingania watu wao na kurejea Makka msimu wa Hijja ijao kuonana na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake).

**Waislamu wapya kutoka Yathrib waahidi kumfuata Mtume (rehema na amani ziwe juu yake).**

Bay'atul Aqabah

Lilirudi kundi hili la watu kutoka Yathrib mwaka uliofata (621 AD) wakiwa na watu wengine sita, baadhi yao kutoka kabila la Aws na wakakaa na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) wakazungumza nae wakamuamini na kuahidi kutomuabudu isipokua Allah peke yake bila kumshirikisha na chochote na hawatoiba, hawatozini hawatoua, wala hawatomuasi Mjumbe wa

Allah (rehema na amani ziwe juu yake). Makubaliano haya yalijulikana kwa jina la "Bay'atul – Akabatul-Uula" yaani Makubaliano ya mwanzo ya kutii yaliyofanyika Aqabah, na yalifanyika sehemu inaitwa Mina (sehemu ambayo Mahujaji hurembea mawe).

Walirejea watu hawa Yathrib wakawa wanalingania viongozi wa makabila ya Aws na Khazraj na wafuasi wao kuingia katika Uislamu, kisha walirejea tena Makka mwaka uliofatia wa msimu wa Hijja (622 AD) wakiwa zaidi ya watu 70 na wanawake wawili

Na wote wakamuahidi Mtume Muhammad (rehema na amni ziwe juu yake) kama walivyoahidi ndugu zao na kikaitwa kikao hiki "Bayatul-Aqabatu-thaniy" yaani makubaliano ya pili ya Aqabah, na ikawa ni muelekeo muhimu katika terekhe ya kulingania dini ya Allah.

### Jamii ya Kiislamu ya mji wa Yathrib ndipo wanapohamia Waislamu

Walikubali dini ya Uislamu viongozi wakubwa wa makabila mawili ya Aws na Khazraj katika mji wa Yathrib na kwa sababu hiyo waliingia katika Uislamu wengi wao au watu wote wa makabila hayo, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akawaruhusu Masahaba zake wa Makka kuhama kwenda Yathrib ili waende kuishi na ndugu zao wawe mbali na mateso ya viongozi wa kikuraishi.

### 622 AD (Mwaka wa kwanza Hijriya)

### Mipango ya viongozi wa Kikuraishi ya kumuuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na kuhamia kwake kwenda Yathrib.



Viongozi wa Kikuraishi waliogopa kuongezeka kwa wafuasi wa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na kuenea dini ya Uislamu katika Bara Arabu, basi wakaamua kumalizana nae, wakakubaliana kwenye kikao chao cha Daaru-Nadwa wamuuwe Mtume. Lakini Mtume (rehema na mani ziwe juu yake) na rafiki yake Sayyidna Abu Bakar Swiddiq walitoka Makka na kuelekea kwenye pango la "Thawr" wakakaa ndani yake kwa muda wa siku tatu kisha wakaondoka kuelekea Yathrib. Kwa hakika hijra ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) imeleta mageuzi makubwa katika tarekhe ya Uislamu. Ndani ya mji wa Yathrib uliimarika Uislamu na kupatikana nidhamu mpya ya kijamii na kuanza chimbuko la dola ya Kiislamu.

## Mwaka 623 – 624 AD.

### Waislamu wanamkubali Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika mji wa Madina

Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) aliungwa mkono kwa kusikilizwa na kutiiwa kwa yenye kufurahisha na yenye kuchukiza katika nafsi zao. Na watu wa Yathrib walikuwa ni mchanganyiko kati ya Waarabu na Mayahud.

Licha ya kuwepo makabila mawili makubwa (Aws na Khazraj) ndani ya mji wa Yathrib pamoja na kuwepo makabila matatu madogo ya Kiyahudi, Lakini jamii ya Kiarabu ndani ya Yathrib ni kubwa zaidi kuliko ya jamii ya Kiyahudi

### Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anabadilisha jina la Yathrib na kuiita Madina

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) aliuita mji wa Yathrib kuwa "Madina", na haukua tena Yathrib (baada ya kuhamia Mtume (rehema na amani ziwe juu yake)) kuwa mji wa Aws au Khazraj au Mayahudi bali ulikua ni mji wa kila waliomuamini Allah ukiongozwa na Mjumbe wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake). Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akauombea kwa Allah mji wa Madina uwe na baraka na aupendezeshe kwa Waislamu, na mara nyengine alisema: ''Hakika ya imani itapata nguvu katika mji huu wa Madina kama anavyopata nguvu nyoka katika shimo lake.'' Amepokea Bukhari na Muslim.

### Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anaanzisha jamii mpya Madina

Jambo la mwanzo alilolifanya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ndani ya mji wa Madina lilikuwa kujenga msikiti ili Waislamu wakusanyike kusali ndani yake na akawaunganisha udugu baina ya waliohama kutoka Makka na watu wa Madina ikaongezeka kuzoeana na kupendana kwao. Mtume ﷺ

akawalingania watu wa Madina kuudumisha umoja na mshikamano wa kijamii na akasema (rehema na amani ziwe juu yake): “Mtume alitaka kufungamanisha baina ya matendo haya na akaridhia Allah mtukufu kuwakusanya watu waishi kwa uadilifu na amani katika jamii ambayo yumo humo Muislamu na asiyekuwa Muislamu.

> “Enyi watu toeni salamu, na lisheni chakula na Salini usiku hali ya kuwa watu wamelala mtaingia Peponi kwa amani”.
> Amepokea Ibnu Maajah (1334) na Tirmidhiy (2485).

**Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anafunga mkataba wa mwanzo na Mayahudi ndani ya mji wa Madina,**

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alifanya makubaliano ya mwanzo ya maandishi yanayodhamini kuishi kwa amani kati ya Waislamu na Mayahudi na kuheshimu haki za pande mbili.

Mkataba umedhamini uhuru wa kufuata dini na kufanya ibada kwa Waislamu na Mayahudi, na kukubali kuwa Mayahudi wana dini yao na Waislamu wana dini yao, na kati yao wana haki ya kunasihiyana na kufanyiana wema, na uadilifu na kuwatetea waliodhulumiwa. Na ukatoa mkataba huo ulinzi na amani kwa kila mkazi wa Madina na kuzuia kuharibu mali za wengine na kuwataka watu wote kushirikiana katika kuulinda mji wa Madina pindi watavamiwa na maadui kutoka nje.

(Tazama kitabu cha Sira cha Ibnu Is-haka)



Ardhi ambayo vilipiganwa vita vya Badri

## 623 - 624 AD (Mwaka wa pili Hijriya)

### "Badr" Pambano walilolazimishwa Waislamu

Wakati Waislamu walipohama Makka kwenda Madina walilazimika wengi kuacha nyumba na mali zao ambazo ziliporwa na viongozi wa Kikuraishi wakazifanyia biashara na kuwazuwia kuondoka nazo.

Waislamu walijuwa kuwa msafara wa kibiashara wa viongozi wa Kikuraishi utapita karibu na mji wa Madina ukiongozwa na Abu Sufiyan, wakatoka kwenda kuzikomboa mali zao kutoka katika msafara huo. Abu Sufyan alipojuwa kutoka huko kwa Waislamu alibadilisha muelekeo wa msafara wake na akapeleka mjumbe kuwajuulisha Makuraishi. Wakatoka wakubwa wa kikuraishi na jeshi la kivita lifikalo watu 950 lililojiandaa kwa vifaa na silaha.

Na Waislamu hawakuwa wamejiandaa kwa vita wala mapambano na idadi yao haikuzidi watu 313 takriban, na hawakuwa isipokuwa na farasi wawili na idadi ndogo ya ngamia. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamuomba Mola wake maombi makubwa akinyenyekea ndani yake na kushikilia kumuomba Allah mtukufu na kumsifu.

Yakakutana makundi mawili eneo la Badri lililopo kusini magharibi ya Madina kwa umbali wa kilomita 155, ilikua siku ya Ijumaa tarehe 17 Ramadhan mwaka wa pili Hijria, na jambo la kuwashangaza Makuraishi na kutolitarajia ni kupatikana kwa ushindi kwa jeshi la Waislamu katika pambano la mwanzo tu, na kuuliwa idadi kubwa ya wakubwa wa Kikuraishi na wasaidizi wao katika pambano hilo kama Abu Jahli, Umayyah bin Khalaf na Waliid bin Utbah.



## 624-625 AD (Mwaka wa tatu Hijriya)

### Viongozi wa Kikuraishi wawavamia Waislamu katika vita vya Uhud

Viongozi wa Kikuraishi walijaribu kulipiza kisasi kwa kule kushindwa kwao katika vita vya Badri, na kuhofia kupoteza nafasi yao ya uongozi katika Bara Arabu, walikusanya jeshi la wapiganaji 3,000 kwa msaada wa makabila yanayowaunga mkono na wakalipeleka ili kuwapiga vita Waislamu.Na vikatokea vita karibu na jabali la Uhud kaskazini ya mji wa Madina na ilikuwa mwaka wa tatu wa Hijra. Mtume Muhamad (rehema na amani ziwe juu yake) aliamrisha kundi la warusha mishale wawepo juu ya jabali dogo ili kulinda jeshi la Waislamu kwa upande wa nyuma, lakini kushuka kwao na kwenda kinyume na amri ya Mtume (rehma na amani ziwe juu yake) na kujishughulisha kwao katika kukusanya ngawira ilimpelekea Khalid bin Walidi (alikuwa katika jeshi la kikuraishi) pamoja na jeshi lake kuwageukia Waislamu kutoka nyuma ya jabali.

Zilipanguka safu za Waislamu na wakapata hasara katika vita hivi, na akapata majaraha Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na wakafa mashahidi wengi katika Masahaba zake miongoni mwao ni Hamza bin Abdul-Mutwalib ami yake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ambae alikuwa akimpenda Mtume mapezi makubwa.



## 626 AD (mwaka wa tano Hijriya)

### Viongozi wa Kikuraishi na makabila tofauti waliuzingira mji wa Madina katika vita vya Khandaki

Vita hivi pia vinajulikana kwa jina la Ahzabu, viongozi wa Kikuraishi na makabila mengine walikubaliana kuwa ipo dharura ya kufanya mashambulizi makubwa ya kumuuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na kuwamaliza Waislamu. Na jambo hilo limepangwa kupitia mpango wa kijeshi wa pamoja uliokusanya wapiganaji elfu kumi kutoka makabila tofauti.



Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akashauriana na Masahaba zake wakaamuwa kuchukua maoni ya Sahaba Salman Al-Farsiy kuchimba handaki katika upande wa kaskazini ya Madina kwa vile mji wa Madina umezungukwa kwa mawe ya volkano yasiyopitika kwa farasi juu yake, kwa hivyo likachimbwa handaki baina ya sehemu ya mashariki (sehemu ya volcano ya mashariki) na sehemu ya magharibi kwa ajili ya kukata njia ya kupita Makureishi na washirika wao.

Waislamu wakachimba handaki kubwa lenye urefu wa kilomita 5.5 na upana wa mita 6.4. Na wakati huo Waislamu walikuwa wapo katika wakati mgumu wakijaribu kuzilinda nafsi zao kwa kiasi cha uwezo walio nao pamoja na kupambana kisaikolojia. Viongozi wa jeshi la Ahzab wakauzunguka mji wa Madina kwa muda wa mwezi mzima na wala hawakuweza kuingia, kisha viongozi wa Makuraishi wakashindwa kusubiri na kupita kimbunga kikubwa kikang`oa mahema yao mengi likalazimika jeshi la Ahzab kuondoka.

## 628 AD (Mwaka wa sita Hijriya)

### Suluhu ya Hudaybiya, Mkataba muda wake ni miaka kumi

Baada ya mwaka mmoja kupita vita vya Khandaki mambo yakatulizana kidogo, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akachukua mapendekezo ya amani akaamua kutekeleza ibada ya Umra katika nyumba ya Allah iliyopo Makka. Na ilikuwa kuitembelea Makka kwa kuikusudia kufanya Ibada ni haki ya Kidini na Kitarekhe kwa Makabila yote ya Waarabu na wakachukua ahadi Makureishi ya kulinda haki hio.

Lilikua ni jambo la kushtukiza kwa viongozi wa Kikuraishi kumuona Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu



yake) amekuja upande wa Makka pamoja na Masahaba wake 1,400 wakiwa hawana silaha walichukua vichinjwa (ngamia, kondoo). Na baada ya majadiliano na viongozi wa Kikuraishi zilikubaliana pande mbili juu ya mkataba kwa muda wa miaka kumi vitasimama vita baina ya Makuraishi na washirika nao kwa upande mmoja na baina ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na watakao ungana nao kwa upande wa pili. Kwa mujibu wa makubaliano hayo Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na Sahaba wake wasiingie katika mji wa Makka kwa mwaka ule bali warejee mji wa Madina watarudi katika mji wa Makka kwa ajili ya kufanya Ibada ya Umra kwa mwaka unaofuata na kwa siku tatu tu..

Na mkataba huu unatoa uhuru kwa makabila na mtu mmoja mmoja kujiunga upande wa Makuraishi au wa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) bila ya upande mmoja kumpiga mwenzake. Lakini atakapoingia yeyote katika washirika wa Kikuraishi kuwa washirika wa Mtume Muhammad ni lazima wamrudishe kwa Makuraishi, lakini Makuraishi wao si lazima kumrudisha yule ambae ataingia katika kundi lao ikiwa anatoka katika kundi la Mtume (rehema na amani ziwe juu yake). Na mkataba umetaja vifungu vyengine na Waislamu wengi waliuona mkataba huo upo kwa manufaa ya Makuraishi na sio kwa maslahi ya Waislamu, lakini Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikua anaangalia mbali zaidi.

### 628-629ad (mwaka wa sita na saba Hijriya)

### Kipindi cha makubaliano Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alifikisha ujumbe ndani ya Bara Arabu na nje yake.

Mkataba huu ulikuwa ni fursa kubwa kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ya kufikisha ujumbe wa Allah Mtukufu ili watu wazungumzie juu ya uhuru pasi na kupingwa na viongozi wa Kikuraishi. Na kupitia kipindi hiki cha suluhu Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alipeleka barua kwa

Wafalme na viongozi akawalingania katika kumuamini Mungu mmoja na kuamini ujumbe aliokuja nao kutoka mbinguni. Na miongoni mwa hao Wafalme ni Najashy mfalme wa Uhabeshi (Ethiopia) na Muqawqis Mfalme wa Alexandria (Misri) na Kisra Parwiz Mfalme wa Fursi na Qaysar Mfalme wa Roma na Harith Al-Ghasaniy kiongozi wa Damascus na vile vile wafalme na viongozi wa Basra na Yamama. Na katika kipindi cha Suluhu wameingia watu wengi katika Uislamu.





## 630 AD (Mwaka wa nane Hijriya)

### Kutekwa mji wa Makka kwa amani bila ya vita

Baada ya chini ya miaka miwili tangu kupitishwa Suluhu ya Hudaibiya, moja ya Makabila washirika wa Makuraishi (Bani Bakr) walivunja makubaliano, wakawavamia washirika wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) (Bani Khuzaa), wakauwawa watu ishirini na kuwafukuza wengine mpaka wakafika Makka. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alipoujuwa uwadui huo alikusanya jeshi la watu Elfu kumi, wakaondoka Madina kuelekea Makka. Na imeelezwa kuwa Abu Sufiyani alikwenda Madina kutetea uwadui wa Bani Bakr juu ya Bani Khuzaa na akataka hifadhi lakini hakuna aliye mkubalia katika mji wa Madina.

Na Makuraishi hawakuwa wamejiandaa kwa ajili ya vita, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akawaamrisha Masahaba wake na jeshi lake kuwa wasimpige isipokuwa atakae wapiga na akaingia katika mji wa Makka kwa amani bila ya vita bali akampa amani kila aliyeingia msikitini na kila aliyeingia nyumbani mwake au nyumba ya Abu Sufyani na yeye ndie kiongozi mkubwa wa Makuraishi na mtukufu wao.



Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akafika katika nyumba ya Allah mtukufu hali ya kuzungukwa na Waislamu wakiwa wananyanyuwa sauti zao kwa Takbir na Tahlili, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamhimidi Allah katikati ya mazingira ya kuteremka rehema kubwa ambapo zilinyenyekea kwake nyoyo za watu.

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alitufu Al-Kaaba na akaondosha Masanamu yaliyokuwemo, na huku akisema: "Haki imekuja na batili imeondoka hakika ya batil ni yenye kuondoka", "Haki imekuja na wala batil haidhihiri wala hairudi".

kisha akawahutubia watu hotuba ya hali ya juu, aliweka mkazo katika kumpwekesha Allah na kumtii yeye na kujiepusha na mambo ya kijahilia na kwamba watu wote wanatokana na Adamu na Adamu anatokana na mchanga na hakika mtukufu wao mbele ya MwenyenziMungu ni mchamungu wao. Kisha alisema aliwaambia watu wa Makka (na wengi wao walimuudhi Mtume na kuwaudhi Waislamu na wakachukuwa mali zao na kuwatowa katika miji yao):

"Enyi Makureshi! Kipi munaona nitakifanya kwenu? (Na katika mapokezi mengine: kitu gani mnasema na kitu gani mnadhania) wakasema: utafanya kheri. Ndugu mtukufu na mtoto wa ndugu mtukufu. Kisha akasema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): Nakuambieni kama alivyosema Yussuf kuwaambia ndugu zake: "Hapana lawama juu yenu. Allah atakusameheni naye ni mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu". Amepokea Bayhaqy katika "Sunanul-Kubra" (9/118) namba (18342). (9/118) namba (18343).

## 630 - 631 AD (Mwaka wa nane na tisa Hijriya)

### Makabila ya Waarabu yajiunga na Uislamu

Baada ya ushindi huu mkubwa walisilimu watu wengi isipokuwa baadhi ya Makabila mfano: kabila la Thaqif na Hawazin, Makabila haya hayakupendezeshwa na jambo hilo (la ushindi) wakampiga vita Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) katika vita vya Hunaini mwaka wa nane Hijriya, Waislamu wakarudi nyuma na kuzidiwa mwanzo wa vita lakini walipata ushindi mwishoni mwa vita hivyo na wakaelekea Twaaif ngome ya kabila la Thaqif na wakawazunguka.

Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamuomba Allah awaongoze watu wa Thaqif na waje kuwa ni Waislamu. Na kwa fadhila za Allah wakaamini kabila la Hawazin na wakaamini kabila la Thaqif. Na Mtume (rehema na amani iwe juu yake) katika mwaka wa tisa Hijriya akawa anapokea wageni na kutuma wajumbe na walinganiaji katika Bara Arabu ili wawafundishe watu ujumbe wa Allah. Wakaingia katika Uislamu makabila mengi ya Kiarabu.

“Hakika Allah amekunusuruni katika sehemu nyingi na siku ya Hunaini ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa lakini haukukufaeni kitu, Na ardhi ikawa dhiki kwenu juu ya upana wake, kisha mkageuka mkarudi nyuma".

"Kisha Allah akauteremsha utulivu wake na juu ya Mtume wake na waumini, na akateremsha majeshi ambayo hamkuyaona,na akawaadhibu wale waliokufuru, na hayo ndio malipo ya Makafiri".

Suratu- Tawba aya ya 25- 26.



## 632 AD (Mwaka wa kumi Hijriya)

### Hotuba ya kuaga

Katika mwaka 632 AD Mtume Muhammad (rehema na aman ziwe juu yake) alitekeleza faradhi ya Hijja katika mji mtukufu wa Makka na akatekeleza pamoja na Waislamu wengine zaidi ya laki moja. Hakika amefikisha Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ujumbe wa Allah kwa watu, akahisi muda wa kurudi kwa Mola wake umewadia.

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alitaka atilie mkazo mambo ya msingi katika Uislamu kama Itikadi na Sharia na awatahadharishe watu wasizifuate hatuwa za Shetani ili wasije wakaingia katika aliyoharamisha Allah. Akawahutubia Waislamu, na walikusanyika katika viwanja vya Arafa, akatowa hotuba iliyokusanya kila kitu cha msingi. Kisha akawahutubia kwa mara ya pili katika masiku ya kuchinja kisha Mtume (rehema na aman ziwe juu yake) akahutubia hotuba ya tatu katikati ya masiku matukufu (Tashriiq), na inaitwa hotuba ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika Hija yake "Hotuba ya kuaga".

Na haikuwa hotuba ya kuaga ni mawaidha tu yaliyoingia katikati ya matendo ya Hija bali ulikuwa ni mkutano wa kiongozi na umma wake, ulikuwa mkutano wa wasia na kuaga. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alifupisha katika hotuba yake misingi mikuu ya dini kwa Waislamu waliokuwepo wakati wa Utume wake na watakaokuja baada yao. Baada ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kutekeleza amana na kufikisha Ujumbe na kuunasihi umma katika mambo ya dini na dunia yao, na ulikuwa mjumuiko wenye unyenyekevu na usikivu. Na wote walitulia kumsikiliza yule ambaye hazungumzi kwa matamanio yake.





Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) aliwataka watu wasikie maneno yake na wayaingize akilini na akawaambia ya kwamba hajuwi pengine mwakani hatokutana nao kama namna hii. Na katika hotuba yake (rehema na amani ziwe juu yake) akatia mkazo katika kumpwekesha Allah mtukufu na kusimamisha dini yake na kujihadhari na shetwani, na akasisitiza kuacha mambo ya kijahilia yenye kuchukiza, na kusimamisha uadilifu kati ya watu. Na akataja uharamu wa kumwaga damu na mali ya watu (kuheshimu uhai wa watu na mali zao) na kuheshimu ahadi na mkataba na kuheshimu haki za wengine. Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akausia kuwafanyia wema wanawake na kuwacha mambo maovu na kujipamba kwa tabia zilizo nzuri.

## 632 AD (Mwaka wa kumi na moja Hijriya)

### Kufariki Mtume (rehema na amani ziwe juu yake)

Katika viwanja vya Arafa iliteremka aya tukufu: "Leo nimekukamilishieni dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimeuridhia Uislamu uwe kwenu ndiyo dini" Suratul- Maida aya ya 3.

Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) hakuishi baada ya hapo zaidi ya miezi mitatu na siku chache. Hakika limemalizika jukumu kubwa baada ya miaka ishirini na tatu kuongoza na kujitolea na kuwa na Imani kubwa kwa Allah.

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alifariki nyumbani kwake katika mji wa Madina ulionawirika na hakuacha mali wala utajiri isipokuwa ameacha kitabu cha Allah na Sunna zake.

Na kitabu cha Allah (Qur-ani Tukufu) bado kinasomwa usiku na mchana na kinatia nuru nyoyo za mamilioni ya watu katika kila sehemu ya ardhi mpaka zama zetu hizi.

Amefariki Mtume Muhammad bin Abdillah (rehema na amani ziwe juu yake) siku ya Jumatatu mwezi wa Rabiil Awwal mwaka wa kumi na moja Hijriya sawa na mwaka 636 AD, kwa mujibu wa mapokezi yenye nguvu zaidi.





Mandhari ya angani ya mji Mtukufu wa Makka, Picha imepigwa na Suzan Eskander





**Msikiti Wa Makka**

Na inadhihiri katikati yake Al-Kaaba tukufu ambayo Allah Mtukufu amemuamrisha Nabii Ibrahimu (amani ziwe juu yake) aunyanyuwe msingi wake. Nayo hio Al-kaaba kibla cha Waislamu katika Sala zao popote pale wanapokuwa katika sehemu yoyote katika dunia. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) aliashiria kwa kusema kwamba Sala moja katika Msikiti Mtukufu wa Makka ni bora kuliko Sala laki moja katika misikiti mengine.





Picha ya angani inayodhihiri Jabal Nuur ndani yake lipo pango la Hiraa linaloelekeana na mnara wenye saa karibu na Msikiti wa Makka Mpiga picha ni Suzan Eskandar.





Mandhari ya angani ya Msikiti Mtukufu wa Makka, mji Mtukufu wa Makka



Mandhari ya Panorama ya Jabal Nuur katika mji Mtukufu wa Makka sehemu liliopo pango la Hiraa.



64

Pango la “Thawri” ambamo alikaa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na Sahaba wake Abubakar masiku matatu katika safari yao ya kuhama kutoka Makka kuelekea Yathrib (Madinatul Munawwara).




المدينة
قباء
ذو الحليفة
ملل
الروحاء
الرويثة
المنصرف
ذو مسلم
الجداجد
بطن ذي كثير
مرجح مجاج
مولجة حجاج
مولجة لقف
ثنية المرة
بدر
رابغ الرمل
الجحفة
كلية
خيمة
أم معبد
المشلل
قديد
خليص
أملج
كديد
غدير الأشطاط
ثنية الغزال
عسفان
بطن مر
سرف
الحديبية
Jeddah
مكة
غار ثور
خط الهجرة
خط سير القوافل



Msikiti wa Quba, ni Msikiti wa mwanzo kujengwa katika Uislamu, uko umbali wa kilomita tano kutoka Msikiti wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika mji wa Madinul Munawwara. Kwa mujibu wa mapokezi ilikuwa siku ya jumatatu tarehe 8 Rabiil Awwal mwaka wa 14 tangu kupewa Utume na mwaka wa kwanza wa Hijra amefika Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na Sahaba wake Abubakar Asswiddiq (radhi za Allah ziwe juu yake) sehemu ya Quba, alikaa hapo siku chache, kisha akaingia katika mji wa Madina.



Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anaenda katika Msikiti Quba kila siku ya Jumamosi kwa kutembea kwa miguu au kwa kipando na akisali ndani ya msikiti huo rakaa mbili, Na akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Kuswali katika Msikiti Quba malipo yake ni kama kufanya ibada ya Umra" Amepokea Tirmidhy






Mandhari ya kubuni inayoonesha Msikiti wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika mji wa Madina uliozungukwa na nyumba na mitende. (Kituo cha Utafiti na Mafunzo cha Madina).



Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliutanua msikiti wa Madina mwaka wa saba Hijriya baada ya vita vya khaybar, kisha ukatanuliwa tena katika zama za Khalifa Omar bin Khatwab (radhi za Allah ziwe juu yake) mwaka wa kumi na saba Hijriya, na baada ya hapo ulitanuliwa Msikiti kwa mara nyingi zama kwa zama, na aliyeutanuwa zaidi alikuwa ni mtumishi wa Misikiti miwili Mitakatifu (Makka na Madina) Mfalme Fahdi bin Abdul-Aziz (Allah amrehemu) ilikuwa kwa ukubwa wa mita za mraba 82,000 na eneo lake kiujumla lilizidi ukubwa wa mita za mraba 400,000 .







Msikiti Mtukufu wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) baada ya kutanuliwa. Picha na Nawshad Ali

Hakika sehemu ambayo lilipo kaburi la Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ni sehemu pekee inayojulikana kwa uhakika kati ya sehemu za makaburi ya Mitume iliyotangulia.

Amezikwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika nyumba yake ambayo ipo jirani na Msikiti wake (nyumbani kwa Bibi Aisha), wakati alipoutanuwa Msikiti Bwana Walidi bin Abdul-Malik mwishoni mwa karne ya kwanza Hijriya kiliingizwa chumba cha Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) - ambacho yeye amezikwa - humo kuwa ni sehemu ya Msikiti Mtukufu wa Mtume.







Hili ndilo Kaburi la Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) (la mwanzo kutoka upande wa kushoto), na pembezoni mwake yapo makaburi ya Makhalifa wake wawili; Khalifa Abu Bakar Asswiddiqi na Khalifa Omar bin Khatwab (radhi za Allah ziwe juu yao).

## Maangalizo

1. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amezaliwa mwaka 571 AD kwa mujibu wa baadhi ya mapokezi na makadirio.
2. Msikiti wa Aqabah au Msikiti wa Bay'ah, upo baina ya mji wa Makka na eneo la Mina. Aliujenga Khalifa wa dola ya Abbassiya Abu Jaafar Al-Mansour sehemu ile ile ambayo Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alipewa Bay'ah na kikundi cha watu 70 kutoka kabila la Awsi na Khazraj miongoni mwa watu wa Madina na wakaingia katika Uislamu.
3. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) baada ya kuhama Madina walibaki Makka Waislamu wachache ambao hawakuweza kuhama.
4. Tarehe ya Hijriya inaanza tokea Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alipohamia Madina tarehe 13/Sept/622AD takriban. Pia Ilikuwa kurudi kwa Waislamu katika mji wa Makka kwa amani bila ya vita tarehe 8/1/630 AD takriban.

---



Mchoro huu ni katika kazi za Bwana Ally Al-Baddah mwalimu wa khati za Kiarabu katika chuo kikuu cha Kuweit.
"Unapoomba muombe Allah" hii ni sehemu ya hadithi na wasiya wa Mtume wa Allah {rehema na amani ziwe juu yake} unafahamisha umuhimu wa kurejea kwa Allah pekee katika furaha na matatizo.

Alipokwenda Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) katika mji wa Twaif ili kuwalingania watu wa mji huo Uislamu, watu wake walimfanyia muamala mbaya na wakamuudhi na wakamtowa katika mji wao, akahuzunika Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) huzuni kubwa akamuomba Mola wake dua yenye kuathiri nafsi imetajwa katika baadhi ya vitabu vya Sira.

## DUA

Ewe Mola kwako nashtakia udhaifu wa nguvu zangu
na uchache wa ujanja wangu, na unyonge wangu kwa
watu.
Ewe mwingi wa kurehemu, wewe pekee ndie Mola wa
wanyonge
na wewe ndie Mola wangu.. Kwa nani umeniwacha?
Kwa mtu wa mbali anae nishambulia
au kwa adui uliyemmilikisha jambo langu?
Kama hujanikasirikia basi sijali...
isipokuwa msamaha wako ndio jambo kubwa
ninalolitaka... Najilinda kwa nuru ya dhati yako ambayo
iliyonawirisha kiza
na likatengenea jambo la dunia na Akhera isije
ikanipata ghadhabu yako au kunishukia hasira zako..
Naomba radhi zako mpaka uniridhie
hakuna ujanja wala nguvu isipokuwa kutoka kwako.
(Amepokea Twabrany na wengineo, na
wameidhoofisha baadhi ya Wanavyuoni).

SURA

# 4

# UTUME NA UJUMBE



Muundo wa kisanaa unaoakisi khati ya Kiislamu ya “Thuluth” kwa aya Tukufu “Na hatukukupeleka wewe isipokua kwa watu wote mwenye kubashiria na kuhofisha”. Ni katika kazi ya mchoraji wa Japan Nubuku Sajawa

Jabali Nuur liliopo mji Mtukufu wa Makka

# UTUME NA UJUMBE

## Hakujuwa Mtume Muhammadi (rehema na amani ziwe juu yake) kuwa atakuwa Mtume

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliishi maisha ya kawaida kama watu wengine katika jamii na alichunga kondoo na alifanya biashara akijulikana kwa Uaminifu na Ukweli. Na hakuwahi kuabudu Masanamu, pamoja na kuwa alikuwa anaishi katika jamii yenye Miungu mingi. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anaamini uwepo wa Mungu mmoja wa Ulimwengu asiye na mshirika, alikuwa anakwenda kwenye pango dogo ili atumie wakati katika kutafakari na kufanya ibada.

Linapatikana pango hili (ambalo hujulikana kwa jina la "Pango la Hiraa") katika mlima uitwao Jabal Nuur lenye muinuko wa mita 634 juu ya usawa wa bahari na Jabal Nuur liko mbali na msikiti wa Makka kiasi cha kilomita 4, ndani ya mji Mtukufu wa Makka.

SOMA

## Haikuwa katika fikra wala ndoto

Wakati alipofikia Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) miaka arubaini katika umri wake alikuwa akipenda upweke na kujitenga na mambo ya kidunia, na katika mwezi wa Ramadhani mwaka 610 AD, wakati Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anatafakari na anamuomba Mola wake katika pango la Hiraa alimfikia kwa mara ya kwanza Malaika Jibrili (amani ziwe juu yake) akamwambia Mtume "Soma" Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akahisi khofu kubwa kwa kuwa alikuwa hajuwi kuandika wala hajui kusoma, alimjibu kwa kusema: "Mimi sijuwi kusoma", akarejea akamtaka mara tatu asome na Mtume (rehema na ziwe juu yake) anamjibu majibu yaleyale. Kisha Jibril (amani ziwe juu yake) akasoma aya kutoka kwa Allah muumba wa ulimwengu ili ziwe mwanzo wa kuteremka Wahyi kutoka mbinguni na mwanzo wa ujumbe wa mbinguni kwa kila mwanaadamu.

Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba ۞ Amemuumba mwanaadamu kutokana na pande la damu ۞ Soma na Mola wako ni Mkarimu ۞ Ambae amemfundisha mwanaadamu kwa kalamu ۞ Ambaye amemfundisha mwanaadamu asiyoyajuwa ۞ Suratul-A'laq aya ya 1-5.

Akatoweka Jibril (amani iwe juu yake) baada ya hapo wala hakumwambia Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kuwa atakuwa Mtume wala Nabii.

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anarejea nyumbani kwake akiwa na hofu

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alirudi nyumbani kwake haraka akiwa anatetemeka, akamsimulia mke wake Bibi Khadija (radhi za Allah ziwe juu yake) yaliyomtokea. Bibi Khadija akamfunika shuka akamtuliza na kumtowa hofu akamwambia hakika Allah hatomuaibisha, akamtajia sifa zake kuwa anaunga ukoo anawasaidia mafakiri anampa mwenye haki haki yake.



Neno "Muhammad" kwa mchoro wa kisanaa Unaelezea kupanda kwa Mtume

(rehema na amani ziwe juu yake) kwenye Jabali Hiraa. Na inaashiria pia kupanda na kukwea kufikia kilele.

Ni miongoni mwa kazi za mchoraji wa Jodan Abdul-Majid Annuayrati



## Ni Wahyi kutoka kwa Allah au kupatwa na shetani?

Bibi Khadija (radhi za Allah ziwe juu yake) aliendа pamoja na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kwa Bwana Waraqa bin Naufali mtoto wa Ami yake Bibi Khadija, alikuwa ni mzee mwenye akili na busara, alikuwa mnaswara tokea ujahilia, alikuwa na elimu ya Tawrati na Injili. Aliposikia Bwana Waraqa yaliyotokea kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alimueleza kuwa aliyemjilia ni Jibril (mjumbe wa mbinguni) ambae alimteremsha Allah kwa Mussa (amani ziwe juu yake), na hakika yey atakuwa Mtume atakayewajuuilisha watu Muumba wao na Mtume anaefikisha Ujumbe wa Mola wao, atawatowa kwenye kiza na atakaye wajuulisha kwenye Mwangaza. Akatamani Bwana Waraqa bora angekuwa kijana ili amnusuru Mtume (rehema na amani ziwe juu yake). Akatabiri kuwa watu wa Makka watamtowa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika mji wake kwani hakuna yeyote katika Mitume aliyepewa Utume kama huu isipokuwa walimfanyia uadui watu wake na walimtoa.



## Muhammad ni Mjumbe wa Allah

Baada ya muda aliteremka Malaika Jibril (amani ziwe juu yake) kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kwa mara ya pili na akamsomea aya hizi katika maneno ya Allah akimuamrisha Mtume afikishe Ujumbe wa mola wake:

> Ewe uliyejigubika ۞ Simama uonye ۞ Na Mola wako mtukuze ۞ Na nguo zako zisafishe ۞ Na machafu yahame ۞ Wala usitoe kwa kutaraji kuzidishiwa ۞ Na kwa ajili ya Mola wako subiri ۞ Suratul-Muddathir aya 1-7

Na akaendelea kuteremka Jibrili (amani ziwe juu yake) na kukutana na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwa muda wa miaka ishirini na tatu, uliteremka katika muda huo Wahyi wa maneno ya Allah Mtukufu Qur-ani Tukufu kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ili aifikishe kwa watu wote.

## Ipi ilikuwa Daawa ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake)?

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliwalingania jamaa zake na watu wake na watu wote ili wajuwe uhakika uliopo ya kwamba ulimwengu una Muumba mmoja ambaye alieumba mbingu na ardhi na watu wote. Basi hairuhusiki kwa yeyote kumuabudu asiye kuwa Allah au kuabudu yoyote pamoja na Allah au akamshirikisha Allah na yoyote katika kufuata hukumu zake na amri zake na makatazo yake.

## Ni upi Ujumbe wa mbinguni aliokuja nao Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake)?

Ujumbe huu ni Uislamu, yaani kujisalimisha kwa Allah kwa kumuamini na kukubali Sharia yake ambayo ni Aqida na Sharia. Na Aqida ni kuamini uwepo wa Allah na kuamini kuwa yeye ni mmoja hana mshirika, yeye pekee ndie mlezi wa watu na mmiliki wa watu na ndie Mola wa watu. Na Sharia ni sharia ya Allah na hukumu zake ambazo zinapanga maisha ya mwanadamu na matendo yake na harakati zake na mambo yote ya kimaisha. Na inagawika Sharia katika vigao vikuu vitatu navyo ni:

1. **Ibada**: Nayo ni hukumu ambazo wanajua watu namna ya kumuabudu Allah kwa mujibu wa sheria ya Allah na inakusanya shahada ya kuwa hapana mwenye kustahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ni Mtume wa Allah na kusimamisha Sala na kutowa Zaka, na kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani, na kuhiji nyumba Tukufu katika mji Mtukufu wa Makka kwa mwenye uwezo.

2. **Miamala**: Na inakusanya hukumu na vidhibiti vya mambo yote ya kila siku kama Mfano: Ndowa, Talaka, Mirathi, na Mahakama, Biashara na Ukulima na Haki za watu.

3. **Tabia**: Na inakusanya maadili na tabia njema ambazo Allah anawataka watu washikamane nazo na waamiliane kwazo baina yao, kama tabia nzuri, ukweli, uaminifu, Ikhlasi, kusaidiana, kupendana, uadilifu, udugu, kuwapendelea watu katika kheri na kutowa, na ukarimu.

## Wasiya wa Ujumbe wa mbinguni

## Ufupisho wa yale aliyoharamisha Allah kwa waja wake

Kwa jina la Allah mwingi wa rehema mwenye kurehemu.

Sema njooni nikusomeeni yale aliyoyaharamisha Mola wenu juu yenu, msimshirikishe na chochote, wafanyieni wema wazazi wenu, musiwauwe watoto wenu kuogopea ufukara tunakupeni riziki na watoto wenu, msikaribie machafu yanayo onekana na ambayo yamejificha, msiuwe nafsi ambayo Allah ameiharamisha isipokuwa kwa haki, nayo amekuusieni kwayo ili mupate kufahamu ۝ Wala msikaribie mali za mayatima isipokuwa kwa njia nzuri, mpaka wafikie baleghe, timizeni vipimo na mizani kwa uwadilifu, hatulazimishi nafsi yoyote isipokuwa anachokiweza, mnaposema fanyeni uadilifu hata kama ni mtu wa karibu, tekelezeni ahadi ya Allah, hayo ndio aliyo kuusieni Allah ili mpate kukumbuka.۝

Suratul-An'aam

Katika aya mbili, za 151 na 152 katika Suratul- An'aam ni ufupisho wa yale aliyoharamisha Allah mtukufu na Nyasia alizoziorodhesha Allah mtukufu ili watu wafanyie kazi na wayawache yale waliyokuwa nayo tangu enzi za Ujahilia. Na hiyo ndio misingi ya .mfumo wa Maadili na ya kivitendo iliyokamilika

---

Ni muhimu kuashiria ya kwamba Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alipitisha miaka 13 akiwa ndani ya mji wa Makka baada ya kupewa Utume. Aliipa kipaumbele katika miaka hiyo kuimarisha Akida na Imani ya kumpwekesha wemyeziMungu mmoja ambaye hana mshirika. Na baada ya kuhama kuelekea mji Mtukufu wa Madina alitumia Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) miaka 10 takriban na alitoa kipaumbele katika kuwafundisha watu misingi ya Sharia na kanuni zake.

## Maelezo ya kivitendo ya Ujumbe wa Kiislamu...lakini katika mji wa Uhabeshi

Huenda maelezo mazuri ya kuwaelezea Ujumbe wa Kiislamu ni ule ambao ulikuja kupitia ulimi wa Sahaba Jaafari bin Abii Twalib (radhi za Allah ziwe juu yake) wakati alipokuwa katika kundi la Waislamu waliokimbia kwa sababu ya dini yao kutokana na dhuluma ya Makuraishi katika mji wa Makka wakaelekea katika mji wa Uhabeshi -Ethiopia ya hivi sasa- wakatafuta hifadhi kutoka kwa mfalme Najashi wa wakati huo. Lilitokea hilo mwaka wa tano wa kuanza Uislamu. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliona yaliyowapata Waislamu kutokana na dhulma, kutezwa nguvu na vikwazo vya kiuchumi kutoka mikono ya washirikina wa Kikuraishi, akawanasihi baadhi yao wahame kuelekea Uhabeshi ambayo Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alielezea kuwa katika nchi hiyo kuna mfalme muadilifu hadhulumiwi mbele yake yoyote.

**Nini alichokisema Jaafar bin Abii-Twalib (radhi za Allah ziwe juu yake) kumwambia Najjashi?**

“Ewe mfalme tulikuwa ni watu wajinga, tunaabudu masanamu, tunakula maiti tunafanya machafu, tunakata ukoo, tunaufanyia ubaya ujirani, mwenye nguvu katika sisi anamuonea mnyonge.

Tulikuwa katika hali hiyo mpaka Allah alipotuletea Mtume anaetokana na sisi tunaijuwa nasabu yake na ukweli wake na uaminifu wake na kujihifadhi kwake na machafu, akatulingania kwa Allah ili tumpwekeshe na tumuabudu Allah na tuwache tuliyokuwa tunayaabudu sisi na baba zetu katika mawe na masanamu kinyume na Allah.

Akatuamrisha kusema ukweli na kutekeleza amana, na kuunga ukoo, na ujirani mzuri na kuacha haramu na kumwaga damu, akatukataza mambo machafu, na kusema uongo, na kula mali ya mayatima, na kumsingizia uchafu mwanamke aliehifadhika, na akatuamrisha kumuabudu Allah peke yake tusimshirikishe na chochote, na akatuamrisha kusali na kutowa Zaka na kufunga.

Tukamsadiki na kumuamini, wakatufanyia uadui watu wetu wakatufitini katika dini yetu na wakatuadhibu ili waturejeshe kwenye kuabudu masanamu wakati walipo tudhulumu wakatubana, wakatuzuwia na dini yetu, tukatoka kuja kwenye mji wako, na tumekuchaguwa wewe tumeacha wengine tukapendelea kutaka hifadhi yako, na matarajio yetu hatuto dhulumiwa mbele yako.

## Mfalme Najjashi anaukubali Uislamu

Najjashi alikuwa muadilifu, anamuogopa Allah katika kutowa hukumu. Akamtaka Sahaba Jaafar amsomee chochote katika Wahyi ambao ameteremshiwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake), Sahaba Jaafari (radhi za Allah ziwe juu yake) akamsomea sehemu ya Suratu-Mariam. Najjashi akasikiliza aya hizo na akaathirka nazo mpaka akalia na zikarowana ndevu zake, kisha akasema:





"Hakika haya na yale aliyokuja nayo Issa yametoka sehemu moja".

Pamoja na majaribio ya Amru bin Aas ambae aliwafata Waislamu huko Uhabeshi (kabla ya kusilimu) ili kumkinaisha Najjashi awarejeshe Makka lakini Najjashi alikubali kuwapa Waislamu hifadhi ya kukaa katika mji wa Uhabeshi.






# UISLAMU...NI UJUMBE WA MWISHO WA MBINGUNI



## Nini Uislamu?

Uislamu...Ni Ujumbe wa mwisho wa mbinguni

Neno "Uislamu" lina maana ya kujisalimisha kwa Allah mmoja aliye pekee. Allah ambae ameumba ulimwengu peke yake na yeye ni Muumba wa kila kitu, wala hana mshirika katika ufalme wake, na hakuna Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye. Na dini ya Uislamu ni dini ya kumpwekesha na kumtakasia Allah Mfalme wa Wafalme na muumba wa viumbe.

## Majina mazuri ya Allah



Allah ana majina na sifa nyingi, kati ya hayo yamekuja katika Qur-ani tukufu na katika hayo yamekuja katika hadithi za Mtume (rehema na amani ziwe juu yake). Na majina yaliyo julikana (maarufu) idadi yake ni 99.

"Na anayo Allah majina mazuri basi muombeni kwayo". (Suratul A'araf aya ya 180)

"Sema: Muombeni Allah au muombeni mwingi wa rehema kwa jina lolote mtakalotumia, basi yeye anayo majina mazuri".(Suratul-Israai aya ya 110)

"Yeye ndiye Allah ambaye hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye tu, anayeyajuwa yaliyo fichikana na yaliyo dhahiri, mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo ۝ Yeye ndiye Allah ambaye hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye tu, mfalme, mtakatifu mwenye salama, mtoaji wa amani, mwenye kuyaendesha mwenyewe mambo yake, mwenye shani, anayefanya analolitaka, mkubwa, Allah yupo mbali na wanaomshirikisha nae ۝".

Suratul-Hashr aya 22-23

“Yeye ndiye Allah muombaji mtengenezaji, mfanyaji wa sura (za namna namna za viumbe), mwemye majina mazuri, kinamtukuza kila kilichomo mbinguni na ardhini, naye ni mwenye nguvu, mwenye hekima”.
Suratul-Hashr aya ya 24



### Mtume Muhammad na Uislamu

Uislamu Imani na Kuwa Imara

Imepokewa kutoka kwa Abi Amri Sufyan bin Abdalla Thaqafy (radhi za Allah ziwe juu yake) alisema: Nilisema :“Ewe Mjumbe wa Allah niambie katika Uislamu neno sitomuuliza neno hilo yeyote asiyekuwa wewe. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema:

“Sema nimemuamini Allah kisha kuwa Imara msimamo”. Amepokea Muslim (38).

Maneno matano pekee yametoka kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) yameweka mfumo wa maisha ulio kamilika, anaufuata mfumo huo Muumini Muislamu, na unamuongoza njia anayopita kuelekea kwa Mola wake, na unamuweka mbali na uchupaji mipaka katika kauli na vitendo. Kwahiyo Uislamu unataka msimamo imara katika kila jambo na kumuamini Allah, ndio njia ambayo huimarisha mwenendo wa mtu na matakwa yake na matarajio yake. Basi mtu huzaliwa upya kunakomuandaa kukubali hukumu za Allah na Sharia zake, basi akaishi hali ya kuwa na amani na mwenye kitulizano, na kufurahia kupata raha na mafanikio. Na ametaja Allah mtukufu sifa za Waumini aliposema: “Hakika wale waliosema Mola wetu ni Allah kisha wakenda mwendo mzuri hao huwateremkia Malaika (wakati wa kutoka roho) wakawaambia: msiogope wala msihuzunike na furahini kwa Pepo mliyoahidiwa”. Suratul- Fuswilat aya ya 30.

## Uislamu na Amani

ASSALAM: Ni jina katika majina mazuri ya Allah ambayo yametajwa katika Qur-ani tukufu. Basi ambae anajisalimisha kwa Allah mmoja asiyekuwa na mshirika ni lazima ahisi utulivu na amani katika nafsi yake na ataishi kwa amani na waliomzunguka, basi haudhi watu wala wanyama au mimea au kitu chochote kilicho kwenye mazingira. Na miongoni mwa vitu vizuri katika Uislamu ni maamkizi baina ya Waislamu ambayo huwa kwa maneno haya:

"Amani iwe juu yenu na rehema za Allah na baraka zake" ambayo mara nyingi hufupishwa kwa kusema "Assalamu Alaykum" (Amani iwe juu yenu)

"Yeye ndiye Allah ambaye hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye tu, mfalme, mtakatifu mwenye salama, mtoaji wa amani, mwenye kuyaendesha mwenyewe mambo yake, mwenye shani, anayefanya analolitaka, mkubwa, Allah yupo mbali na wanaomshirikisha nae". Suratul-Hashr aya 23

## Ni Waislamu au wafuasi wa Muhammad (Muhammadiyyun)?

Hakika Waislamu waliomkubali Mtume Muhammad (rehema na amani ziwa juu yake) hawaitwi "Muhammadiyyun" yaani wafuasi wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kinyume na wafuasi wa dini nyengine. Na yeyote atakayeukubali Uislamu kama dini yake na dira ya maisha yake anaitwa "Muislamu" yaani amemuamini Allah na amejisalimisha kwake.

### Zipi nguzo za Imani na zipi daraja za dini katika Uislamu?

Nguzo za Imani ni sita, nazo: Kumuamini Allah, na kuamini Malaika wake, na kuamini vitabu vyake, na kuamini Mitume yake, na kuamini siku ya mwisho, na kuamini Kadari kheri na shari.

### Ama daraja za dini katika Uislamu ni:




**Ihsani:** Ni kumuabudu Allah kama kwamba unamuona na kama wewe humuoni basi yeye anakuona.

Haya ni kutoka mapokezi ya Khalifa Omar bin Khattab, suala alilouliza Jibrili (amani iwe juu yake) kumuuliza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kuhusu Uislamu na Imani na Ihsani.

### Nguzo za Kiislamu

Uislamu umejengeka juu ya mambo matano ya msingi, haifai kukanusha lolote katika hayo, wala mtu hawi Muislamu mpaka aziamini nguzo za Uislamu tano.

| | | |
|---|---|---|
| **1** | **Shahada** | Kutamka shahada na kuamini kwa yakini na kufanyia kazi makusudio yake.<br>Nayo ni: Nashuhudia kuwa hapana anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na nashuhudia kuwa Mtume Muhammad ni Mjumbe wa Allah |
| **2** | **Sala** | Kutekeleza Sala tano za faradhi kwa wakati wake |
| **3** | **Funga** | Kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani kila mwaka |
| **4** | **Zaka** | Kutoa Zaka ya mali. |
| **5** | **Hijja** | Kukusudia nyumba tukufu ya Allah kwa mwenye uwezo. |



## 1. Shahada

Shahada ni msingi wa dini na nguzo yake, na ndio kithibitisho cha upweke wa Allah mwenye kutukuka hana mshirika na hakuna mwenye haki ya kuabudiwa asiyekuwa yeye.

Na mtu husifika kuwa ni Muislamu wakati anapotamka Shahada na akaitakidi kwa yakini bila ya kuwa na shaka, basi ikathibiti katika moyo wake na akafanyia kazi kwa mujibu wa yakini akatekeleza nguzo za Uislamu Sala na Funga na Zaka na Hija na vikanyenyekea viungo vyake, akashikamana na halali na akajiepusha na haramu.



Na maneno ya Shahada ni kusema: “Ninashuhudia kwamba hapana anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na nashuhudia kuwa Mtume Muhammad ni Mjumbe wa Allah. Na kushuhudia kuwa Mtume Muhammad ni Mjumbe wa Allah ni kukubali Utume wake na Ujumbe wake ambao alikuja nao kutoka kwa Allah mtukufu Ujumbe ambao unaamrisha pia kuamini Mitume yote iliyomtangulia.

## 2. Sala tano

Sala ina nafasi kubwa katika Uislamu, ndio kitu cha mwanzo kuhesabiwa siku ya Kiama, nayo ni alama yenye kumtenganisha Kafiri na Muislamu ambae katamka Shahada kwa ukweli kabisa. Na Allah amefaradhisha kwa Waislamu Sala tano kila siku, na ndani yake kuna nidhamu ya kipekee ya kuupanga wakati wa mwanadamu. Ni wajibu kwa kila Muislamu atekeleze Sala katika wakati wake uliopangwa na kwa namna alivyowafundisha Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) Waislamu.

Sala ni Utekelezaji wa kivitendo wa




> "Na waja wangu watakapokuuliza hakika yangu. (waambie kuwa) Mimi nipo karibu yao, Naitikia maombi ya muombaji anaponiomba, Basi na waniitikie na waniamini ili wapate kuongoka".
>
> Suratul-Baqarah aya ya 186

Neno Sala katika lugha ya kiarabu limetokana na neno "Waswala" yaani ameunga, kwahiyo Sala ni mahusiano na kiunganishi kati ya mja na Mola wake, na anawasiliana mtu na Muumba wake basi anamshukuru na kumsifu na kumtajia matatizo yake na anamuomba msaada wake na uongofu wake na maelekezo yake kama anavyomuomba hifadhi na ulinzi wake.

Na Sala katika Uislamu ni kukutana kati ya Mwanadamu na Muumba wake mara tano kwa siku, humpa nguvu ya kiroho na utulivu wa nafsi yake inayomletea uimara na furaha kwa muda wa uhai wake. Na hazichukui Sala tano kila siku zaidi ya nusu saa au dakika arubaini kwa kuzigawanya siku nzima.

**Nguvu ya kiroho na msaada wa kinafsi**

Hakika mwanadamu kiwiliwili na roho, kiwiliwili kinahitaji nguvu za kimwili kwa kula chakula mara tatu au mara nne kila siku na kwa kupumzika na kulala, na haya yanatumia muda mrefu kuliko wakati wa Sala ambayo humpatia mwanadamu nguvu za kiroho na utulivu wa nafsi.

## 3. Zaka ya Mali



Allah mtukufu amefaradhisha kwa Waislamu Zaka ya mali, nayo ni kiasi cha asilimia mili na nusu 2.5% katika mali ambayo imefikia kiwango na kuzidi mahitaji yake ya msingi na ikapitiwa mali hiyo na mwaka mzima. Na hutolewa Zaka na kupewa mafakiri na masikini ambao wanamiliki baadhi ya mali lakini haitoshelezi mahitaji yao, na wenye kufanya kazi ya kukusanya Zaka na kuigawa, na waliosilimu wepya ili kuzipooza nyoyo zao, na wenye madeni ambao wameshindwa kulipa madeni yao, na msafiri alie haribikiwa mwenye kuhitaji mali ili apate kufika kwao, na kuwakomboa watumwa, na kwa ajili ya njia ya Allah. Kutowa Zaka ni ibada ya mali ameifaradhisha Allah mtukufu kwa waja wake ili hiyo Zaka iwasafishe nafsi zao kutokana na ubakhili na kuzitakasa nafsi za wenye kuhitaji kutokana na husda na kutia nguvu mapenzi na kupatikana heshima baina ya tajiri na maskini, na inazidisha umoja wa kusaidiana na kudhaminiana katika jamii na kupatikana uadilifu wa kijamii kwa kuhamisha mali kutoka kwa wenye kujitosheleza na kuwapelekea wenye kuhitajia.

Kwa maelezo zaidi ya aina ya Zaka na namna ya kuzigawa kwake tafadhali rejea katika vitabu vya Fiqhi.

Tunataja hapa aina hizo kwa njia ya mifano wala sio kwa ukamilifu wake.

(Zaka za Maadini kama dhahabu na fedha, Wanyama kama ngamia, kondoo, mbuzi na ngombe, na tende, nafaka na mali ya biashara).

2.5%
Zaka
ya Mali

## 4. Funga ya mwezi wa Ramadhani



Allah mtukufu amefaradhisha kwa Waislamu kufunga kama alivyo faradhisha kwa waliopita kabla yao.

Na inakuwa funga katika mwezi wa Ramadhani nao ni mwezi ambao Allah mtukufu ameiteremsha ndani yake Qur-ni tukufu. Muislamu anajizuwia kula, kunywa na kustarehe kindoa kuanzia kuchomoza Alfajiri mpaka kuzama jua.

Na ndani ya Funga Muislamu anaishi maisha yake ya kawaida yaliyo ambatana na mazingatio ya kihisia na usafishaji wa kinafsi na kuihisabu nafsi na kufanya matendo mema.

Na Funga inayo faida kubwa za kiafya, imethibitisha tiba ya kileo, na ndani yake anajifundisha mfungaji njia ya kutawala matakwa na matamanio yake na kupanda daraja yake kiroho.

Na mfungaji anahisi udhaifu na kumhitajia kwake Allah mtukufu na msaada wake na riziki zake na kuwaonea huruma mafakiri pamoja na wale waliopatwa na njaa na wenye uwezo mdogo wa kimali na chakula katika miji yao.

| **MIEZI YA MIANDAMO** | |
|---|---|
| 1 | Muharram |
| 2 | Safar |
| 3 | Rabiil-Awwal |
| 4 | Rabiil- Aakhirah |
| 5 | Jumadal-Uula |
| 6 | Jumadal-Aakhirah |
| 7 | Rajab |
| 8 | Shaaban |
| 9 | **Ramadhan** |
| 10 | **Shawwal** |
| 11 | **Dhul-Qaadah** |
| 12 | **Dhul-Hijjah** |

## 5.Hija

Hija ni nguzo ya tano katika nguzo za Kiislamu, nayo ni lazima kwa kila Muislamu aliye baleghe mwenye akili sio mtumwa mwenye uwezo. Ni wajibu kuhiji katika umri mara moja kwa yule ambae anao uwezo wa kumiliki mali na uwezo wa kimwili kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Hija na hio ndio safari tukufu anayoifanya Muislamu katika uhai wake hataki ndani yake isipokuwa radhi za Mola wake mtukufu na Muumba wake ambae kwake yeye ndio marejeo yake.

Hija ni ibada tukufu inayofanywa kwa pamoja, mamilioni ya watu wanasafiri kwa ajili ya ibada hiyo kutoka sehemu mbali mbali za dunia kwenda mji Mtukufu wa Makka na wanakusanyika wote katika mwezi tisa Dhul-hija katika viwanja vya Arafa na wanashirikiana katika kumuomba Allah na kumsifu kwa lugha tafauti na makabila tafauti.

Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): "Mwenye kuhiji kwa ajili ya Allah mtukufu akawa hakufanya uchafu na hakufanya uovu atarudi kama siku aliyozaliwa na mama yake". Amepokea Bukhari (1521) na Muslim (1350)



## Mungu mmoja na Ujumbe mmoja

**Manabii wa Allah na Mitume yake:** Ametilia mkazo Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kuwa Allah mtukufu yeye ni Mola mlezi wa viumbe vyote, basi hakuwaacha pasi na muongozo au kuwaelekeza bali aliwapelekea Manabii na Mitume kwa zama tofauti na kubeba Ujumbe mmoja unaotia mkazo juu ya uwepo wa Allah mtukufu na upweke wake. Na malengo ya Ujumbe wa Allah mtukufu ni kuwajuulisha watu Mola wao, na hekma ya kuumbwa kwao na kuwahifadhi na upotevu na kupotea na kuwaongoza wao kwenye tabia tukufu.



Na Qur-an tukufu imewataja Manabii na Mitume ishirini na tano na ikataja visa vya baadhi yao, imetaja kisa cha Nabii Adam baba wa Manabii (amani iwe juu yao) mara 25, kisa cha Nabii Nuh (amani iwe juu yake) mara 43, kisa cha Nabii Ibrahim (amani iwe juu yake) mara 69, kisa cha Nabii Mussa (amani iwe juu yake) mara 136 na kisa cha Nabii Issa (amani iwe juu yake) mara 25.

Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): "Hakika mfano wangu na mfano wa Mitume kabla yangu ni kama mfano wa mtu amejenga nyumba akaifanya nzuri na akaipamba isipokuwa sehemu ya tofali tu pembezoni mwa jengo, wakawa watu wanalitembelea na kushangaa na wanasema: Kwanini lisiwekwe hili tofali? akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): Mimi ndio tofali na mimi ndio mwisho wa Mitume". Amepokea Bukhari (3535)

Angalizo: neno "Labina" (kwenye hadithi, ni jiwe la kujengea, na kusudio hapa ni kuwa kwenye jengo kulikuwa na uwazi pembeni, akaja Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akaziba ule uwazi. Na jengo au nyumba nzuri ni mfano wa Ujumbe wa juu kutoka mbinguni ambao alioutuma Allah mtukufu tangu zama za Nabii Adamu (amani iwe juu yake) mpaka zama za Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake).

"Na kwa yakini tuliwatuma Mitume kabla yako, wengine katika hao tumekusimulia (majina yao na habari zao) na wengine hatukukusimulia. Na haikuwa kwa Mtume yeyote kuleta muujiza wowote ila kwa idhini ya Allah. Na itakapokuja hukumu ya Allah kutahukumiwa kwa haki, na wafanyao mambo ya batil watapata hasara wakati huo". Suratu-Ghaafir aya (78)

"Semeni nyinyi (Waislamu waambiwe Mayahudi na Manasara; waambieni): Tumemwamini Allah na yale tuliyoteremshiwa, na yale yaliyoteremshwa kwa Ibrahim na Ismaili na Is-haqa na Yaaqubu na kizazi (chake Yaaqubu), na waliyopewa Mussa na Issa na pia yale waliyopewa Manabii (wengine) kutoka kwa Mola wao, hatutafautishi baina ya yoyote katika hao (wote tunawaamini) na sisi tumenyenyekea kwake".

Suratul-Baqarah aya (136).

## Tawrati, Injili na Qur-an ni vitabu vya Allah kwa binadamu

Nguzo za imani katika Uislamu ni kumuamini Allah na Malaika wake na vitabu vyake, na Mitume yake, na siku ya mwisho, na kuamini maamuzi ya Allah katika kheri yake na shari yake. Basi ni lazima kila Muislamu kuamini vitabu vya mbinguni ambavyo ameviituma Allah mtukufu kwa viumbe, kama Suhufi Ibrahimu, na Taurati ambayo ameiteremsha Allah kwa Nabii Mussa (amani iwe juu yake), na Zaburi ambayo Allah alimpa Nabii Daudi, na Injili ambayo Allah amempa Nabii Issa (amani iwe juu yao).

Na wala Qur-an tukufu haipingani na vitabu vya mbinguni vilivyotangulia kwa sababu vyote vimekuja kutoka katika chimbuko moja, na Qur-an tukufu ndio khitimisho la sheria zote, nacho ni kitabu cha mbinguni pekee kilichokusanya maneno ya Allah mtukufu kimatamshi na maana, na wala hayajaingiliana na matamko yoyote katika viumbe kama ambavyo ilivyotokea katika vitabu vya mbinguni vilivyo tangulia.

Allah ameihifadhi Qur-an tukufu kutokana na ubadilishwaji, na ndani yake imesahihisha kila ubadilishaji uliofanyika kwa vitabu vya mbinguni vilivyo tangulia, kwa hilo Qur-an tukufu inakuwa ni Muujiza wa kudumu milele wanapokeana kizazi baada ya kizazi mpaka kisimame kiama.

"Hakika tuliteremsha Tawrati yenye uwongofu na nuru, ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Allah) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia (walihukumu kwa hio Tawrati) kwa sababu walitakiwa kuhifadhi kitabu (hicho) cha Allah nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi (nyinyi Waislamu) msiwaogope watu, bali niogopeni (mimi). Wala msibadilishe aya zangu kwa thamani chache (ya duniani) na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Allah basi hao ndio Makafiri".

Suratul- Maida aya ya 44

"Watu wa Injili wahukumu kwa yale aliyoyateremsha Allah ndani yake. Na wasiohukumu kwa (kufuata) yale aliyoyateremsha Allah basi hao ndio waasi". Suratul- Maida aya 47

"Na tumekuteremshia kitabu kwa (ajili ya kubainisha) haki, kinachosadikisha vitabu vilivyokuwa kabla yake, na kuvihukumia (kama haya ndiyo yaliyoharibiwa au ndiyo yaliyosalimika). Basi wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Allah, wala usifuate matamanio yao kwa kuacha haki iliyokufika, na kila (umma) katika nyinyi (binaadamu) tumeujaalia Sharia yake na njia yake, na kama Allah angetaka angekufanyieni kundi moja (la kufuata Sharia moja) lakini anataka kukujaribuni kwa hayo aliyokupeni, basi shindaneni kuyafikilia mambo ya kheri, nyinyi nyote marudio yenu ni kwa Allah, naye atakwambieni (yote) yale mliyokuwa mkikhitilafiana". Suratul- Maida aya 48

"Hao ndio aliowaneemesha Allah miongoni mwa Manabii, katika kizazi cha Adam, na katika (kizazi cha) wale tuliowachukuwa pamoja na Nuhu (jahazini), na katika kizazi cha Ibrahimu na Israili, na katika wale tuliowaongoza na tukawachagua. Wanaposomewa aya za Allah huanguka kusujudu na kulia".

Suratu Mariyam aya ya 58

| Nabii au Mtume | Ibrahimu | Mussa | Issa[1] | Muhammad |
|---|---|---|---|---|
| Maisha yake takribani | 1700 Kabla ya kuzaliwa Issa | 1400 Kabla ya kuzaliwa Issa | 1-33 Miladia | 232-570 Miladia |
| Umri wake (kwa kukadiria) | 175 | 120 | 33 | 63 |

## Mtume Muhammad na Mtume Ibrahim (rehema na amani ziwe juu yao)

Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) anazingatiwa ni baba wa Manabii mbele za Mayahudi, Wakiristo na Waislamu kwa sababu ya Manabii wote waliokuja baada ya Nabii Ibrahim wanatokana na kizazi chake (Nabii Issa mtoto wa Bibi Maryam (amani ziwe juu yao) anatokana na kizazi cha Nabii Ibrahim vile vile kupitia mama, na hana baba). Na wanaamini Waislamu kuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) anatokana na kizazi cha Nabii Ismaili (amani iwe juu yake) ambae mtoto wa mwanzo wa Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) na ndie hunasibika kwake wengi katika makabila ya Waarabu. Ama Manabii wa Bani Israili kwa mfano Nabii Yaqubu, Nabii Yussuf, Nabii Ayyub, Nabii Mussa, Nabii Zakaria na Nabii Yahya (amani ziwe juu yao) hawa wanatokana na kizazi cha mtoto wake wa pili (Nabii Ibrahim) Nabii Is-haka (amani ziwe juu yake). Nabii Ibrahim (amani iwe juu yake) alimuoa Bibi Sara, lakini Allah hakuwaruzuku mtoto kipindi cha ujana wao. Nabii Ibrahim (amani iwe juu yake) akamuoa Bibi Hajar akazaa nae Nabii Ismail (amani iwe juu yake). Na baada ya kufikia utuuzima Bibi Sara na kuwa kikongwe

[1]- Kisha Allah amemnyanyua kwake, na atateremka duniani kabla ya kusimama Kiama.

Allah mtukufu alimkadiria kuchukuwa mimba ya Muujiza katika hali ya utuuzima wake, akamzaa Nabii Is-haka (amani iwe juu yake). Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) alitambuwa uwepo wa Allah mtukufu na upweke wake na akajitolea maisha yake kusomesha watu Imani ya Tauhidi na kwamba Mola wao hawezekani awe ni Sanamu au Moto au Jua au Mwezi bali yeye Allah mtukufu ni Muumbaji wa kila kitu na yeye ni mmoja hana mshirika. Na Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) amewacha mfano mkubwa katika historia kwa kujitolea kwake na kujisalimisha na amri ya Allah kwa kauli na vitendo. Akajitolea pale walipomtupa watu wake katika moto pasi na kurudi kuiacha Imani ya Tawhidi, akamuhamisha mke wake wa pili Bibi Hajar na mwanawe mdogo Nabii Ismail (amani iwe juu yake) kwenye jangwa lisilo na mazao wala maji katika Bara Arabu kwa kutekeleza amri ya Allah mtukufu na mwenye yakini naye, kisha akataka amchinje mwanawe Nabii Ismail ambae alichukua miaka mingi kumpata, amchinje kwa ajili ya kuitekeleza amri ya Allah ambayo aliitambuwa Nabii Ibrahim kutokana na ndoto aliyoiona katika usingizi wake .



"Na nani aliyebora kwa dini kuliko yule ambaye ameuelekeza uso wake kwa Allah naye ni mwema, na anafuata mila ya Ibrahimu (kuwa Muislamu kweli kweli) Na Allah amemfanya Ibrahimu kuwa ni kipenzi chake"

Suratu-Nisaa aya ya 125

"Na nani atajitenga na mila ya Ibrahimu (akaichukia dini hii ya Kiislamu) isipokuwa anaitia nafsi yake katika upumbavu? na kwa yakini sisi tulimchagua (Ibrahim) katika dunia, na kwa hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema (kabisa)."

Suratul-Baqarah aya ya 130.

**Mungu Mmoja hana Mshirika**

Yakini ya Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) kuwa Allah yuko ilikuwa juu ya kila kitu, na ilikua Imani yake kwa Allah inalingana na Imani ya umma, basi Allah akamchagua Nabii Ibrahim (amani iwe juu yake) kuwa kipenzi chake (na imethibiti sifa hii katika vitabu sahihi vya zamani) na akamfanya kuwa ni imamu kwa watu, pia amemsifu kuwa yeye ni mwenye kumtii Mola wake, na yuko mbali na batili.

"Hakika Ibrahimu alikuwa Imamu (mfano mzuri wa wema wa kuigwa), mnyenyekevu kwa Allah, mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina (120) (alikuwa) Mwenye kuzishukuru neema zake (Allah zilizo juu yake). Akamchagua na kumuongoza katika njia iliyonyooka (121) Na tukampa wema katika dunia, na hakika yeye katika Akhera atakua miongoni mwa watu wema (pia) (122)Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahimu (aliyekuwa) mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina(123)" Suratu-Nahli aya 120-123.

Na Waislamu wanachunga kumpa Nabii Ibrahim (amani iwe juu yake) heshima kubwa kwa sababu yeye ndiye aliyewapa jina la Waislamu (yaani wale waliojisalimisha kwa Allah mtukufu na wakatii amri zake na wakaishi maisha yao ya kwa mfumo wa Allah.

“Ibrahim hakuwa Myahudi wala Mkiristo, lakini alikuwa mwongofu, mtii, wala hakuwa katika Washirikina (67) Watu wanaomkurubia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeye (katika zama zake) na Mtume (Muhammad) huyu na waliomuamini (Mtume huyu). Na Allah ndie mlinzi wa wenye kuamini”. Suratu-Aal-Imraan aya 67-68.

Qur-an tukufu inataja kwamba Allah mtukufu amemuamrisha Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) kuinua nguzo kwenye nyumba ya mwanzo iliyowekwa kwa ajili ya watu katika Ardhi kwa ajili ya kumpwekesha Allah mtukufu na kumuabudu yeye, na Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) kwa kusaidiwa na mwanawe Nabii Ismail (amani iwe juu yake) walizinyanyuwa kuta za nyumba (Al-Ka'ba tukufu) na akanyanyua mpaka ukawa kama ulivyo leo takriban, nayo (Al-Ka’ba) ipo ndani ya Msikiti mtukufu katika mji Mtukufu wa Makka.

“Na (kumbukeni khabari hii pia) tulipoifanya nyumba (ya Al-Ka’ba) iwe pahala pa kuendewa na watu na mahala pa salama, na mahali alipokuwa akisimama Ibrahimu pafanyeni pawe pa kusalia. Na tulimwusia Ibrahimu na Ismaili (tukawaambia): “itakaseni (isafisheni) nyumba yangu kwa ajili ya wale wanaoizunguka kwa ajili ya kutufu na wanaokaa hapo na (kwa ajili ya) wanaorukuu na kusujudu pia”. Suratul-Baqarah aya ya 125

## Dua ya Nabii Ibrahimu na Nabii Ismail (amani iwe juu yao).

"Ee, Mola Wetu! Utufanye tuwe wanyenyekevu kwako. Na miongoni mwa kizazi chetu (pia ufanye) umma mnyenyekevu kwako. Na utuonyeshe njia ya ibada yetu na utusamehe: Bila shaka Wewe ndiye Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu."

Suratul-Baqarah aya ya 128.





## Hija ni Ibada ya Nabii Ibrahim

Kila mwaka takribani Waislamu milioni tatu hukusudia Msikiti mtukufu wa Makka kwa ajili ya kutekeleza faradhi ya Hija katoka nchi mbali mbali ulimwenguni, hakika Waislamu wamechukua Sharia na faradhi hii kutoka katika Qur-an na mafundisho ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake), nayo kwa ujumla ni Sharia ya Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake), yaani inafungamana na matendo ya Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) na mkewe Bibi Hajar.

**Twawafu**: Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alifanya Twawafu kuizunguka Al-Ka'ba, na maana ya neno "Twawafu'' ni mwendo wenye kuzunguka pembezoni mwa Al-Ka'ba tukufu katika kunyenyekea kwa ajili ya Allah mtukufu mara saba kwenda kinyume na mzunguko wa saa. Twawafu inazingatiwa ni aina ya Sala na ibada ambayo hutakiwa twahara na ndani yake kuna dua na kusoma Qur-an na kunyenyekea kwa ajili ya Allah mtukufu na kutubu kwake.

Twawafu inaendana na mzunguko wa Dunia, Mwezi, Jua, na Sayari hata na mwendo wa Elektroni kuzunguka kiini cha Atomi ambao unazunguka mzunguko mmoja kama wa Twawaf, na





unawakilisha mzunguko huu unyenyekevu kwa kanuni za Allah kiulimwengu na nidhamu yake kwa viumbe vyake. “Haliwi jua kulifikia mwezi, (wakati wa nguvu zake) wala usiku kuupita mchana, (ukaja kwa .ghafla kabla ya wakati· wake). Na vyote vinaogelea katika njia (zao)” Suratu Yasin aya ya 40.

“Zinamtukuza zote mbingu saba na ardhi na vilivyomo ndani yake. Na hakuna chochote ila kinamsabihi (Allah) kwa sifa Zake njema. Lakini nyinyi hamfahamu . kusabihi (kutukuza) kwake. Hakika Yeye Allah ni Mpole (na) Mwingi wa kusamehe” Suratu Israa aya ya 40.

**Kisimamo cha Nabii Ibrahim (amani iwe juu yake):** Baada ya kuzunguka pembezoni mwa Al-Ka'ba, Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alisali rakaa mbili nyuma ya Maqamu Ibrahim, nayo ni sehemu aliyosimama juu yake Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) kwa ajili ya kujenga Al-Ka'ba na ndani yake mpaka hivi sasa lipo jiwe ambalo alikua akinyanyukia, na baadae pamejengewa juu ya Maqamu Ibrahimu jengo la madini na pembezoni mwake kuna vioo kama inavyoonekana kwenye picha. Muislamu anasimama kwa ajili ya kusali nyuma ya sehemu hii kwa kufuata mwenendo wa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake), kama alivyosimama Imamu wa Waislamu Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) ambae alinyanyua misingi ya Al-ka’ba na kujenga jengo lake kwa kufuata amri ya Allah, ili iwe nyumba ya Allah mmoja mpweke anayekusudiwa na kila muumini mpwekeshaji katika ardhi yote.



**Sa'yi**: Alitembea Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) baina ya kilima cha Swafaa na kilima cha Marwa nayo ni sehemu ambayo alitembea Bibi Hajar akiwa anatafuta maji kwa ajili ya mwanae mchanga Nabii Ismail (amani iwe juu yake) baada ya kuachwa mahala hapo na Nabii Ibrahimu (amani ziwe juu yake) akiwa anatekeleza amri ya Allah mtukufu, na Allah Mtukufu alitaka pawe pahala hapo ni sehemu ya Ibada na Amani kwa watu wote. Na kwa Muujiza kutoka kwa Allah Mtukufu yalichimbuka maji matamu yenye kufaa kwa ajili ya kunywa kutoka chini ya nyayo za mtoto wa Bibi Hajar; Nabii Ismail (amani iwe juu yake), na kwa uwezo wa Allah maji haya yameendelea kutoka mpaka sasa na wanakunywa kutokana na maji hayo wakaazi wa Makka na mamilioni ya Mahujaji na wafanya Ibada ya Umra ambao wanazuru katika kila mwaka Msikiti Mtukufu katika mji Mtukufu wa Makka.

Hukusudiwa jina la "Sa'yi" ni mwendo baina ya kilima cha Swafa na Marwa mara saba huitwa kila mwendo mzunguko, na baina ya kilima cha Swafa na kilima cha Marwa yapo masafa yanayokadiriwa kiasi cha Mita 395, kwa hivyo inakuwa mkushanyiko wake wa masafa ya Sa'yi ni Mita 2760, Hakika Bibi Hajar aliikubali amri ya Allah Mtukufu na akaridhika kubakia katika sehemu hii ya jangwa akaishi hapo miaka mingi yuko mbali na mume wake mpaka wakaja watu kufanya makazi ukawa ni mji wenye wakaazi, ikawa maisha yake na utafutaji wake ni kwa ajli ya Allah pekee. Na pindi



Muislamu anapotekeleza ibada hii basi airejeshe Sa'yi yake katika maisha yake (kwa kutafakari) na akumbuke maneno ya Allah mtukufu katika kitabu chake kitukufu: "Na kwamba mtu hatapata ila yale aliyoyafanya (39) Na kwamba amali yake itaonekana (40) Kisha atalipwa malipo yaliyo kamili(41) Na kwamba mwisho (wa kila jambo) unarejea kwa Mola wako" Suratu-Najm aya ya 39-42.

Na amesema Allah Mtukufu:

"Sema: Je! Tukujulisheni wenye hasara katika vitendo (vyao)? (103) Hao ambao bidii yao (hapa duniani) imepotea bure katika maisha ya dunia, nao wanafikiri kwamba wanafanya amali njema!" Suratul- Kahf aya ya 103-104.




Kurusha mawe: Na kati ya Ibada ya Hija ni (Rajm) na inakusudiwa kurusha vijiwe, Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) katika Hija yake alienda sehemu inayoitwa hivi sasa "Jamarati" nayo ni sehemu katika mji wa Mina ambayo inapatikana mashariki ya msikiti mtukufu wa Makka. Na ibada hii ya kurusha vijiwe inazingatiwa kuwa ni kukiiga kile alichokifanya Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) wakati alipomrushia Iblisi vijiwe mara nyingi wakati alimdhihirikia kwa umbile la mtu mkongwe wa umri, na akajaribu kumzuwia asitii amri ya Allah Mtukufu ya kumchinja mwanawe Nabii Ismail (amani iwe juu yake) kwa lengo la kujikurubisha kwa Allah. Basi wakati Muislamu anatekeleza faradhi ya Hija hakika anakuwa anatekeleza kitu ambacho alikifanya Nabii Ibrahimu (amani ziwe juu yake), na kufanya hivyo ni kumpa ushindani Shetani na kuishinda nafsi inayoamrisha uovu na shari zake.

Kuchinja: Kama ambavyo Allah Mtukufu alivyomkombowa Nabii Ismail (amani iwe juu yake) kwa Kondoo Mtukufu baada ya baba yake Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) alipotaka kumchinja kwa ajili ya Allah Mtukufu, ikawa kuchinja ni katika ibada za Hija (Hija ya Tamatui na Qirani, na inawezekana akawa mnyama wa kuchinja ni Ngamia au Ng'ombe, na hukmu zake zipo katika vitabu vya Fiqhi). Na amewafundisha Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) Waislamu watangulize wanyama kwa Allah Mtukufu na wachinje mbuzi katika Idi ya kuchinja ili kuigawa nyama yake kwa mafakiri.

Hakika wasifu mzuri zaidi wa kujisalimisha Nabii Ibrahimu na mwanae (amani ziwe juu yao) katika maamrisho ya Allah ni ule uliokuja katika Qur-an Tukufu Suratu-Saaffati.

“Basi wote wawili walipojisalimisha (kwa Allah), na akamlaza kifudifudi (amchinje) (104) Pale pale tulimwita: "Ewe Ibrahimu:" (105) "Umekwishasadikisha ndoto. (Usimchinje mwanao)." Kwa yakini hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema (106) Bila shaka (Jambo) hili ni jaribio lililo dhahiri, (mtihani ulio dhahiri) (107) Basi tukamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa mtukufu (108) Na tukamuachia (sifa nzuri) kwa (watu wote) waliokuja baadaye (109) Amani kwa Ibrahimu (110) Hivi ndivyo tunawalipa watendao mema (111) Bila shaka yeye alikuwa miongoni rnwa waja wetu waliomini (kweli kweli).”

Suratul-Saaffati aya aya 103-111.

Na mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amefundisha Waislamu kukhitimisha kila Sala katika Sala zao kwa dua inayoitwa (Salatu-Ibrahimiya) na tamko lake ni: “Allahumma Salli alaa Muhammad wa alaa Aali Muhammad kamaa Sallayta alaa Ibrahim wa alaa Aali Ibrahim, wabaarik alaa Muhammad wa alaa Aali kamaa baarakta alaa Ibrahimu wa alaa Aali Ibrahim fil aalamina innaka hamaidun majiidu.”

Na imekuja katika hadithi kwamba mmoja wa Masahaba alimuita Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): “Ewe mbora wa viumbe” Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akamjibu kwa unyeyekevu: “Huyo ni Ibrahimu kipenzi cha Allah Mtukufu” Amepokea Muslim (2369).

Na kuna umuhimu wa kuashiria ya kwamba Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amemuita mmoja wa watoto wake jina la “Ibrahimu” ambae alimzaa Bibi Mariyah Al- Qibtiyya lakini alifariki akiwa bado mtoto mdogo na alihuzunika sana Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika kifo chake.

“Sema: "Kwa hakika mimi Mola wangu ameniongoza katika njia iliyonyoka, (katika) dini iliyo sawa kabisa ambayo ndiyo dini ya Ibrahimu aliyekuwa mwongofu; wala (kabisa) hakuwa miongoni mwa washirikina." (162) Sema: "Hakika Sala yangu, na ibada zangu (zote nyingine) na uzima wangu, na kufa kwangu; (zote) ni kwa Allah. Muumba wa walimwengu wote (Likinisibu jambo limenisibu kwa kutaka Allah si kwa kutaka viumbe vyake. Na yote ninayoyafanya nayafanya kwa ajili yake)." (163) “Hana mshirika wake. Na haya ndiyo niliyoamrishwa, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha (kwa Allah)." (164) Sema: "Je, nishike mola mwengine asiyekuwa Allah, na bali Yeye (Allah) ndiye Mola wa kila kitu?" Wala nafsi yoyote haichumi (ubaya) ila ni juu yake; (hatalipwa kiumbe mwingine kwa ubaya wake). Wala mbebaji (mizigo yake ya dhambi) hatabeba mizigo ya mwingine (kumsaidia). Kisha marejeo yenu (nyote) ni kwa Mola wenu. Naye atakuambieni yale mliyokuwa mkihitalifiana” Suratul- An’ami aya ya 161 – 164.



Msikiti wa Al-Ibrahimiy katika mji wa Al-Khalil ulioko, Palestina.







Kaburi la Nabii Ibrahim

Nabii Ibrahimu (amani ziwe juu yake) amezikwa katika mji wa Al-Khalili ulioko Palestina lakini sehemu ya kaburi lake hasa haijulikani isipokuwa watu wakajenga kaburi, na kwa sasa limo ndani ya eneo la Msikiti wa Al-Ibrahimiy. Na unazingatiwa msikiti Al-Ibrahimiy ni katika Misikiti ya zamani katika mji wa Al-Khalil, ni msikiti ulio mashuhuri, na waliugeuza Kanisa katika kipindi cha vita vya msalaba, kisha ukarudi tena Msikiti katika zama za utawala wa Salahu-Dini Ayyubi.

Na Msikiti huo una umbile la marefu na umezungukwa na ngome kubwa na una minara miwili yenye pembe nne.

Msikiti Al-Ibrahimiy unakusanya vyumba vingi, ndani yake kuna kaburi la Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yae) na mke wake Bibi Sara na mwanawe Nabii Is-haqa na mke wake Rifqah bint Batuueel (na yeye ni mtoto wa ami yake Naahur bin Azar) na chumba cha upande wa kaskazini yapo makaburi mawili, kaburi la Nabii Ya'qub na mke wake Laikaa kwa mujibu wa simulizi za Kinasara, na makaburi haya yapo kabla ya Uislamu na wala Waislamu hawajayagusa kwa ubaya.



Picha ya mji wa Al-Khalil, mtaa uliozunguka Msikiti wa Nabii Ibrahim







# Musa, Nabii ambaye Mungu alizungumza naye

## Mtume Muhammad na Nabii Mussa (amani ziwe juu yao).

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amemsifia ndugu yake Nabii Mussa na ametupa habari ya kuwa Nabii Mussa (amani iwe juu yake) atasimama siku ya Kiama (siku ya hukumu) pembeni mwa Arshi ya Allah na akiwa ameikamata.

Amepokea Bukhari katika "Jamii Sahih" (4/157) namba (3408), (4/159) namba (3414).Na Muslim katika "Jamii Sahih" (7/100) namba (2373), (7/101) namba (2373) Kutoka kwa Abu Huraira (radhi za Allah ziwe juu yake).




Na wakati Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alipofika mji wa Madina aliwakuta Mayahudi wakifunga siku ya tarehe kumi ya mwezi wa Muharam nao ni mwezi wa mwanzo kwa hesabu ya kalenda ya Kiislamu

Na siku ya 10 ya mwezi wa Muharam ni siku ambayo Allah mtukufu amemuokoa Nabii Mussa na watu wake Bani Israil kutokana na Firauni wa Misri baada ya kupasuliwa bahari na kupita na Allah Mtukufu kumuangamiza Firauni na jeshi lake. Basi hio ni siku ambayo haki imeishinda batili na Allah Mtukufu akawaokoa wanaodhulumiwa dhidi ya Madhalimu. Nabii Mussa akafunga kwa kumshukuru Allah Mtukufu.

Na Mtume Muhammad (rehma na amani ziwe juu yake) akawahimiza Waislamu kufunga siku hio na kuifanya funga hii kuwa Sunna.

Qur-ani Tukufu imeelezea ya kuwa Allah Mtukufu amemsemesha Nabii Mussa (amani iwe juu yake) kwa njia ya mazungumzo na Allah Mtukufu akamsifia Nabii Mussa (amani iwe juu yake) kupitia Qur-ani Tukufu kuwa yeye ni miongoni mwa Mitume waliopata tabu sana Mitume ambao Allah Mtukufu amewapa mambo muhimu na makubwa nao ni Nabii Nuhu, Nabii Ibrahimu na Nabii Mussa na Nabii Issa na Mtume Muhammad (rehema na amani).

Na pia Qur-ani imeeleza kisa cha Nabii Mussa (amani iwe juu yake) kwa undani katika maeneo mbali mbali na ukiangalia visa vya wana wa Israil na mafunzo yanayopatikana kwao yanakaribia thuluthi ya Qur-ani Tukufu takribani.

Nabii Mussa (amani iwe juu yake) amekufa katika sehemu ya karibu na inayotizamana na Msikiti wa Aqswa, nayo kwa sasa ipo Jodan.

Angalizo: Mlima Mauab Nibu - ambayo ni sehemu aliyopita Nabii Mussa (amani iwe juu yake) - imekuwa ni sehemu ya utalii nchini Jodan










Na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ameelezea sehemu alozikwa Nabii Mussa (amani iwe juu yake) hiyo sehemu ipo karibu na udongo mwekundu kwenye njia ya kwenda Ardhi Tukufu.

Na mwisho Waislamu wanaona mambo mengi yanafanana baina ya Mtume Muhammad na Nabii Mussa (rehema na amani ziwe juu yao).

Wote wawili ni Manabii na Mitume, Allah Mtukufu amewateremshia vitabu kutoka mbinguni na vyenye kubeba Sharia za Allah Mtukufu. Na wote wawili wamehama miji yao na kisha wakarejea.

Na pia kila mmoja alikuwa kiongozi katika watu wake na Mtume wa Allah Mtukufu na wote wawili wameishi muda mwingi katika zama na watu wao na wote walioa na wakapata watoto.



## Mtume Muhammad na Nabii Issa (rehema na amani ziwe juu yao)

Amesema Mtume Muhammad kuhusu Nabii Issa bin Maryam (rehema na amani ziwe juu yao)

"Mimi ni mbora zaidi kwa ukaribu na mtoto wa Maryam (Nabii Issa) hapa duniani na Akhera, hakuna baina yangu na yeye Mtume mwengine, Na Mitume wote ni ndugu, ni watoto wa kizazi kimoja (baba mmoja) mama zao tofauti, na dini yao moja" Amepokea Bukhari (3285). Neno "Al-'Allaati" (lililotumika katika hadithi) katika lugha ya Kiarabu lina maana ya ndugu wa mama tofauti.

Qur-ani Tukufu inaelezea mazazi ya Nabii Issa bin Maryam yalikuwa pasi na baba kwa njia ya Miujiza katika Suratu Maryam:

Na mtaje Mariamu Kitabuni (humu). Alipojitenga na jamaa zake, (akenda) mahali upande wa mashariki (ya Msikiti) (17) Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea Muhuisha Sharia yetu (Jibril) akajimithilisha.ithilisha kwake (kwa sura ya) binadamu aliye kamili (18) "(Mariamu) akasema: "Hakika mimi najikinga kwa - (Allah) Mwingi wa rehema (aniepushe) nawe. Ikiwa unamuogopa Allah (basi ondoka nenda zako)". (19) (Malaika) akasema: "Hakika mimi ni Mjumbe wa Mola wako: ili nikupe mwana mtakatifu." (20) Akasema: "Ninawezaje kupata mtoto, hali hajanigusa mwanamume (yoyote kwa njia ya halali) wala mimi si (mwanamke) mwenye kuzini."(21)(Malaika) akasema: "Ni kama hivyo (unavyosema; lakini) Mola wako amesema: 'Haya ni sahali kwangu, na ili tumfanye Muujiza kwa wanaadamu na rehema itokayo kwetu (ndiyo tumefanya hivi);' Na hili ni jambo lililokwisha hukumiwa."(22)Basi akachukua mimba yake, na akaondoka nayo mpaka mahali pa mbali.(23) Kisha uchungu ukampeleka katika shina la mtende, (akawa anazaa na huku) anasema: "Laiti ningekufa kabla ya haya, na ningekuwa niliyesahaulika kabisa."

Suratu-Maryam aya ya 16-23.



Nasirat ni miongoni mwa miji muhimu ya Palestina kihistoria, lipo Kanisa la Katoliki ambalo hujulikana pia kwa jina Bishara ya Bazilika. Na kwa mujibu wa itikadi za Wakiristo kuwa limeanzishwa kanisa katika sehemu ya nyumba ya Bibi Maryamu

Na kwa mujibu wa kisa cha Bibi Maryam (amani iwe juu yake) katika Qur-ani Tukufu kwamba Bibi Maryamu amembeba mtoto wake (baada ya kujifungua) na akarejea kwa watu wake, wakampinga kuwa na mtoto pamoja nae na kumuelekezea shutuma (lawama) lakini Miujiza ya kiungu ilimtamkisha.

"(Yule mtoto) Akasema: "Hakika mimi ni mja wa Allah, Amenipa Kitabu na Amenifanya Nabii, (30) "Na Amenifanya mbarikiwa popote nilipo. Na Ameniusia Sala na Zaka maadamu ni hai."(31) "Na (ameniusia) kumfanyia merna mama yangu: Wala hakunifanya niwe jeuri, muovu."(32) "Na amani iko juu yangu siku niliyozaliwa na siku nitakayokufa na siku nitakayofufuliwa kuwa hai"(33) Huyu ndiye Issa bin Mariamu. (Hii) ndiyo kauli ya haki ambayo (Wakristo) wanaifanyia shaka." (34) "Haiwi kwa Allah kufanya mtoto;Ametakasika. Anapolitaka jambo basi huliambia tu kuwa; nalo likawa." (35)
Suratu-Maryam aya ya 30-35

Na imekuja Qur-ani Tukufu kumsifia Nabii Issa (amani iwe juu yake) katika sehemu nyingi ndani yake kwamba yeye ni neno la Allah Mtukufu na Roho itokayo kwake, Allah Mtukufu amemuunga kwa kumteremshia Jibril (amani iwe juu yake) Na akamtumiliza kuwa Mtume kwa watu wa Bani Israil ili kuwaongowa kwenye njia iliyonyooka.

Na Qur-ani ikamsifu Nabii Issa (amani iwe juu yake) kwamba yeye ni Mtukufu duniani na Akhera nae ni katika wa karibu (wenye kujikurubisha) kwa Allah Mtukufu, Na Allah Mtukufu akamfundisha kitabu na Hekima na Taurati na Injili, na akamjaalia uwezo kwa idhini yake kuwaponya vipofu na wenye Ukoma, na kuwafufua walokufa na kuwajuulisha watu wanachokula na kuhifadhi katika majumba yao.



Kanisa la Mahdi katika mji wa Bathlehem - Palestina - ni kanisa kongwe duniani, na Wakiristo wengi wanaitakidi kuwa Nabii Issa (amani iwe juu yake) kazaliwa katika sehemu hiyo.

Je, Masihi atarudi?

## Kurejea kwa Nabii Issa "Masihi" (amani iwe juu yake) kwa mtazamo wa Uislamu

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amewabashiria Waislamu kurejea kwa Masihi Nabii Issa mwana wa Maryamu (amani iwe juu yake) katika zama za mwisho, na yeye pindi akirejea atakuja kuwa kiongozi wa Waislamu katika zama hizo, na yeye ndie atakaekuja kupambana na Masihi Dajjali (Mwenye jicho moja) atamuuwa na kuondoa uovu na kuwaunganisha wenye kumuamini Allah Mtukufu na basi watakuwa wenye itikadi ya kumpwekesha Allah Mtukufu mmoja na wataifuata dini ya Kiislamu, na atahukumu kwa uwadilifu na kheri itaenea kwa watu.







Picha za mji wa Damascus -Syria: kwa mujibu wa baadhi ya mapokezi ni kwamba Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ameashiria kuwa Masihi Issa (amani ziwe juu yake) atarudi na atashuka kutoka mbinguni kwenye eneo la mashariki mwa mji wa Damascus.

## Uislamu ni Ujumbe wa Allah Mtukufu kwa binaadamu wote

Ujumbe wa Uislamu haukuwa kwa Waarabu peke yao bali ametaka Allah Mtukufu umfikie kila mtu. Baada ya kufikisha Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) Ujumbe kwa watu wake alituma wajumbe wake nje ya Bara Arabu ili wafikishe ujumbe wa Allah Mtukufu kwa waja wake katika kila pande ya dunia.

“Na Hatukukutuma hatukukuleta ila kwa watu wote, uwe Mtoaji wa habari nzuri na Muonyaji; lakini watu wengi hawajui (lolote, wanajifuatia tu waliyowakuta nayo wazee wao)” Suratu-Sabai aya ya 28.

**Mfalme wa Roma Heraclius amepokea barua ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake)**

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ametuma wajumbe na barua kwa Wafalme na Maraisi na Watawala wa Nchi za Jirani ya Bara Arabu, nayo ni yale yaliyokuwa ni mataifa makubwa kwa wakati huo. Mfano wa Fursi, Byzantin, Misri, akiwaita katika kumuamini Allah Mtukufu na Ujumbe wa Uislamu.

Mfalme wa Roma Heraclius alipoipokea barua ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake), aliuliza ikiwa katika mji wake yupo mtu kutoka mji wa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juwe yake), ikabahatika kuwepo kwa Abuu Sufyani na biashara zake katika mji wa Sham. Heraclius akamuita Abuu Sufyani akamuliza kuhusu Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na akamuweka mtarjuma, akauliza Heraclius: Vipi nasabu yake kwenu? Na anasimulia kisa hiki Abuu Sufyani mwenyewe: Nikasema, yeye kwetu ni mwenye nasabu tukufu.

Akasema Heraclius: je! Wazee wake walikuwa Wafalme?.
Nikasema: Hapana.

Akasema Heraclius: Je! Mlikuwa mnamtuhumu kwa uwongo kabla ya kudai madai anayoyasema?
Nikasema: Hapana.

Akauliza Heraclius: Je! Anafuatwa na watu watukufu au wanyonge?.
Nikasema: Hapana, bali wanyonge ndio wanaomfuata.

Akasema Heraclius: Wanazidi au wanapungua?
Nikasema: Hapana, bali wanazidi.

akasema Heraclius: Je! Wanaritadi miongoni mwao katika dini yake kwa kuichukia baada ya kuikubali?.
Nikasema: Hapana.

Akasema Heraclius: Je! Mmepigana nae?
Nikasema: Ndio.

Akasema Heraclius: Yalikuwa vipi mapigano yenu na yeye?
Nikasema: vinakuwa vita baina yetu na yake ushindi wa zamu mara anatushinda na mara nyengine tunamshinda.

Akasema Heraclius: Je! Anasaliti?
Nikasema: Hapana

Akasema Heraclius: Je! Amewahi kuyasema maneno haya (yaani ya kulingania watu kuamini Ujumbe wa Allah Mtukufu) kwa yoyote kabla?
Nikasema: Hapana.

Akasema Heraclius: Anakuamrisheni nini?
Nikasema: Anatuamrisha kusali na kutoa Zakka, na kuunga jamaa na kujizuia na machafu.

Akasema Heraclius: Ikiwa mliyosema yote ni kweli; Hakika yeye ni Mtume, na nilikuwa najua kuwa atatokea, na sikudhania kama atakuwa miongoni mwenu. Lau ningejuwa nitamfikia vipi ningelienda kukutana nae, na lau ningekuwa mbele yake ningemkosha miguu yake. Na Ufalme wake utafika chini ya Miguu yangu

Angalizo: Heraclius ametawala Ufalme wa Kirumi katika kipindi cha baina ya mwaka 610-640 AD. Katika kipindi hicho aliwashambulia Kijeshi Wafursi (Waajemi) mara tatu na wakashindwa Wafursi na wakarejesha utawala wa Siria, Palastine na Misri. Na mwaka wa 636 AD Uislamu uliingia Palestine, Siria na Misri na sehemu kubwa ya kaskazini ya Afrika, na mwaka 642 AD Uislamu uliingia miji ya Fursi.

## Uislamu ni Dini ya Ulimwengu mzima

Inahesabika Uislamu kwa sasa ni dini ya pili kwa ukubwa baada ya Ukristo. Na tafiti zinaashiria kuwa idadi ya Waislamu imefikia Bilioni 1.57 katika mwaka 2010, nao ni asilimia 23% kwa idadi ya wanaoishi duniani kote ambayo inafikia watu Bilioni 6.8, na kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2015 idadi ya Waislamu duniani ilizidi kuongezeka kufika Bilioni 1.8. (Pew Forum on Religion & Public Life).

Na idadi ya Wakristo ni Bilioni 2.1 takribani sawa na asilimia 33% ya idadi ya watu duniani. Ama idadi ya dini ya Mayahudi ni takriban Milioni 16 sawa na asilimia 0.22% kwa idadi ya watu wote wa duniani.

## Je! Waislamu wote ni Waarabu?

Waislamu wa Kiarabu ni chini ya robo ya idadi ya Waislamu waliopo duniani. Pamoja na kwamba dini ya Uislamu imekuja kwa lugha ya kiarabu lakini idadi kubwa ya Waislamu sio Waarabu, na hii inatujuulisha kwamba Waarabu walijishughulisha kufikisha Ujumbe nje ya mipaka ya Bara Arabu, wakaufikisha kwa ukweli na nia safi kwa watu wote.



## Maangalizo

1. Waislamu na Wakristo na Mayahudi idadi yao inafika Bilioni 3.65-3.89 kwa makadirio. Na hii inamaanisha nusu ya wanaoishi duniani wanatambua uwepo wa Allah Mtukufu, ama nusu nyengine wanaoishi duniani ni ima wasioamini uwepo wa Mungu au wapo katika dini ya wanaoabudu Masanamu. Na utafiti uliofanyika katika kituo cha Pew cha Utafiti huko Marekani unakisia kuwa idadi ya Waislamu itakuwa kubwa zaidi ukilinganisha na dini nyengine kwa kipindi cha miaka ijayo ambao watakaribia Bilioni 2.8 ya idadi ya watu wote duniani ifikapo mwaka 2050 AD.

2. Kwa maelezo zaidi unaweza kutembelea tovuti ( website) www.Guidetoislam.com



(Bismillahi Rrahmaani Rrahiim) na (Laa Ilaaha illa-llaah) kwa khati za Kuufi ni katika kazi za mchoraji wa Misri Iswam Abdul-Fattah

SURA

# 5

# MAADILI NA USTAARABU





120

## KWANZA: MAENDELEO YA UTU NA UKUAJI WA DHATI YA MTU

Allah Mtukufu amemuumba mwanaadamu akiwa na mwili, akili, na roho na kwa kila kimoja akamjalia mahitaji yake. Na kunahitajika kuwepo usawa baina ya mahitaji ya mwili kama chakula, kinywaji, starehe na mapumziko, na mahitaji ya roho kama utulivu, amani na nafsi iliyosawa, na mahitaji ya akili kama kujifunza, kufikiria na kuiva kifikra kuliko sahihi ambako kunapelekea matokeo chanya yaliyonyoka.



Dini ya Kiislamu hairuhusu Utawa ambao unataka kuzuia mwili kwenye baadhi ya mahitaji yake ya kimaumbile. Imepokewa kutoka kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Itakapokimiwa Sala na kumeletwa chakula cha usiku wakati huo basi anzeni na chakula" Amepokea Bukhari na Muslim. Hayo (yamesemwa) Ili mtu asije akashughulishwa na njaa yake huku anasali. Kama alivyoamrisha Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) watu wasali Sala za usiku au Sala za Sunna kiasi wanachoweza na pindi wakichoka basi wapumzike.

"T'aha! Hatukukuteremshia Qur-ani ili upate mashaka" Suratu Taha aya ya 1-2.

"...Allah anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito..." Suratul- Baqarah aya ya 185.

## Jihadhari na kuchupa mipaka, hakuna kuchupa mipaka katika Uislam




ni kuchupa mipaka ya mambo yaliyo sawa ikiwa ni katika mambo ya dunia au katika mambo ya dini. Kwa hakika ameuwekea Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) misingi ya kifikra na kimwenendo ili kupiga vita uchupaji mipaka.

Kwa hakika imechukiwa katika dini uchupaji wa mipaka na kutia uzito mambo kama ilivyochukiwa kuzama katika starehe mpaka katika vyakula na mavazi na mengineo katika mambo ya kidunia.

"Na vivyo hivyo tumekufanyeni umati bora (kama kibla chenu tulivyokifanya bora) ili muwe mashahidi juu ya watu..." Suratul-Baqarah aya ya 143.

Mara moja walikuja watu watatu wanaulizia kuhusu ibada ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akiwa nyumbani kwake, walipoelezwa waliona ni Ibada kidogo wakadhani kwa kuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake)ameshasamehewa dhambi zake ndio anafanya ibada kidogo, na kwamba ni lazima wao wazidishe kupita kiasi katika ibada zao ili kupata radhi za Allah Mtukufu hata ikibidi kuwacha mahitaji yao ya kimwili. Akasema mmoja wao yeye ataswali usiku kucha (hatopumzika au kulala), akasema wa pili yeye atafunga kila siku ya mwaka na hatofungua milele, na akasema wa tatu yeye atajitenga na wanawake na hatooa milele. Angalia hadithi katika Sahihi ya Bukhari (4776).

Basi alipokuja Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na akajuwa waliyosema, akasema kuwambia" "Nyinyi ndio mliosema hivi! Wallahi mimi ndie ninayemuogopa Allah Mtukufu na MchaMungu zaidi kuliko nyinyi, lakini mimi nafunga na nafungua (siku nafunga na siku sifungi), nasali na kupumzika, na naoa wanawake basi mwenye kujiepusha (kuchukia) mwendo wangu si katika mimi" Amepokea Bukhari (1184) na Muslim (849).

### Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anachukia kuweka uzito katika Dini

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anapenda kufanya wepesi katika mambo yake, hajapewapo mambo mawili achaguwe isipokuwa huchaguwa lilokuwa jepesi katika mawili hayo ikiwa hakuna dhambi. Na hakuwa mwenye kushikilia maoni au jambo isipokuwa ikiwa hakki miongoni mwa hakki za Allah kama alivyowafundisha watu kwamba dini sio Itikadi na Ibada tu bali pia ni mfumo mzima wa maisha na muamala uliosahihi kwa mtu binafsi na watu na visivyo na uhai, wanyama na mimea.

Kutoka kwa Abdillah bin Masoud (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Wameangamia wenye kushadidia mambo na kuchupa mipaka) amesema mara tatu" Amepokea Muslim (2670).



"Mutanatwiuun" ni wenye kuvuka mipaka na wenye kupita kiasi au wenye kuzua na kuzidisha katika dini.

### usafi ni sehemu ya tohara

Uislamu umetilia mkazo usafi kwa kiasi kikubwa mpaka ukawa usafi ni alama katika alama za jamii ya Muislamu. Usafi ni katika Imani na wala haikamiliki Imani isipokuwa ujisafishe mwili na roho.

Allah Mtukufu amesema: "...Hakika Allah huwapenda wanaotubu na huwapenda wanaojitakasa" Suratul-Baqarah aya ya 222.

"Na nguo zako uzisafishe" Suratul-Muddathir aya ya 4.

### udhu na kukoga katika uislamu

Waislamu wanatofautiana na wasiokuwa Waislamu kwa kutia Udhu katika kila Sala na haisihi ibada ya Sala pasi na Udhu. Udhu unajumuisha kukosha uso na mikono miwili mpaka visigudi viwili na kupangusa (sehemu ya) kichwa na kuosha miguu miwili mpaka vifundoni.



Na katika Udhu kuna Sunna nyingi tunataja baadhi: mwanzo kusukutua na kupandisha maji puani kwa mkono wa kulia na kuyatoa (kupenga) kwa mkono wa kushoto, na kupembua baina ya vidole vya mikono na miguu, na kupangusa masikio mawili na kutumia msuaki kusafisha kinywa.

Ama kukoga nako ni kukosha mwili mzima, nako kupo namna mbili katika Uislamu, kuoga kuliko lazima na kuoga kuliko Sunna. Kukoga kuliko lazima ni sharti ya kujisafisha na wala haisihi Sala pasi na kufanya hivyo baada ya Hedhi na Nifasi na maingiliano ya kindoa na Janaba (kutokwa na maji ya uzazi). Kama ilivyokuwa haifai kumzika maiti isipokuwa baada ya kumuosha isipokuwa wale ambao wamekufa wakiwa mashahidi.

Ama kukoga kulikokuwa ni Sunna yaani amehimiza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ni kukoga siku ya Ijumaa kabla ya kwenda kusali na kwa siku kuu, na kukoga kabla ya kuhirimia ibada ya Hija au Umra na kufanya usafi wa mwili kiujumla.

Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): “Inapaswa kila Muislamu akoge katika kila wiki siku moja, akoshe kichwa chake na mwili wake” Amepokea

Bukhari (1184) na Muslim (849).

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amewahimiza Masahaba zake kudumu na Usafi na amewalingania usafi katika nyumba zao, viwanja vya nyumba zao na akawafundisha kuondoa taka njiani ni katika sadaka, na miongoni mwa mafunzo yake ya kuhifadhi usafi kwa kiwango cha juu cha usafi binafsi ni kama:



- Kuvaa mavazi safi na yenye kupendeza bila ya kufanya israfu na kupindukia.
- Kutumia manukato na mafuta mazuri hasa kabla ya kuelekea Msikitini na kukutana na watu.
- Kupunguza kucha na kuondosha nywele zilizozidi na nywele za kwapa.
- Kukosha mikono miwili kabla ya kula chakula na baada ya kula na kabla ya kugusa chakula unapo amka.
- Kusafisha meno kila siku na wakati wa Sala.

**Kupiga Msuwaki...Ni usafi wa mdomo na kuhifadhi harufu nzuri:**



Hakika Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kutumia Msuwaki au kupiga Msuwaki kwa ajili ya kusafisha meno kunabeba maana za kiadabu na kiafya na tiba
Na tiba ya sasa imegundua hilo baada ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kusema:



"Kupiga Msuwaki kunasafisha mdomo na kumridhisha Allah Mtukufu" Amepokea An-Nasaai (1/3)

Na amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake)

"Lau kama sio kuwatia uzito umma wangu ningewaamrisha kupiga Msuwaki kila (wanapotaka) kusali" Amepokea Bukhari (7241).

Baadhi wanaitakidi kuwa kusafisha meno kwa Msuwaki (wa kijiti) ni jambo la zamani kabla ya kuja kwa dawa za meno. Lakini sayansi imethibitisha athari ya Msuwaki katika kulinda meno yasioze na kuharibika, basi Msuwaki ni usafi wa kimaumbile kwa mdomo, kuifanya harufu ya mdomo kuwa nzuri na safi.
Na Utafiti wa kitaalamu umethibitisha kuwa Msuwaki una madini mazuri kwa utendaji kazi kuyalinda meno na ufizi kwa muda mrefu kutokana na madhara ya Bakteria.

Nao (Msuwaki wa kijiti) umejaa madini yanayosafisha na yenye kuzuwia utokaji wa damu utokaji uzima na kuua vijidudu na kuipa uwezo kukinga tabaka la Enamel na kuondoa kwa chokaa (calcium) na kubadilika kwa meno. Msuwaki umekusanya zaidi ya madini 25 ya asili yaliyo muhimu kwa usalama wa meno. Na kijiti cha Msuwaki kimetokana na mti aina ya (Selvodor Parsik) nao ni maarufu katika Bara Arabu, Afrika, India, na Marekani ya Kusini.

## Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) anawahamasisha watu kutafuta elimu




Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amekuja na ujumbe wa mbinguni wa milele, umeanza na neno "Soma" ili uwatowe watu katika giza la ujinga na kuwapeleka katika nuru ya utambuzi, na kuwatoa katika upotevu na kuwapeleka katika uwongofu.

Na katika kipindi cha miaka michache Uislamu ukawa umepiga hatua kubwa ya Utamaduni katika dunia, ukazidi katika muda huo kila aina ya maarifa, na ulimwengu ukashuhudia maendeleo ya kielimu na maendeleo yaliyorefuka athari zake mamia ya miaka.

Hakika yule ambae anaisoma Qur-ani Tukufu atagundua kujikariri maana za usisitizo wa kusoma na ugunduzi na mazingatio na kutafakari na kufahamu na kukumbuka.

Mambo hayo ndio misingi ya utafiti na kujifunza na kufahamu na kujua vitu vilivyopo na kujua sababu na kufikia katika uhakika wa mambo.

Na hakika Allah Mtukufu amempambanua binaadamu kwa neema ya akili na viumbe vyengine, na akamjaalia kuzingatia na kutafakari uumbaji wa Allah Mtukufu, na dalili za ulimwengu ni sababu ya imani kwa binaadamu ya kuwepo muumbaji wake na upweke wake.

"Katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja (za kuonesha kuwepo Allah mmoja), kwa wenye akili (190) Ambao humkumbuka Allah wakiwa wima - na wakikaa na - wakilala. Na hufikiri umbo la mbingu na ardhi (pia. 'Namna gani Allah alivyoumba'. Wakasema:) "Mola wetu! Hukuviumba hivi bure. Utukufu ni wako. Basi tuepushe na adhabu ya Moto (191) Suratu-Aal-Imraan aya ya 190-191

Na katika ardhi zimo (alama namna kwa namna za kuonesha kuwepo Allah) kwa wenye yakini (20) Na katika nafsi zenu (pia zimo alama hizo). ]e! Hamuoni? (21) Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyoahidiwa (22) Basi naapa kwa Mola wa mbingu na ardhi, kuwa hakika haya ni haki, kama ilivyo (haki) ya kwamba nyinyi mnasema" (23) Suratu-Dhhariyati aya 20 – 23.

Na hakika Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amewashajiisha watu kutafuta elimu na akawakataza kuficha elimu yenye manufaa.

Na akawahimiza Masahaba zake kujifunza na kufundisha watu aina tofauti za elimu zenye manufaa, na kuisambaza na kufaidika nayo. Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake):

**Mwenye kufuata njia kwa ajili ya kutafuta elimu, Allah Mtukufu atamrahisishia mtu huyo njia ya kuelekea peponi"**

Amepokea Muslim "Jaami'i Sahihi" (8\71) namba (2699) kutoka kwa Abuu Huraira (radhi za Allah ziwe juu yake).

Na kwa ubora wa mahimizo haya ikawa lugha ya Kiarabu (lugha ya Qur-an tukufu) ni lugha ya Utabibu na Fizikia na Kemia, na Hesabu na kila aina ya elimu ambazo zimekua zinasomeshwa katika vyuo vikuu katika ulimwengu kwa karne nyingi. Na wakawa wengi katika wanavyuoni wa Kiislamu ni katika wanavyuoni maarufu ulimwenguni kwa kile walichokiongeza katika uvumbuzi wa kielimu ulioleta ukuaji wa Ustaarabu wa aina yake, na lau kama si hivyo ustaarabu wa Wamagharibi ungechelewa kwa mamia ya miaka.

Jadweli (2): Michango ya wasomi katika kukuza Ustaarabu wa Kiislamu

| Msomi | maelezo kwa ufupi |
|---|---|
| **Jabir bin Hayyan**<br><br>(Baba wa Kemia)<br><br>**721 – 815AD** | Jaabir bin Hayyan bin Abdullah Al-Azdi yeye ndiye muanzilishi wa elimu ya Kemia ya kivitendo yeye ndiye wa mwanzo aliyefanya majaribio ya Kemia akaweka vipengele vya Kemia kupitia uzoefu, uchunguzi na uvumbuzi wake wa kielimu,<br>Alikuwa ni mwingi wa kubuni na kuvumbua, hukutana kemia na jina lake akaitwa jina la "mzee wa wana kemia" na "Baba wa kemia" ameikuza Kemia na akaifanya mpaka kufikia kuwa elimu kubwa na akaanzisha misingi ya kutafuta nyenzo za Kemia na kuamiliana nazo Alivumbua Al-Kali na chumvi ya Amonia na akawa bingwa katika mbinu za kusafisha chuma na maandalizi yake na kupaka rangi vitambaa. |
| **Muhammad bin Mussa Al-**Khawaarizmi<br><br>(Baba wa kanuni za hesabu ya kipeo uzio) (logarithm)<br><br>**780-850AD** | Muhammad bin Mussa Al-Khawaarizmi ni miongoni mwa wanavyuoni wa kwanza wa Kiislamu wa Hisabati, yeye ndie muanzilishi wa kanuni za Logarithm na minyambuliko ya Hesabati, juhudi zake zimechangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza elimu ya hesabu katika zama zake, Khalifa Maamun alimkabidhi kuchora ramani ya dunia ambayo zaidi ya WanaJografia sabiini walifanya kazi hiyo. Al- Khawaarizmi amewacha idadi kubwa ya vitabu katika fani ya Falak na Jografia, miongoni mwa vitabu vyake muhimu ni (Kitabu Aljabru Wal-Muqaabalah) kitabu ambacho kimetarjumiwa kwa lugha ya kilatini katika mwaka wa 1135 AD na kuingizwa maneno mfano Aljebra na neno Zero katika lugha ya Kilatini |



bin Siina

LATIN FIGURES:

I, II, III, IV, V, VI, VII, VIII, IX, X

ARABIC NUMBERS :

1, 2, 3, 4, 5, 6, 7, 8, 9, 10

| | |
|---|---|
| **Abubakar Muhammad bin Zakariya Ar-Raazi** (baba wa tiba) **865 – 929AD** | Abubakar Muhammad bin Zakariya Ar-Raazi mmoja kati ya wanavyuoni wa Kiislamu walio mahiri katika upande wa Tiba na Kemia na kuwa na upeo mkubwa wa maarifa na kuwa hodari katika elimu za Hisabati na Musiki akaweza kuoanisha aina za elimu. Na Arrazi amechangia katika mambo mingi aliyovumbua katika nyanja ya Tiba na Kemia, yeye ndiye wa mwanzo aliyetofautisha baina ya maradhi ya Ndui na Surua na kutoa sifa ya kila kimoja kati ya maradhi mawili hayo.<br>Raazi ndiye wa mwanzo aliyetumia Kemia katika Tiba akafanya kazi ya kuandaa idadi kubwa ya mchanganyiko wa Kemia ambao hutumika katika elimu ya Famasia, naye ndiye wa mwanzo aliyetayarisha mada ya “Alcohol” inayotokana na chachu za suluhisho la Sukari, na Sulphuric Acid kutokana na matone ya Iron Sulfate, ametunga kitabu kiitwacho Al-Haawi fi Atwibi ambacho kimekua ndio marejeo ya mwanzo katika elimu ya Tiba ndani ya Bara la Ulaya kwa muda wa miaka 400 |
| **Al-Hussein bin Siina** (Baba wa Tiba za Kileo) **980-1037 AD** | Al-Hussein bin Abdallah bin Siina ametambulikana kwa jina “Shekhe mkuu” na wanamuita WaMagharibi "Kiongozi wa Madaktari" na "Baba wa Tiba za Kisasa", ametunga takriban vitabu 200 vya Tiba na elimu za kitabia na Hisabati na Falsafa pamoja na Muziki na maudhui nyenginezo. Na katika kazi zake maarufu Muziki kitabu kinachoitwa “A-Shifaa” ambacho ni kitabu kilichokusanya mambo mengi yanayozungumzia elimu ya Sayansi ya Asili, na kitabu “Kanun katika Tiba” ambacho kimetafsiriwa kwa lugha tofauti na kilikua kinasomeshwa kitabu hicho katika Vyuo Vikuu vingi vya Ulaya mpaka kufikia mwishoni mwa karne ya 19. |
| **Abul-Izz bin Ismail Al-Jazarii** (Baba aa Kemia) **1136- 1206AD** | Abul-Izz bin Ismail Al-Jazari, anaefahamika kwa jina la “Al-Jazary”. Ni mmoja wa wahandisi na wana Kemia katika historia, amepata hadhi ya kuenziwa na watawala wa eneo la Bakri liliopo kusini mwa Uturuki ya leo, amefanya kazi ya kuwatumikia watawala hao kwa muda wa miaka 25 akawa ni mkubwa wa wahandisi wa mekaniki wa Watawala, na akaisherehesha mifumo hiyo katika kitabu chake alichokiita “Arraai’ul- Jaami’u baynal-Ilmi Wal-‘Amalun-Naafi’i fiy Swina’atul-Hiyal” chenye michoro ndani yake ya upambanuzi. |

## Akili nzuri ipo katika mwili wenye afya

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anajilinda kwa Allah Mtukufu kutokana na kushindwa mambo, na uvivu, na dhiki, na huzuni, na alikua anapenda uchangamfu na akiwahimiza Masahaba zake kuwafundisha watoto wao michezo tofauti kama kukimbia mbio na kupanda farasi na kuogelea na mengineyo, na alikua Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akishindana na mkewe Bibi Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake), mara nyengine Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anashinda na mara nyengine Bibi Aisha anashinda yeye.

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alianzisha uwanja wa kushindana mbio upande wa magharibi ya Msikiti wake, bado sehemu hio ni maarufu mpaka leo, na pamejengwa pembezoni mwa uwanja msikiti mdogo (baadae ukaitwa msikiti wa mashindano)

Na amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) "Muumini mwenye nguvu ni bora na anapendeza zaidi kwa Allah Mtukufu kuliko muumini dhaifu, na kwa kila mmoja kuna kheri, fanya pupa kwa yale yanayokunufaisha na mtake msaada Allah wala usishindwe" Amepokea Muslim (4822).



Na michezo ya pamoja inakuza moyo wa kusaidiana na ushindani mzuri na inahifadhi afya ya kiwiliwili, kwa hiyo ni chakula cha mwili na akili kwa pamoja, na mazoezi katika Uislamu yana vithibiti vilivyojengwa kwa misingi ya Maadili na Kitamaduni ikiwemo kuvaa mavazi ya heshima na kutoshughulishwa na mazoezi mpaka ukaacha Sala na haki za Allah mtukufu na kutojishughulisha na kujiingiza katika rehani zinazo fanana na kamari na kutosababisha uhai wa mwanaadamu au mnyama kuwa hatarini.

# PILI: MIKO YA KIJAMII NA KIMAADILI

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anawahimiza Waumini kupendana baina yao



Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) "Hatokua na imani ya kweli mmoja wenu mpaka ampendelee ndugu yake yale anayoyapenda katika nafsi yake",

na pia akasema: "Naapa na yule ambae nafsi yangu iko mwake, hamtoingia Peponi mpaka muamini, na hamtoamini mpaka mpendane, je! nikujulisheni jambo ambalo mkilifanya mtapendana? Toleaneni salamu baina yenu" Amepokea Muslim (54).

Na akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) - katika mambo ambayo yanayohusiana na kusaidiana na kusameheana baina ya watu na kueneza mapenzi baina yao - : "Mwenye kumfanyia wepesi mwenye uzito, basi Allah Mtukufu atamfanyia wepesi duniani na Akhera". Na akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Na Allah Mtukufu yupo katika kumsaidia mja madamu mja huyo anamsaidia ndugu yake" Amepokea Muslim (2699)

Amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake)

"Kutabasamu kwako katika uso wa ndugu yako (Muislamu) ni Sadaka".

Amepokea Bukhari katika "Al- Adabul-Mufrad" (891) kutoka kwa Abu Dharr (radhi za Allah ziwe juu yake).

## Maamkizi ni ujumbe wa Amani

Mtu mmoja alimuuliza Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): "Ni upi Uislamu bora? Akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Ni kulisha chakula na kutoa salamu kwa unaemjua na unayemjuwa" Amepokea Bukhari (12) na Muslim (29).

Na katika riwaya nyengine amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Usidharau katika mambo mema chochote japo kukutana na ndugu yako kwa uso wa bashasha" Amepokea Muslim (2626).

Na pia amesema: "Enyi watu, toleaneni salamu, na lisheni chakula na ungeni ukoo, na salini usiku wakiwa watu wamelala, mtaingia Peponi kwa amani" Amepokea Tirmidhiy (2485).

**Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anaanza yeye kuwatolea salamu watu na anakutana nao kwa mapenzi na makaribisho.**



Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anaanza kutowa Salamu na maamkizi kwa anayekutana nae.

Na anapopeana mkono na mtu hauwachi mkono wake kabla mwenyewe hajauwacha na alikuwa anakutana na watu kwa uso wa bashasha, anaburudika anayemtazama.



**Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anawafanyia mzaha Masahaba wake na hucheza na watoto wake.**

Ilikua kicheko chake mara nyingi ni kutabasamu, alikuwa hacheki sana na kutoa sauti, na alikuwa ni mwenye utu wenye kupendeza na mwenye utulivu wenye hadhi ya heshima baina ya watu. Na alikuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akiwafanyia mzaha Masahaba wake na akicheza na watoto wake na wajukuu wake Hassan na Hussein lakini hasemi isipokua ukweli wala hazungumzi bila ya haja, na imepokewa ya kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ameonekana mara nyingi akishindana mbio na mkewe katika zama ambazo mashindano ya farasi ilikuwa ni jambo lililo enea.

**Mizaha yake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwa mwanamke kikongwe**



Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) hali ya kumfanyia mzaha mtu mzima ya kwamba hatoingia Peponi mkongwe, akasema (Bibi mtu mzima): wana nini wao hali ya kuwa wanasoma Qurani? Akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): Je hujasoma? "Hakika sisi tutawarudisha wanawake katika umbo la

mwanzo na tutawafanya Mabikira" yaani hakika ya mwanamke ataingia peponi akiwa ni kijana mdogo.

Na akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) mara moja kumwambia mwanamke aliyekuja kumtafuta mumewe: "Mumeo ni yule mwenye weupe katika jicho lake? akaogopa. asijekuwa mumewe kapatwa na kitu katika jicho lake, (yule bibi) akamuuliza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema: "Amejeruhiwa? Na lini umemuona? Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamwambia: "Hakuna jicho lolote isipokua ndani yake kuna weupe" Twabrany katika Al-Awsat' 5/258 namba(5545).

## Mizaha yake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwa Masahaba zake

Amesimulia Sahaba Suhaibu-Rrumi (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba yeye alikwenda kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akiwa anakula tende na katika jicho lake kuna maumivu, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamwambia kumfanyia mzaha: "Je Unakula tende na katika jicho lako kuna maumivu?" akasema Suhaib (radhinza Allah ziwe juu yake): "Hakika nakula katika upande ambao jicho lipo zima" akacheka Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kutokana na aliyoyasema Suhaib".

Amepokea Al-Hakim katika "Mustadrak" (4/411) namba (8357) na Ibnu Maajah katika "Sunan" (4\500) kwa namba (3443) na Ahmad kwenye "Musnad" (7/3636) namba (16859), (10/5503) namba (23651).

Amepokea Anas bin Malik, yakwamba mtu mmoja (katika riwaya ni mwanamke) alikuja kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) pamoja na watu wake akasema: "Ewe mjumbe wa Allah tupakie kwenye ngamia, akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Jee! Niwachukuwe kwenye mtoto wa ngamia? Akasema yule mtu: "Atatusaidia nini mtoto wa ngamia? Akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Je! Ngamia si hazai isipokua ngamia? Amepokea Tirmidhiy na Abuu Daud.

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anawapenda watoto na anawalea

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anawasimamia watoto kwa usimamizi maalumu, anazungumza nao na anawatolea salamu na anacheza nao, imesimuliwa kuna mtoto anayejulikana kwa jina "Abu Umair" alikuwa na ndege mdogo anacheza nae, akafa ndege wake akahuzunika, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema: "Ana kitu gani mtoto? Wakasema: amekufa ndege wake, akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kumwambia mtoto kwa upole ili amuondoshee huzuni zake: "Ewe Abaa Umair ndege kafanya nini? Amepokea Bukhari

katika "Sahih" (8/30) namba (6129), (8/45) namba (6202), na Muslim katika "Sahihi" (6/176) namba (2150) kupitia hadithi ya Suhaib (radhi za Allah ziwe juu yake)

Na alikuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anahimiza wazazi kudhihirisha mapenzi na huruma na uadilifu kati ya watoto wao, na alikuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anawabusu watoto wake na wajukuu zake, na mara moja bwana Aqra'a At-Tamimy alimuona Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akimbusu Hussein bin Aly bin Abi Talib, akasema bwana Aqra'a kumwambia Mtume: "Hakika mimi nina watoto kumi sijawahi kumbusu hata mmoja kati yao, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamuangalia kisha akasema: "Asiye kuwa na huruma hahurumiwi" Amepokea Bukhari.

Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Wenye huruma basi Allah mtukufu mwingi wa rehema atawahurumia, wahurumieni walio ardhini, atakuhurumieni aliyekuwepo mbinguni"

Amepokea Tirmidhy (1924) na Abu Daud (4941).





Na Anas bin Malik (radhi za Allah ziwe juu yake) ameeleza kuna kijana wa Kiyahudi alikuwa akimuhudumia Mtume (rehema na amani ziwe juu yake), aliumwa, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akaenda kumtazama nyumbani kwake" Amepokea Bukhari katika "Sahihi" (2/94) namba (1356) kupitia hadithi ya Anas (radhi za Allah ziwe juu yake)

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anausia wema kwa Jirani

**Kuwa Mpole Kwa Jirani yako**

Amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Mwenye kumuamini Allah Mtukufu na siku ya mwisho basi asimuudhi jirani yake, na katika mapokezi mengine "basi amfanyie wema jirani yake," na akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika mnasaba mwengine:

**"Hakuacha Jibril (amani iwe juu yake) kuniusia kumfanyia wema jirani mpaka nikadhani atamrithisha",** Amepokea Bukhari kwenye "Sahihi" (8/10) namba (6015), na Muslim kwenye "Sahihi" (8/37) namba (2625).

Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema kumwambia Abuu Dhar Al-Ghafary: "Ewe Abu Dhar utakapopika mchuzi zidisha maji na umgawiye jirani yako", na katika mapokezi mengine "basi angalia watu wa nyumba ya karibu katika majirani zako uwachotee kwa wema" Amepokea Muslim katika "Sahihi" (8/37) namba (2625) kupitia hadithi ya Abu Dhar (radhi za Allah ziwe juu yake).

Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Wallahi hajaamini! Wallahi hajaamini! Wallahi hajaamini, akaulizwa ni nani ewe Mjumbe wa Allah? Akasema: "Ambaye jirani yake hana amani kwa kero zake" yaani shari zake na maudhi yake. Amepokea Bukhari (6016) na Muslim (46).

**Hakuna Masihara wala Dharau:** Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amekataza kuwafanyia masihara na kuwadharau watu au kuwafanyia ubaya kwa namna yoyote ya ubaya sawasawa ikiwa kwa mkono au ulimi, na alimuuliza Abuu Mussa Al-Ash'ary Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ni wepi Waislamu bora? Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema: "Ni yule ambae watasalimika Waislamu kutokana na ulimi wake na mkono wake" Amepokea Bukhari na Muslim.



"Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msitukanane kwa kabila, wala msiitane kwa majina mabaya (ya kejeli): Jina baya kabisa kuambiwa mtu ni asi baada ya kuwa ni Muisilamu. (Na kufanya baya ni uasi) Na wasiotubu, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao)" Suratul –Hujrat aya ya 11.

## Hakuna kudhaniana mabaya, kutiliana shaka, kuchunguzana wala kusengenyana

"Enyi mlioamini! Jiepusheni sana na (kuwadhania watu) dhana (mbaya) kwani (kuwadhania watu) dhana (mbaya) ni dhambi. Wala msipeleleze (habari za watu). Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine. Je! Mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La, Hampendi; (Basi na haya msiyapende). Na Mcheni Allah. Bila shaka Allah ni Mwenye kupokea toba (na) Mwingi wa kurehemu" Suratul-Hujrat aya ya 12.

## Usieneze habari mbaya

"Enyi mlioamini! Kama fasiki, (asiyekuwa wa kutegemewa) akikujieni na habari (yoyote ile msimkubalie tu) bali pelelezeni (kwanza), msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda"

Suratul-Hujrat aya ya 6.



## Adabu za kuamiliana na mambo mazuri (Ladha) katika Uislamu




Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alitilia mkazo adabu za mwenendo mzuri na muamala mzuri na akawafundisha Masahaba zake kwamba tabia nzuri na adabu za kuamiliana na watu ni katika sunna zake tukufu, na Qur-ani tukufu imehimiza katika aya zake nyingi kuamiliana vizuri na watu na kuwa na tabia nzuri, na ikataja adabu nyingi za kuamiliana na watu na mwenendo mzuri kama kushusha sauti na kubisha hodi na kwenda kwa unyenyekevu na mengineyo. Na mafundisho ya Kiislamu yamejitosheleza kwa adabu za kuamiliana na watu wengine na hizi ni baadhi katika adabu za Kiislamu:

- Weka mkono wako kwenye mdomo utakapokwenda miayo na waombee rehema wengine wanapopiga chafya.

- Usinyanyue sauti yako kwenye mazungumzo wala usitumie maneno mabaya na usiwe na matendo machafu wala usiwe mwenye kulani wala usitembee katika ardhi kwa kujigamba kama mwenye kiburi.

- Atakapoumwa ndugu yako nenda kamtembelee na kumjuulia hali, na ukifika kwake usikae sana ukampa uzito na umpe nafasi ya kupumzika.

- Usije Msikitini utakapokula kitunguu maji na kitunguu saumu kwani harufu zake inawakera wengine wenye kusali kama vile ambavyo Malaika wanakereka kama wanavyokereka binaadamu, na ukienda Msikitini vaa nguo safi na jitie manukato na wala usiwavuke mabega waliokaa, na wasaidie ndugu zako kwa kuwatengea nafasi hasa ikiwa sehemu imejaa watu.

Zungumza na mwenzako kwa anayoyapenda kwani maneno mazuri ni sadaka, na waite wengine kwa majina wanayo yapenda, na utakapo kutana na ndugu zako harakia kuwatolea salamu na kutabasamu kwani kutabasamu katika nyuso za wenzako ni sadaka, na utakapokua pamoja na watu na ukataka kumnon'goneza mtu mmoja (yaani kuzungumza nae kwa siri) haijuzu kufanya hivyo mtakapokuwa watu watatu ili mtu wa tatu asisimame peke yake na akawa ametengeka na mazungumzo na kama hakuna budi basi subiria mpaka aje mtu wa nne au zaidi ili uweze kujitenga na rafiki yako kwa mazungumzo.

◈ Kuwa na unyenyekevu na huruma kwa wazazi wako, wala usinyanyuwe sauti yako mbele yao, wala usiwambie (aah!) ama watoto wadogo na wakubwa ni juu yao waombe ruhusa kabla ya kuingia chumbani kwa wazazi wao katika nyakati tatu kwa siku "Kabla ya Sala ya Asubuhi, na wakati wa mchana na baada ya Sala ya Isha."

◈ Ikiwa unawapatia watu maji basi adabu nzuri uwe wewe wa mwisho kunywa na utakapokunywa kunywa mafunda matatu, wala usipumue katika chombo.

◈ Utakapoalikwa chakula basi unapaswa kuitikia wito na utakapokula taja jina la Allah Mtukufu unapoanza kula, na ule sehemu ya karibu yako wala usiwape tabu wengine.

**Adabu za kuamiliana na Mwanamke**

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ameusia adabu za kuamiliana na Wanawake, na akawaeleza kwamba Wanawake kama chupa za Kigae (yaani wao ni wepesi kama kioo) na akawaamrisha wanaume kuinamisha macho, na akakataza kuwatizama Wanawake. Mara moja alionekana Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) anapinda goti lake ili mkewe Bibi Safia (radhi za Allah ziwe juu yake) apande juu yake (kwenye goti la Mtume) ili apande ngamia.

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anaweka misingi ya Ustaarabu katika kuamiliana na wengine:

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliishi pamoja na Masahaba zake miaka ishirini na tatu baada ya kupewa Utume akakuza ndani ya kipindi hicho maadili na tabia njema na akaweka misingi ya Ustaarabu ya kuamiliana na wengine (Waislamu na wasiokuwa Waislamu) kwa vitendo huku watu wanayashuhudia na kuvutika nayo.

Je wewe ni mwepesi wa Muamala na wengine? Amesema Anas bin Malik (radhi za Allah ziwe juu yake):

Nilimhudumia Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) miaka kumi hajawahi kuniambia aah! hata mara moja, wala hajawahi kuniambia kwa kitu nilichokifanya "kwanini ukafanya?" wala kwa kitu nilichokiwacha "kwanini ukawacha?" na alikuwa Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) ni mzuri wa watu kwa tabia njema...mpaka mwisho wa hadithi" Amepokea Tirmidhy (3351).

## Ukweli na Hekima katika kuamiliana na watu

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anao mtazamo wa kweli na hekima kubwa zilizomfanya awe kiongozi wa kipekee anaependwa na watu na kuridhika na hukumu zake. Na imepokewa kuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) aliwaamrisha Waislamu katika vita vya Banii Quraydha kwa kusema "Asisali mmoja wenu Sala ya laasiri isipokua Bani Quraydha (sehemu hiyo)" Amepokea Bukhari katika 'Jaami'i Sahihi" (2/15) namba (946), (5/112) namba (4119) na Muslim katika "Jaami'i Sahih" (5/162) namba (1770) kupitia hadithi ya Ibnu Omar (radhi za Allah ziwe juu yake). Basi miongoni mwao walifika kabla ya Magharibi huko Bani Quraydha wakasali laasiri (walipofika), na wengine walichelewa wakasali (Sala ya laasiri) njiani wakiogopa kuipoteza Sala (ya laasiri) na kuingia wakati wa Magharibi, na kwa hakika aliondosha Mtume wa Allah mjadala katika jambo hili na akakubali kitendo cha makundi yote mawili bila ya kubagua rai ya wowote kati yao.

Na katika Vita vya Dhata-Salaasil kulikuwa na hali ya hewa baridi sana, kiongozi Amr bin Al-'Aas alisemwa kwa kukosolewa na Masahaba wakubwa kwa sababu aliamka na Janaba basi hakukoga wala hakutia udhu, bali alijitosheleza kwa kutayammamu na akasalisha watu Alfajiri akiwa Imam kwa sababu alikuwa kiongozi wao na hakumtanguliza yoyote katika Masahaba wakubwa awaongoze Waislamu. Wakati aliporejea Madina Masahaba walimlalamikia Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) nae Mtume akamtaka atowe ufafanuzi na akasikiliza yale aliyo yatanguliza Amru bin Al-Aas katika udhuru wa kwamba usiku (ule) kulikuwa wa baridi.

Na yeye akaogopea kuumwa na kushindwa kuwaongoza Waislamu kwenye vita kwa kutoa ushahidi wa kauli yake Allah Mtukufu “Wala msiziuwe nafsi zenu hakika Allah kwenu nyinyi ni mwingi wa huruma”, akacheka Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kwa kauli yake (hiyo) na jitihada yake wala hakumlaumu wala kumkosoa kwa alichofanya” Amepokea Al-Hakimu “Mustadrak” (1/177) namba (634) na Abu Daud kwenye “Sunan” (1/132) namba (334) na Ahmad kwenye “Musnad” (7\/4007) kwa namba (18091) kupitia hadithi ya Amr bin Al-Aas (radhi za Allah ziwe juu yake.

**Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) anahimiza mashauriano na kutekeleza kwa vitendo pamoja na Masahaba wake.**




Pamoja na kwamba Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anapokea wahyi kutoka mbinguni lakini alikuwa akiwashauri Masahaba zake mpaka Wake zake katika mambo mengi ya kidunia Na alikuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akiwausia Masahaba zake kufuata njia ya haki na kutokuwa na ushabiki (katika misimamo yao), na alikuwa akiimarisha misimamo yao ili wafanye maamuzi yanayofaa.

Na mfano wa hayo ni wakati walipopanga viongozi wa Makka na Makabila mengine ya Waarabu kuivamia Madina, Salman Al-Farisy alitoa rai ya kuchimbwa handaki kwenye upande wa kaskazini ya Madina baina ya mitaa miwili ya mawe iliyozunguka Madina, pamoja na kwamba fikra hii ilikuwa ni ngeni na haijawahi kutekelezwa katika Bara Arabu, lakini Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) aliikubali kwa dhati na kujadiliana na Masahaba zake nao wakaiona ni rai nzuri, wakachimba handaki urefu wake kilomita 5.5 na mapana yake mita 4.6, ikawa ndio sababu kuu katika sababu za kuzuwia hatari ya maadui.

Na katika vita vya Badri Waislamu walipiga kambi katika sehemu ambayo mmoja kati ya majeshi wa Kiislamu aliona sio sehemu sahihi, akaja kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) nae akiwa ni kiongozi wa jeshi akamuuliza ikiwa kuichagua sehemu hio ni jitihada yake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) au ni Wahyi kutoka kwa Allah Mtukufu? Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akajibu kwa unyenyekevu kwamba kuchagua sehemu hio ni jitihada yake binafsi, basi yule mwanajeshi akatoa maoni ya kuondoka sehemu hio na kuweka kambi sehemu nzuri zaidi na akamtolea na sababu zake, na baada ya mashauriano mengi Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) pamoja na Waislamu wengi wakaukubali ushauri huo kisha wakahamia kuelekea sehemu nyengine iliyokuwa bora kivita.

### Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) anatilia mkazo kuamiliana vizuri na wafuasi wa dini nyenginezo

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anawahimiza Masahaba wake kuamiliana kwa wema na uzuri pamoja na wafuasi wa dini nyengine, pamoja na kushikamana na ufahamu sahihi wa kiini cha Akida ya Kiislamu na kuchanganyika na watu kwa tabia za Kiislamu na maadili yake mazuri, na imepokewa kuwa Mtume (rehema na amani ziwe

juu yake) alisimama kwa ajili ya jeneza la Myahudi katika mji wa Madina, jambo ambalo lilileta mshangao kwa Masahaba zake, akawaambia: "Jee! si mtu" Amepokea Bukhari kwenye "Jaami Sahihi" (2/85) namba (1312) na Muslim kwenye "Jaami'i Sahihi" (3\/58) namba (961), anamaanisha kuwa huyo ni binaadamu bila ya kutizama kabila lake na dini yake na daraja yake ya kijamii na mauti ni haki kwa watu wote.

## Ujirani mwema na wasiokuwa Waislamu

Mazungumzo chanya

Katika zama za Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) Waislamu waliishi pamoja na Mayahudi katika mji wa Madina na wakabadilishana manufaa ikiwemo kuuza na kununua mpaka ikatokea Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alifariki na ngao yake ya kivita ilikuwa ni rehani kwa Yahudi miongoni mwa Mayahudi wa Madina.

Na tarekhe ya Kiislamu imejaa mifano ya ujirani mwema kwa miaka mingi baina ya Waislamu na Manasara na wengineo katika wafuasi wa dini nyengine. Na hayo yalijitokeza kutokana na mafunzo ya Kiislamu ambayo yanaamrisha uadilifu na kukataza dhulma.

Na umeingia Uislamu Indonesia kwa kufika wafanyabiashara Waislamu katika kisiwa cha Sumatra katika karne ya kumi na tatu AD, na yakawa matengamano yao mazuri na matukufu pamoja na watu wake ambao walikuwa wanatokana na Makabila ya dini tofauti kama Budhi na Hindu (kwa sasa idadi ya Waislamu katika nchi ya Indonesia ni zaidi ya watu milioni mia mbili)



## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anapokea Ujumbe wa Kinasara katika Msikiti wake.

Baada ya miaka kumi takribani kutoka Hijra ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ya kuelekea Madina Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) aliwapokea wajumbe wengi wakiwemo wajumbe wa Wakristo wa mji wa Najran waliokuja kutoka Yemen, akawapokea Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) Msikitini mwake, na akawaruhusu wasali (Sala zao) kisha akazungumza nao kwa njia nzuri, akawafahamisha Uislamu na akajibu maswali yao.



"Waite (watu) katika njia ya Mola wako kwa hikima na amani, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora (siyo kwa kuwatukana wao au kutukana dini yao. K wa njia hii huwezi kumvuta mtu). Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake, naye ndiye anayewajua walioongoka"

Suratul-Nahli aya ya 125.

"Wala msibishane na watu waliopewa Kitabu (kabla yenu) ila kwa yale (majadiliano) yaliyo mazuri, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: "Tunaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu, na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja; nasi ni wenye kunyenyekea kwake" Suratul-'Ankabut aya ya 46.





**Msikiti wa Omar (radhi za Allah ziwe juu yake) na kanisa la Qiyamah la Quds Palestina**

## Usamehevu wa dini

Mji mkongwe wa Quds unao mfano mkubwa unaendelea maridhiano ya kidini na mfano huu unaendela kuwepo tokea karne kumi na nne, pale alipoingia kiongozi wa Waislamu Khalifa Omar bin Khatwab (radhi za Allah ziwe juu yake) katika mji wa Quds kwa amani bila ya kumwaga hata tone la damu mnamo mwaka 638 AD. Alipokea mwaliko kutoka kwa Askofu wa Quds aitwae Sofronius kutembelea Kanisa la Qiyamah ambalo ni Kanisa kubwa katika mji wa Quds.

Na ulipofika muda wa Sala Askofu alimwita Khalifa Omar ili asali ndani ya Kanisa lakini Khalifa Omar (radhi za Allah ziwe juu yake) alihofia kuzozana Waislamu na Manaswara juu ya umiliki wa kanisa hilo pindi akisali ndani ya Kanisa hilo.







akasali umbali wa mita kadhaa kutoka kwenye Kanisa hilo, na ulipopita muda ulijengwa sehemu hiyo Msikiti ili kulidumisha tukio hilo la kihistoria, na unaitwa Msikiti huo kwa jina la "Masjid Omar".

Na Kanisa la Qiyamah linazingatiwa ni moja kati ya Makanisa makongwe zaidi ulimwenguni, kwa kuwa limejengwa juu ya jiwe kubwa ambalo wanaamini Manasara wa sasa kwamba Nabii Issa (amani iwe juu yake) amesulubiwa hapo katika mji wa Quds ya zamani.

Na vile vile kuna kaburi takatifu (yaani sehemu ambayo Manasara wanadai kuwa Nabii Issa (amani iwe juu yake) amezikwa hapo. Ama Kanisa liitwalo "Al-Mahdi" liliopo katika mji wa Bathleham hilo ni Kanisa ambalo wanaamini Manasara kuwa Nabii Issa (amani iwe juu yake) amezaliwa hapo, na pia huzingatiwa kuwa ni moja kati ya Makanisa makongwe ulimwenguni.




Hati ya Khalifa Omar bin Khatwab (radhi za Allah ziwe juu yake)




Mlango wa kuingilia Masjid Omar

Wakati Khalifa Omar bin Khatwab (radhi za Allah ziwe juu yake) alipopokea funguo za Quds akamteua kuwa Kadhi wa mji huo Sahaba Ubada bin Swamit Al-Khazrajiy (radhi za Allah ziwe juu yake) kutoka mji wa Madina, akawa ndie Kadhi wa kwanza Muislamu wa Quds, na akatakiwa kuhifadhi na kulinda Makanisa ya Manasara.

Na alifariki Sahaba Ubada bin Swamit Al-Khazrajiy (radhi za Allah ziwe huu yake) ndani ya mji wa Quds na alizikwa katika makaburi yaliyopo katika mlango uitwao "Ar-Rahma" upande wa kusini wa kuta (uzio) ambao umezunguka Quba As-Swakhrah (Quba la manjano) na Masjid Aqswa.

### Hati ya Mkataba wa Khalifa Omar (radhi za Allah ziwe juu yake) ni mfano tosha wa usamehevu wa kidini

Khalifa Omar bin Khatwab (radhi za Allah ziwe juu yake) alisisitiza uadilifu wa Uislamu na kuishi kwa amani baina ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Akawapatia watu wa Quds ahadi inayodhamini uhuru wa kuabudu na kulinda amani yao na Makanisa yao na vitu vyao, na iliendelea ahadi hii au Mkataba huu kuwepo katika kuta za Msikiti karne nyingi.



Na katika zama zetu hizi watalii na watu wanaozuru Quds wanauona ubao wa jiwe ulio mweupe uliotundikwa katika kuta za Msikiti wa Khalifa Omar na umeandikwa ndani yake kwa kuchimbwa "Ahadi ya Omar bin Khatwab kwa watu wa Elia (Quds)."

Na la muhimu kuelezwa ni kwamba Ahadi ya Khalifa Omar (radhi za Allah ziwe juu yake) ni sehemu ya makubaliano yaliyokusanya masharti ya haki za Waislamu vile vile.

### Sehemu ya Mkataba (wa Ahadi) wa Khalifa Omar

Hii ni ahadi aliyowapa mja wa Allah kiongozi wa Waislamu (Omar bin Khatwab) watu wa Elia (Quds), amewapa amani ya nafsi zao na mali zao na Makanisa yao, Misalaba yao,na wagonjwa na wasio na hatia, na madhehebu yao, kwamba: Makanisa yao hayatokaliwa wala hayatovunjwa wala hayatopunguziwa wala kheri zao wala Msalaba wao wala hazitoharibiwa mali zao wala hawatotezwa nguvu katika kubadili dini yao wala hatodhuriwa mtu yoyote miongoni mwao wala hakuna Yahudi atakayeishi nao hapo Elia.

## TATU: MAADILI YA KAZI NA BIA

**Mtume (rehema na amani iwe juu yake) anahimiza kufanya kazi ya halali na ushindani wa Haki.**

Mtume Muhammad (rehema na amani iwe juu yake) alilingania kufanya biashara kwa mujibu wa Maadili mazuri ya Kiislamu ambayo yanapinga hadaa na miamala isiyo na Maadili na hadaa na udanganyifu na kufutika mali na ubinafsi, na akalingania watu kuwepesisha mauziano ya kibiashara kati yao kwa misingi ya ukweli, uaminifu, ushindani mzuri na kukimbilia kupata pato la halali.

Amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake):

"Amerehemewa na Allah Mtukufu mja mwenye kufanya wepesi wakati anapouza na wakati anaponunua na wakati anapokopa" Amepokea Bukhari (1970).

Kuwa mkweli wala usiwafanyie watu hadaa, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alipita katika soko akamuona mtu mmoja anauza chakula akaingiza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) mkono wake ndani ya chakula hicho akahisi umaji umaji ndani yake akasema: “Nini hiki ewe mwenye chakula? Akasema: chakula hiki kimepatwa na mvua, akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwanini hujakiweka juu (hicho kilichoroa) ili watu wakione? kisha akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Yeyote atakaetufanyia udanganyifu basi si katika sisi" Amepokea Muslim (150).

## Jiepushe na Unafiki... na ni upi huo Unafiki?

Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): "Mambo manne mwenye kuwa nayo atakuwa ni mnafiki wa wazi wazi, na atakae kuwa na jambo moja katika mambo hayo atakua na sehemu ya unafiki mpaka atakapoliwacha jambo hilo,

**Kataa Unafiki**

- Akiaminiwa hufanya khiyana
- Akizungumza husema uwongo
- Akiahidi hatekelezi
- Anapogombana huchupa mipaka

.(Amepokea Bukhari (34) na Muslim (58



**Biashara Huria:** Na imepokewa kwamba baada ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kuhamia Madina amekuta Mayahudi wanachukua kodi kwa mwenye kuuza na kununua katika masoko yao, akaamrisha kununuliwa kipande cha ardhi na ifanywe ardhi hiyo kuwa ni sehemu ya biashara huria. Na ikaitwa ardhi hiyo kwa jina la "Al-Munakha" ambapo watu wanauza na kununua ndani yake bila ya kutoa kodi.



Maana ya neno "Al-Munakha" ni sehemu ambayo ngamia hupiga magoti ili kushusha mzigo uliopakiwa juu yake kwa lengo la kufanyiwa biashara. na sehemu hio ya ardhi ipo mpaka leo.

**Sehemu ya Biashara huria**

Moja ya Masoko ya mji wa Madina



Picha ya kisasa inayoonesha ukuta wa kisasa wa soko la "Al-Munakha" mji wa Madina Munawwara.



Picha ya Jaami'i Sultan nchini Oman, na inaonesha wazi Sanaa ya ujenzi wa Kiislamu kupitia ujenzi wa dari za mbao na nakshi zenye kuelekeana na mapambo ya ukuta.



Neno "Muhammad" lililoandikwa kwa utaalamu wa Sanaa kwa umbo la Kuba na umbo la milango ya Kuweit Kazi hiyo imefanywa na mtaalamu wa khati wa Kuweit Farid Ally.



**"Mbora wa watu ni mwenye kunufaisha watu"**

Ni kazi ya mtaalamu wa khati Hassan Shalaby.



Masjid Quba As-Sakhra – Quds - picha ya mpiga picha mtaalamu Peter Sandar.

SURA

# 6

# HAKIZAMWANAMKE





154

# HAKI ZA MWANAMKE

Katika zama zilizopita na kabla ya Uislamu haki za mwanamke zilikuwa chache sana, na mtazamo wa watu kiujumla ulikuwa mbaya kiasi ambacho katika baadhi ya jamii mwanamke akizikwa pamoja na mumewe atakapokufa mume huyo kabla ya mke, au anakua mwanamke huyo ni katika miliki ya jamaa zake mumewe baada ya kufa mume.

## Hakuna kubagua baina ya watoto wa kiume na wa kike

Waarabu kabla ya Uislamu walikuwa wakiwapenda watoto wa kiume kuliko wa kike, na baadhi yao walikuwa wakiwazika watoto wa kike wakiwa hai, lakini Uislamu ukazikataa tabia hizi zisizo za kiutu, na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akatilia mkazo kuwapenda watoto na kuwafanyia uadilifu kati yao na kutowabagua baina yao bali amehimiza kuwatunza watoto wa kike na kuwalea vizuri mpaka wawe wakubwa na kuolewa.

Na amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika sehemu nyingi: "Usianeni kuwafanyia wema wanawake" Amepokea Bukhari na Muslim.

Na amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika yale yanayohusu hukumu za Sharia: “Hakika wanawake ni wenza wa wanaume” Amepokea Abu Dawd katika “Sunan” (1/95) namba (236) na Tirmidhy katika “Jaami'i” (1/154) namba (113) na Ahmad katika “Musnad” (12/6314) namba (26836) kutoka hadithi ya Ummu Suleym (radhi za Allah ziwe juu yake).

## Uislamu umempatia Mwanamke haki ya kurithi.

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amekuja na mfumo wa mirathi kutoka kwa Allah Mtukufu ambao hakuna kiumbe aliyeingiza lake katika mfumo huo. Mfumo huo umempa mwanamke haki ya urithi, hayo yakawa ni mabadiliko ya Ustaarabu na mageuzi makubwa katika mfumo wa kijamii kwa jamii ambayo haimpi mwanamke

haki ya kurithi na mifumo hiyo ilikua ikizingatia mwanamke ni sehemu ya vimiliki vya mwanamme na sehemu ya mirathi wakati anapokufa mumewe, na baadae mfumo wa mirathi ya Kiislamu ukawa marejeo ya Wanasheria wengi ulimwenguni.

### Uislamu umempatia Mwanamke utambulisho wa kujitegemea




Uislamu unamuangalia mwanamke kuwa ni mtu kamili aliyehuru na anadhati maalumu na utambulisho unaojitegemea, na anajulikana kwa nasaba yake na familia yake na wala halibadilishwi jina la Ukoo wake baada ya kuolewa kama ilivyo hali ya jamii nyingi za Kimagharibi. Mwanamke ni mwajibikaji mbele ya sheria, anahaki zake anazostahiki ana wajibu unaomlazimu na wala hatofautiani na mwanaume isipokuwa kwa baadhi ya Sheria na majukumu.

### Mwanamke ana nafasi kubwa katika jamii ya Kiislamu

Hakika Uislamu umemshika mkono mwanamke na kuutambua mchango wake katika kujenga jamii pasi na kuchupa mipaka au kugongana nafasi yake na ya mwanamme bali kila mmoja hukamilisha la mwenzake, pamoja na kwamba kazi ya mwanamke imewekwa nafasi ya kwanza katika kulea watoto na kuwakuza makuzi mema ili watoto wawe chanzo cha kujenga jamii na wasiwe chanzo cha kuharibu jamii. Basi mwanamke wa Kiislamu amekuwa na nafasi kubwa katika maisha ya jamii na siasa.

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alipanga siku maalumu katika wiki ya kuwafunza wanawake na aliwataka wanawake wahudhurie Sala ya Idi na kushiriki katika kuunga mkono na kutoa fikra zao, alikua akiwataka ushauri Wake zake katika mambo ya kidunia kama alivyokuwa akichukuwa ushauri kwa Masahaba zake nao wakimshauri Mtume na

kupeleka mambo yao, mpaka wajakazi na watumishi wa kike walikua hawaogopi kwenda kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ili kupeleka maombi na madai yao. Na Uislamu umemhimiza mwanamke afanye kazi katika nafasi za kutumikia jamii na kulea kizazi kama vile ufundishaji, kuuguza na kutibu.

### Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) anahimiza kuamiliana na mwanamke kwa vizuri.

Amehimiza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika sehemu tofauti kuamiliana na mwanamke kwa njia nzuri, na akamfananisha mwanamke na chupa ya kigae yenye sifa ya kuvunjika haraka yaani anahitaji muamala wa upole.

Na imepokewa katika hadithi kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesisitiza umuhimu wa kuwalea wanawake malezi mema mpaka wawe wakubwa, na kwamba mwanamme ataingia peponi kwa malezi mazuri ya watoto wake wa kike na akawalea malezi yaliyobora mpaka wawe wakubwa.

**Kama alivyohimiza kuwa na subra kutokana na maudhi yao akaseme Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): “Mwenye kujaribiwa (kupewa mtihani) kwa watoto wa kike akawatendea wema basi watakua watoto hao ni stara kwake kutokana na moto.”** Amepokea Bukhari (1418) na Muslim (2622).

### Mwanamke sio chombo cha starehe

Mwanamke ni nusu ya jamii, Allah Mtukufu amemuandaa ili awe mwajibikaji katika kulea na kukuza kizazi cha baadae, sasa vipi ihujumiwe nafasi yake kwa kufanywa ni chombo cha starehe (ngono), kama ilivyo kwa baadhi ya jamii ambazo Ukahaba umekuwa ni kazi, na biashara ya kujiuza mwili (ngono) imekua ni kivutio cha Utalii na sehemu ya uchumi. Hakika Uislamu umezuia yote hayo na ukakataza Zinaa na mahusiano ya ngono yaliyo nje ya mfumo wa ndoa. Na zimekataza aya za Qur-an kuwateza nguvu wanawake katika ngono kwa ajili ya kupata mali na zikatahadharisha kukurubia Zinaa (kufanya ngono bila ya ndoa).

"Wala msikikaribie zinaa. Hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kabisa)." Suratul-Israa aya ya 32.

## Hadhi maalum na daraja kubwa aliyonayo Mama katika Uisilamu



Uislamu umetukuza daraja ya wazazi wawili na ukasisitiza kuwaheshimu, amesema Allah Mtukufu: "**Na Mola wako amehukumu kuwa msimuabudu yoyote ila Yeye tu. Na (ameagiza) kuwafanyia wema (mkubwa) wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee, (naye yuko) pamoja nawe, au wote wawili, basi usiwaambie hata Ah! Wala usiwakemee. Na useme nao kwa msemo wa hishima (kabisa).** (23) **Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa (njia ya kuwaonea) huruma (kwa kuwaona wamekuwa wazee). Na useme: "Mola wangu! Warehemu ( wazee wangu) kama walivyonilea katika utoto."**
(24) Suratul- Israa aya ya 23-24.

Bwana mmoja alimuuliza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): Ni nani mwenye haki zaidi ya kuwa nae (kwa wema)? akajibu Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Ni mama yako" akasema yule bwana kisha nani: Akajibu Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Ni mama yako" akarejea bwana huyo suala lake na likawa jawabu la Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwa mara ya tatu ni "mama yako", na kutokana na msukumo wa kutaka kujua zaidi akarejea tena bwana huyo suala lake kwa mara ya nne na likawa jawabu la Mtume (rehema na amani ziwe juu ake): "Ni baba yako." Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikusudia kuitukuza nafasi ya mama katika jamii ya Kiislamu

Neno hili "Muhammad" kwa kiarabu, limechorwa kwa umbo la Kisanaa la mfanano, linafanana nusu yake ya kwanza na nusu ya pili, ni kazi ya Ustadh Farid Al-'Aliy.

na umuhimu wa kupatiwa muamala mzuri kutoka kwa watoto wake. Amepokea Bukhari katika “Jaami'i Sahih” (8/2) namba (5971) na Muslim katika “Jaami'i Sahih” (8/2) namba (2548) kutoka hadithi ya Abu Huraira (radhi za Allah ziwe juu yake).

Na baadhi ya wanavyuoni wanaelezea kusudio la hadithi ya kwamba, mama anapitia aina tatu za matatizo, nayo ni:

**1. Kubeba ujauzito.** **2. Uchungu na kujifungua.**

**3. Kunyonyesha na kuachisha.**

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anahimiza kuishi vizuri na Mke.

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa akiusia wafanyiwe wema wanawake na hilo ni katika kutekeleza amri ya Allah Mtukufu aliposema: “...Na kaeni nao kwa wema...” Suratu-Nisaa aya ya 19. Na amehimiza Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) katika matukio mbalimbali kuamiliana vyema na Mke, hata katika hotuba yake ya mwisho aliyoitoa kwa Waislamu “Hotuba ya kuaga” akafungamanisha baina ya kuamiliana vyema na wanawake na ukamilifu wa Imani na tabia njema.Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): “Mkamilifu wa imani katika Waumini ni yule mwenye tabia njema zaidi, na mbora wenu ni yule mbora wenu kwa wake zake.” Amepokea Al-Hakim katika “Mustadrak” (1/3) namba (1) na Abuu Daud katika “Sunan” (4/345) namba (4682).



Mchoro uliotengenezwa na mtaalamu wa khati Wisam Shawkat, ni dua (maana yake) "Ewe Mola mwenye kugeuza nyoyo uthibitishe moyo wangu kwenye dini yako na katika kukutii wewe.”

# KUMHIFADHI MWANAMKE.

## Hijabu katika Uislamu



Hijabu katika Uislamu ni jambo la wajibu kwa kila mwanamke aliyebaleghe, nayo ni msisitizo wa kulazimiana na kivazi cha heshima na kujistiri sehemu zenye kufitinisha katika kiwiliwili, na kwenye hilo ni kumlinda mwanamke kutokana na kuvamiwa na kutamaniwa na wenye nafsi dhaifu. Kama ilivyokuwa kujilazimisha mwanamke na mavazi ya heshima ndani yake kunamlinda mwanamme kutokana na kuamsha hisia na matamanio, kwa sababu hio Uislamu umemzuwia mwanamke kudhihirisha kiwiliwili kutumia sehemu zake za kuvutia kwa ajili ya kuvutia wamuonao, au kuwavutia watu katika namna yoyote ile ikiwemo kwenye picha, filamu, matangazo ya biashara ambayo wanategemea kuyadhihirisha maeneo yenye kuvutia ya mwanamke na kuhadaa kwa ajili ya kuitangaza biashara. Na Uislamu umefunga mlango wa kila machafu kama kukaa utupu, na filamu chafu, na Ushoga, na mahusiano yasiyokua ya kisheria, na kubaka,na yanayofungamana nayo ikiwemo kuwepo watoto wa nje ya ndoa na kutoa mimba na kila maradhi mabaya yanayo sababishwa na ngono.



## Hakuna mahusiano nje ya mipaka ya ndoa




Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake juu) amehimiza kuoa ili kuanzisha mwanzo mwema wa jamii, na akawafundisha Waislamu Maadili mema na misingi mikubwa ya kuanzisha mahusiano baina ya mwanamme na mwanamke na kuzuia mahusiano ya ngono nje ya mfumo wa kisheria (Ndoa).

Amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Enyi vijana mwenye uwezo wa kuowa kati yenu na aowe kwa sababu kuowa kunashusha macho chini na kinga ya utupu. Na akasema vile vile: "Hazini mzinifu wakati anazini akawa ni Muumini wala haibi mwenye kuiba wakati anaiba akawa Muumini wala hanywi pombe mwenye kunywa wakati anakunywa akawa Muumini" Amepokea Bukhari katika "Jaami'i Sahih" (3/26) namba (1905).

Alikuja kijana mmoja kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akamuomba Mtume amruhusu kuzini! Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamuuliza kijana huyo: "Unapenda (kuziniwa) kwa mama yako?" akajibu kijana "Hapana Wallahi, Allah anijaalie mimi nikuzuilie mabaya yasikukute" akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "hivyo hivyo watu hawapendi (kuziniwa) kwa mama zao, kisha akarejea tena Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kumuuliza: "Unapeda (kuziniwa) kwa mwanao?" akajibu

kijana: "Sipendi", akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Na watu hawapendi (kuziniwa) kwa watoto wao", akamuuliza tena Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Je unapenda (kuziniwa) kwa dada yako?" akajibu kijana: "Sipendi", akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Na watu hawapendi (kuziniwa) kwa dada zao, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamuuliza tena kijana huyo: "Unapenda (kuziniwa) kwa shangazi yako?" akasema

kijana: “sipendi”, akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): “Na watu hawapendi (kuziniwa) kwa Shangazi zao” akamuuliza tena kijana huyo: “Je unapenda (kuziniwa) kwa mama yako mdogo?” akasema kijana: “sipendi”, akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): “Na watu hawapendi (kuziniwa) kwa mama zao wadogo.” Akaweka Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) mkono wake katika kifua cha kijana huyo na akasema “Ewe Mola wangu msamehe dhambi zake na usafishe moyo wake na uhifadhi utupu wake. Amepokea Ahmad katika “Musnad” (10/5220) namba (22641), (10/5221) namba (22642) kutoka hadithi ya Abu Umamah (radhi za Allah ziwe juu yake).

## Ndoa ni neema kutoka kwa Allah Mtukufu

Ndoa ni mafungamano matukufu yaliyotukuka kwa sharia



ya Allah Mtukufu baina ya mwanamme na mwanamake juu ya misingi madhubuti ya mapenzi na upole na kujitolea. Ni lazima kwa wanandoa washirikiane ili kuifanikisha ndoa na kuidumisha na iwe katika malengo yao ni kuleta utulivu wa nafsi na amani ya moyo kwa mwanamke na mwanamme na kuzaa kizazi kilicho chema.

> "Na katika Ishara zake (za kuonyesha ihsani zake juu yenu) ni kuwa Amekuumbieni wake zenu katika jinsi yenu ili mupate utulivu kwao, naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika haya zimo Ishara kwa watu wanaofikiri” Suratu-Rruum aya ya 21.



## Talaka katika Uislamu

**Talaka Kwa Masharti**

Na kwa upande mwengine Uislamu umehalalisha Talaka wakati mahusiano ya ndoa yatakapoharibika na ikashindikana kuendelea na maisha hayo, na Qur-an Tukufu ikaweka sharti za Talaka na kanuni ili kuhifahi haki za mwanamke na nasaba na haki za wanaozaliwa au watoto na kuwalea baada ya Talaka.

> Amesema Allah Mtukufu: "Talaka (unazoweza kumrejea mwanamke) ni (zile zilizotolewa) mara mbili (za kwanza). Kisha ni kumweka kwa wema au kumwacha kwa ihsani" Suratul-Baqarah aya ya 229.

Talaka ni jambo lenye kuchukiza kwa sababu ndani yake kuna kuvunja ahadi nzito ahadi ambayo imefungwa kwa Sharia ya Allah Mtukufu na dini yake, na inapaswa wanandoa wasikimbilie kwenye Talaka isipokuwa baada ya kushindikana njia za ukweli katika kutatua mzozo uliopo baina yao kabla haijafikia kwenye tatizo sugu linalokuwa kila kukicha litakalofanya jambo la talaka kuwa halina budi litokee.

---

Hili ni neno "Muhammad" kwa lugha ya kiarabu, alieliandika mtaalamu Farid Al-'Aly lililopo kwenye umbo la Uwa na kichwa cha Uwa ndio herufi ya "Mim" ya kwanza ya nenon Muhammad, ama "Mim" ya pili ipo katika umbile la jani.



## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ni mume mwenye mapenzi na muaminifu.

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa ni kigezo kwa Masahaba zake katika kupenda na uwaminifu kwa wake zake, kwani aliishi miaka ishirini na tano akiwa na Bibi Khadija (radhi za Allah ziwe juu yake) mpaka alipofariki, na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) siku zote alikuwa anataja sifa za Bibi Khadija na akiwakirimu shoga zake baada ya kufariki. Na wakati Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alipomuowa Bibi Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake) alikuwa anacheza nae na kushindana nae na anazungumza nae kwa nambo anayoyapenda Bibi Aisha kama Sira ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) inavyoeleza.



## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anayathibitisha mapenzi yake kwa wake zake.

Bibi Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake) alimtajia Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kisa cha mapenzi cha “Abuu Zar’i” kwa mke wake, baada ya kumaliza kusimulia kisa akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kumwambia mke wake: “Nimekuwa kwako kama Abu Zar’i kwa Mama Zar’i.” Na Sahaba mmoja alimuuliza Mtume (rehma na amani ziwe juu yake): “Ni Mtu gani anapendeza zaidi kwake?” akajibu Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) “Aisha”, akauliza tena: kisha nani? Akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): “Baba yake, Abu Bakar” Amepokea Bukhari katika “Jaami'i Sahih” (5/5) namba (3662). (5/165) namba (4358) na Muslim katka “Jaami'i Sahih” (7/109) namba (2384).

Na alipokuwa bibi Safiya bint Huyai (radhi za Allah ziwe juu yake) ni mke wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake), watu walimsema kuwa ni mtoto wa Kiyahudi, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamwambia kwa mahaba na mapenzi: "Wewe ni mtoto wa Nabii Mussa (amani iwe juu yake) na Ami yako ni Nabii Harun (amani iwe juu yake), na ni mke wa Mtume (yaani mke wa Muhammad Mtume wa Allah na Mjumbe wake) (rehema na amani ziwe juu yake). Amepokea Tirmidhiy katika "Jaami'i"(6/188) namba (3894) na Ahmad katika "Musnad" (5/2609) namba (12587).

Na alipofariki Mtume (rehema na amani ziwe juu yake), Bibi Safia (radhi za Allah ziwe juu yake) alielezea mapenzi ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na mahaba yake na muamala wake mzuri kwake.

## Kuoa Wake wengi katika Uislamu

**Kuowa wake wengi lilikuwa ni jambo lililoenea kabla ya Uislamu.** Kuoa wake wengi lilikuwa ni jambo lililoenea na lenye kukubalika, na hakuna dalili bora kama Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) alikuwa na wake wawili Bibi Sara na Bibi Hajar, na kwa mujibu wa mapokezi ya Injili, Nabii Ya'aqubu (amani iwe juu yake) alikuwa na wake wawili na vijakazi wawili. Na ilikuwa imeenea katika jamii kabla ya Uislamu jambo la kuwa na wake wengi bila ya mipaka, na ilienea katika jamii ya Bara Arabu mwanamme kuwa na wanawake wengi iwe sawa ni wakeze au vijakazi.

**Uadilifu kabla ya kuoa wake wengine**

Kwa hivyo Uislamu haukuamrisha watu kuoa wake wengi bali umekuja na Sharia za Allah Mtukufu kupanga na kuweka kikomo katika kuoa wake wengi kwa maslahi ya mwanamme na mwanamke na jamii, Uislamu umeweka mipaka ya wake wanne tu, na ukaweka masharti ya kuwa na wake wengi na msingi mkubwa ni uadilifu kati ya wake katika kuweka zamu ya kulala pamoja na (uadilifu katika) chakula mahitaji mengine, na Uislamu umemlazimisha

mwanamme kutosheka na mke mmoja ikiwa hawezi kufanya uadilifu kwa mke wa mwanzo na mwengine katika wake zake.

"...Na mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi (oeni) mmoja tu" Suratu-Nisai aya ya 3

"Nanyi hamwezi kufanya uadilifu (kwelikweli) baina ya wake, ijapokuwa mtataka kufanya hivyo..." Suratu-Nisai aya 129.

Na pia ipo Hekima kubwa ya kuruhusiwa kuoa mke zaidi ya mmoja na kuweka nidhamu zake, kwani mwanamme anaweza kugundua mke wake ni Tasa (hazai) na vile vile huenda mke akapata ajali au ugonjwa jambo linalopelekea kutokutekeleza haki za kindoa ikawa kuoa mke wa pili ni bora kuliko kumuacha mke wa mwanzo, na kwa upande mwengine hutokezea mwanamke akawa kwa muda mrefu imeshindikana kuolewa na pia ikatokea mwanamke akamkosa mumewe na akawa mjane anahitaji mume akaridhika kwa mume aliyeoa mke mwengine badala ya kubakia peke yake bila ya mume. Kwa hivyo kuwa na mke zaidi ya mmoja inathibitisha faida kwa pande zote mbili na kupelekea msaada na ukamilifu katika jamii kupitia vipengele vya sharia vinavyozuia kuenea kwa machafu na khiyana ya kindoa.

Baada ya vita vya pili vya dunia waliuliwa wanaume wengi katika jamii ya Wajerumani na ikaongezeka idadi ya wanawake, katika hali kama hii inakuwa kuoa wake wengi ni ufumbuzi wa kutosha kwa jamii inayodhamini kuhifadhi nasabu na kulinda vizazi vipya kutopotea na kuzuwia kuenea zinaa na machafu.

## Je! Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alioa wake wengi?

Mke mmoja miaka 25

Pamoja na kuwa kuoa wake wengi na kuwa na vijakazi wengi lilikuwa limetawala kwa Makuraishi; lakini Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alioa mke mmoja kwa muda wa miaka ishirini na tano mpaka alipofariki mke wake huyo. Na alikuwa baba wa watoto wanne wa kike na wawili wa kiume. Baada ya kufariki mkewe Bibi Khadija (radhi za Allah ziwe juu yake) alioa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akiwa na miaka hamsini alimuoa Bibi Sawda bint Zam'a (radhi za Allah ziwe juu yake) aliyekuwa mjane mwenye umri mkubwa ambapo alifariki mume wake baada ya kurejea pamoja nae kutoka Uhabeshi, na walitumia muda mrefu huko kwa ajili ya dini na kutekeleza amri ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake)

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anaoa mtoto wa rafiki yake Sahaba Abubakar Assiddiq (radhi za Allah ziwe juu yake)

Baada ya miaka michache toka kufariki Bibi Khadija (radhi za Allah ziwe juu yake) alihama Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kutoka Makka kwenda Madina na akamuowa bibi Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake) ambae ni mtoto wa Sahaba wake na rafiki yake wa mwanzo Sahaba Abubakar Assiddiq (radhi zaa Allah ziwe juu yake) nae ni wa kwanza kuingia katika Uislamu katika wanaume, akabeba ujumbe wa Allah Mtukufu pamoja na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake), ndoa hiyo ikawa ni heshima na utukufu kwa Sahaba Abubakar na binti yake (radhi za Allah ziwe juu yao).

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anamuoa mtoto wa rafiki yake Sahaba Omar bin Khatwab (radhi za Allah ziwe juu yake)

Baada ya takribani miaka miwili ya kuhamia Madina, vilitokezea vita vya Uhud na kufariki mume wa Bibi Hafsa bint Omar bin Khatwab (radhi za Allah ziwe juu yake), Sahaba Omar akapeleka maombi kwa Sahaba Abubakar na Sahaba Othman bin Affan (radhi za Allah ziwe juu yao) (ili wamuoe binti yake), wote wakamuomba udhuru kuhusu kumuowa Bibi Hafsa, na akamuowa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kuonesha utukufu wa binti huyo na kwa baba yake.

## Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) anamuoa Mama wa Maskini.

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alimuoa Bibi Zainab bint Khuzaima ambae aliuliwa mume wake katika vita vya Badri au Uhud (kwa mujibu wa baadhi ya mapokezi) na alikuwa akiitwa bibi huyu "Mama wa Masikini" (Ummul-Masaakiin) kwa sababu alikuwa anapenda kutoa sadaka na kuwalisha maskini, kufanya mambo mema, isipokuwa alifariki muda mchache baada ya kuolewa na Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake).

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anamuoa Bibi Ummu Salamah (radhi za Allah ziwe juu yake), ni mwanamke wa mwanzo aliyehamia Uhabeshi na mtoto wa mtu Mkarimu katika Waarabu.

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alimuoa Bibi Hindi bint Abi Umayya (Ummu Salamah) na akawalea watoto wake baada ya kufariki mumewe (ambae ni ndugu yake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) wa kunyonya na mtoto wa shangazi yake Bibi Barrah) na (mume wa kwanza) alimuachia watoto wanne, alikuwa mwanamke wa mwanzo aliyehamia kwenda Uhabeshi, Ummu Salamah (radhi za Allah ziwe juu yake) alikuwa ni mtu mwenye Hekima na akili nzuri, na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa akichukuwa ushauri (kutoka kwake) katika mambo tofauti.

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anamuowa mtoto wa shangazi yake kwa kutekeleza amri ya Allah ya kuondoa ada ya Kuasili katika Uislamu.

Kama alivyoowa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) Bibi Zainab bint Jahshi (radhi za Allah ziwe juu yake) (mtoto wa shangazi yake Bibi Umaimah) na hiyo ilikuwa ni amri ya Allah Mtukufu ya kuondoa ada ya Kuasili (kumfanya mtoto wa watu kuwa ni mwanao). Na ilishatangulia kwa Bibi Zainab (radhi za Allah ziwe juu yake) kuolewa na Bwana Zaid bin Harithah (radhi za Allah ziwe juu yake) na alikuwa anaitwa Zaid bin Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kwa sababu alilelewa na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake), lakini Bwana Zaid na Bibi Zainab (radhi za Allah ziwe juu yao) hawakuafikiana katika ndoa , kwa hivyo Bwana Zaid akamuacha Bibi Zainab (radhi za Allah ziwe juu yao), na akamuowa yeye Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) baada ya kushuka aya katika Qur-an iliyomruhusu Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kumuoa ili isiwe uzito kwa Waislamu au kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwamba yeye kamuoa mke ambae ni daraja (sawa) na binti yake (kwani hapakuwa kati ya Mtume na Zaid nasabu).

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anamuowa Bibi Juwayriya bint Al-Harith (radhi za Allah ziwe juu yake)

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alimuowa Bibi Juwayriya bint Al- Harith ambae alikuwa mtoto wa kiongozi wa kabila la Bani Mustwaliq, (ndoa hio ilikuwa) baada ya vita vya Bani Mustaliq ambavyo Bibi huyu alitekwa katika vita hivyo, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamuacha huru na akamkirimu na akamuowa, na Waislamu wakawaacha huru mateka wengi waliokuwa katika watu wa Bibi Juwayriya kwa ajili ya kumtukuza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na Bibi Juwayriya (radhi za Allah ziwe juu yake) ambae kawa mama wa Waumini.

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anamuoa mwanamke wa Kiyahudi jina lake anaitwa Bibi Safia (radhi za Allah ziwe juu yake)

Ndoa hii ina kisa ambacho kinarudi kwa kabila la Bani-Nadhiir kabila la Kiyahudi ambalo lilikuwa linaishi Madina na wakaekeana

ahadi na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kuulinda mji wa Madina na kusimama pamoja na kiongozi wa Madina Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) dhidi ya uadui wowote, lakini wakatengua ahadi yao na wakakubaliana kumuua Mtume (rehema na amani ziwe juu yake), ndipo Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akawadhibiti katika mwaka wa nne wa Hijria wakajisalimisha na wakachukuliwa mateka miongoni mwao akiwemo Bibi Safia ambae ni mtoto wa kiongozi wao. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alimwacha huru Bibi Safia (radhi za Allah ziwe juu yake) kisha akamposa nae akakubali baadae akamuowa, na alikuwa yeye pamoja na watu wake wakweli, alikuwa anamsifu Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) hata baada ya kufa kwake kwamba yeye ni mume mwenye mapenzi, mkweli, na mwaminifu.

## Ndoa ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na Bibi Ummu Habiba, Mjane Muislamu na mtoto wa Adui.

Bibi Ramla (radhi za Allah ziwe juu yake) alikuwa maarufu kwa jina la Ummu Habiba mtoto wa Abu Sufyani kiongozi mkubwa wa Makka na ndie aliyefanya uadui na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake kwa muda wa miaka ishirini isipokuwa mtoto wake Bibi Ramla (radhi za Allah ziwe juu yake) alisilimu na akawa ni miongoni mwa wanawake wa mwanzo mwanzo kuhama kwenda Uhabeshi (alihama) pamoja na mume wake, wakaishi huko, na akafariki mumewe huko Uhabeshi, na akabakia Bibi Ramla (radhi za Allah ziwe juu yake) peke yake akiwa ni Muislamu, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamposa nae akakubali kuolewa na yeye. Na Allah Mtukufu akataka baada ya hapo baba yake Bwana Abu Sufyan (rehema na amani ziwe juu yake) kuingia katika Uislamu.

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anamuowa Bibi Maimuna bint Al-Harithi (radhi za Allah ziwe juu yake)

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alimuoa Bibi Maimuna bint Al-Harith (na aliitowa nafsi yake kwa Mtume kwa mujibu wa mapokezi ya sira), na ndie dada wa mke wa Ami yake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) Bwana Abaas (radhi za Allah ziwe juu yao) na mama mdogo wa Ibnu Abbas (radhi za Allah ziwe juu yake) na ndoa hii ilifanyika baada ya Umra ya kulipa. (Mtume) Akawafanyia walima watu karibu na mji wa Makka mpaka Makuraishi wakasema: "mkwe bora kwetu ni Muhammad" (yaani ananasibiana nasi na kuoa kwetu), basi nyoyo zao zikalainika.

## Bibi Mariyah Al-Qibtiyya.

Baada ya kutimia suluhu ya Hudaybia kati ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na Washirikina Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alianza kuwaandikia barua Wafalme wa Mataifa makubwa akiwalingania katika Uislamu, na miongoni mwao ni Muqawqis Mfalme wa Misri, Isipokuwa Muqauqis alijizuilia kuukubali Uislamu na alikuwa mfuasi wa dini ya Kikristo, baada ya hapo akarejesha kwa Mtume (rehema na amani juu yake) barua kwa heshima, pia alimpelekea zawadi na mjakazi jina lake Mariyah. Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alizipokea zawadi za Muqawqis na akamfanya Bibi Mariyah mjakazi wake, basi akasilimu ukawa mzuri Uislamu wake pia akamzalia mtoto akamuita Ibrahim (radhi za Allah ziwe juu yake) lakini alifariki bado ni mtoto mdogo, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akahuzunika kwa kifo chake.



## Kushuka amri ya Allah Mtukufu ya kuweka nidhamu na mipaka ya kuoa wake wengi.

Waarabu walikuwa wanaoa wake wengi bila ya mipaka na hapakuwa na Sheria zinazoonesha haki za wake. Ulipokuja Uislamu ikashuka amri ya Allah Mtukufu kwamba isizidi idadi ya wake wanne, na hairuhusiwi kuoa mke zaidi ya mmoja isipokuwa kwa sharti ya uadilifu kati ya wake na kuchunga haki zao zote.

**Basi Mkiogopa kutofanya Uadilifu basi mmoja**

Na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kabla ya hapo alikwishaoa zaidi ya wake wanne, na lilikuwa jambo hili linataka hukmu maalumu, na kwa sababu Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anapokea Wahyi kutoka mbinguni basi wake zake wakapata bahati ya utukufu wa kuolewa na Mtume wa Allah Mtukufu basi wakawa na daraja ya kuwa Mama wa Waumini ambao wanawafundisha akina mama wa Kiislamu mambo ya dini yao, basi Allah Mtukufu akafaradhisha kwa Mtume na kwa wake zake vidhibiti vinavyo wafikiana na heshima kubwa hii.

## Hukumu maalumu kwa wake zake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake)

Allah Mtukufu aliruhusu Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kubakia na wake zake na akaweka vidhibiti kwao ya kwamba wasiolewe na mtu yeyote baada ya kufariki Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ili iwe heshima kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na heshima kwao kwa sababu wamekuwa mama wa Waumini wote. Qur-ani Tukufu imewasifu wake wa Mtume (radhi za Allah ziwe juu yao) kwamba wao sio sawa na wanawake waliobakia kwa vile ni wajibu wao kuwa vigezo kwa wanawake wote, na kwa hivyo Qur-ani ikaeleza kwamba atakapofanya mmoja wao dhambi basi adhabu yake ni mara mbili zaidi, na wakati wakifanya kheri malipo yake huongezwa mara mbili zaidi.


172

“Ewe Mtume! Waambie wake zako: "Ikiwa mnapenda maisha ya (hii) dunia na uzuri wake (mimi sinayo, na mimi siwezi kukulazimisheni kukaa na mimi katika hali ya ufakiri; basi mkipenda nikuacheni), njooni, nitakupeni kitoka nyumba, (baadhi ya matumizi) na kukuacheni muwachano mzuri." (28) Na kama mnamtaka Allah na Mtume wake na nyumba ya akhera, basi Allah Amewaandalia wafanyao mema hayo, miongoni mwenu, malipo makubwa. (29) Enyi wake wa Mtume! Atakayefanya maovu dhahiri miongoni mwenu, atazidishiwa adhabu mara mbili; na haya ni sahali kwa Allah. (30) Na miongoni mwenu atakayemtii Allah na Mtume wake, na kutenda mema, Tutampa malipo yake mara mbili, na kumwandalia riziki yenye hishima (31) Enyi wake wa Mtume, nyinyi si kama yoyote tu katika wanawake wengine. (Nyinyi wakeze Mtume). Kama mnataka (kufanya jambo la) kumcha Allah, basi msilegeze sauti (zenu mnaposema na wanaume) ili asitamani mtu mwenye ugonjwa moyoni mwake (kufanya mabaya na nyiye) na semeni maneno mazuri: (32) Na kaeni majumbani mwenu, wala msioneshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionesha mapambo yao wanawake wa zama za Ujahili (Ujinga, ukafiri) na simamisheni Sala na toeni Zaka, na Mtiini Allah na Mtume Wake. Allah Anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa nyumba (ya Mtume), na (anataka) kukutakaseni kabisa kabisa (33) Na watajieni (watu) yasomwayo majumbani mwenu katika Aya za Allah na (maneno ya) hikima (ya Mtume), kwa hakika Allah ni Mjuzi wa mambo ya siri na Mjuzi wa mambo ya dhahiri. (34) ” Suratul-Ahzab aya ya 28-34.

## Hiyari kutoka kwa Allah Mtukufu kwa wake zake Mtume (radhi za Allah ziwe juu yao)

Haziruhusu hukumu za Allah Mtukufu kwa yeyote kati ya wake zake Mtume (radhi za Allah ziwe juu yao) kuolewa na mtu baada ya kufariki Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kutokana na heshima ya Mtume na wake zake. Na baada ya kushuka amri ya Allah Mtukufu alimtaka Mtume wake (rehema na amani ziwe juu yake) awape hiyari wake zake wanaotaka kuachwa na kutoka katika majukumu ambayo Allah Mtukufu amewawajibishia Mama wa Waumini au wabakie katika himaya ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na kujitolea maisha yao kwa ajili ya dini ya Kiislamu. Basi ikawa chaguo lao ni kudumisha heshima ya kuishi na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake), na hakuna yoyote aliyeolewa miongoni mwao baada ya kufariki Mtume (rehema na amani ziwe juu yake).

### Maangalizo:

1. Kwa mnasaba wa mapokezi ya kitabu cha Injili kuhusu ndoa za Nabii Ya'aqubu (amani iwe juu yake) kuoa mke zaidi ya mmoja, angalia "Book of Genesis" 22-32 "Kisha akasimama usiku huo na akachukua wake zake wawili na vijakazi wake wawili na watoto wake kumi na moja na kuvuka mto wa "Yabbuq"".

2. Imeruhusu Sharia (Khul'u) nayo ni talaka inayopatikana kwa kutaka mke kuachwa na kushikilia kwa kutoa mali na kumpa mume, "…Basi mkiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Allah, hapo itakuwa hapana dhambi kwao (mwanamume wala mwanamke katika) kupokea (au kutoa) ajikomboleacho mwanamke..." Suratul Baqarah aya ya 229.

3. Allah Mtukufu ameweka Sharia ya (Eda) kwa mwanamke baada ya kutengana na mume wake, iwe kwa sababu ya kuachwa au kufiwa, na jambo hili la Eda linatukuza mafungamano ya ndoa aliyoamrisha Allah Mtukufu baina ya mwanamme na mwanamke, na kujua kutowepo mtoto kwenye mfuko wa uzazi na kuthibitisha nasabu ikiwa mke ni mja mzito, alipoachwa au akadhania kuwa ni mja mzito. Eda ni kipindi anachosubiria mwanamke kabla ya kuolewa na mume mwengine.

| HUKUMU ZA EDA | MWANAMKE ALIYEACHWA NA MUMEWE | MWANAMKE ALIYEFILIWA NA MUMEWE |
|---|---|---|
| Ikiwa ameachwa kabla ya kukutana na mumewe kindoa | Hapana eda | Eda ni miezi minne na siku kumi kama amri ya Allah (Al-Baqarah aya ya 234) |
| Ikiwa ameachwa nae ni mja mzito (ana mimba) | Eda ni kipindi kilichobakia cha Mimba mpaka ajifungue | Eda ni kipindi kilichobakia cha Mimba mpaka ajifunguwe. |
| Ikitokea ameachwa nae si mja mzito | Muda wa Eda ni Quruu tatu (yaani tohara 3 au hedhi) au miezi mitatu kila mmoja kulingana na hali yake) | Eda ni miezi minne na siku kumi |

Inaelezwa kwamba Ada kabla ya Uislamu wanawake wa Kiarabu walikuwa wanalazimika kujizuwia kuolewa mwaka mzima baada ya kufariki waume zao na kujipakaza kwa vitu vyeusi muda wote huo. Ama India kwa mujibu wa Ada za "Saati" za itikadi za Kihindu za mazishi mwanamke alikuwa anachomwa moto na kugeuka jivu baada ya kufiwa na mume wake, ukaja Uislamu ukasisitiza heshima ya mahusiano ya kindoa bila ya kuchupa mipaka.

SURA

7

# HAKI ZA BINAADAMU

## Azimio la Kimataifa la haki za binadamu - Umoja wa Mataifa

Haki za binadamu ni zile haki za msingi kimaumbile ambazo bila hizo hawezi mwanaadamu kuishi kama mwanadamu kamili, na hapana tofauti katika hilo baina ya mwanamme na mwanamke, wote ni sawa sawa mbele ya Kanuni na mbele ya Allah, na katika haki za msingi za kibinadamu ni haki ya kuishi, na haki ya amani, haki ya uhuru na haki ya heshima na haki ya kuhukumiwa kwa njia ya uadilifu.



# UHURU NA UADILIFU NA KULINDA HAKI KATIKA UISLAMU

"Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja; Adamu) na (yule yule) mwanamke (mmoja; Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu basi; siyo mkejeliane). Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Allah ni Mjuzi, Mwenye habari (za mambo yote)." Suratul-Hujurat aya ya 13.

## Uhuru na Heshima ya mwanadamu.



Mfumo wa utumwa ulikuwa umeenea kabla ya Uislamu sio katika Bara Arabu peke yake, bali katika nchi tofauti ulimwenguni, na ilikuwa ni sehemu ya mifumo ya kijamii na kiuchumi kwa jamii nyingi, na walikuwa watumwa ni mali za baadhi ya watu na utajiri wao. Uislamu umeweka vichocheo vinavyohimiza kuachwa huru mtumwa, miongoni mwa vichocheo hivyo ni kuwanunua watumwa au vijakazi na kuwaacha huru kwa ajili ya kujikurubisha kwa Allah au kufutiwa madhambi na kupata msamaha kutokana na kwenda kinyume na baadhi ya Sharia za Kiislamu au kupata msamaha kutokana na kuwafanyia maudhi watumwa bila ya sababu za msingi. Na ikaendelea hali hio katika Uislamu mpaka ilipomalizika mifumo ya utumwa kidogo kidogo mpaka kwisha kabisa.

Siku moja imetokezea Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alimuona mtu anaitwa Abu Masoud Al-Badry anampiga mtumwa wake kwa mijeledi, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamwambia: "Ewe Abu Masoud! Tambua kwamba Allah anauwezo kwako kuliko uwezo wako juu ya huyu kijana" akatulia Abu Masoud akasema hali ya kutaka msamaha kwa Mtume: "Simpigi tena mtumwa baada ya huyu milele, na nitamuacha huru kwa kutaka radhi za Allah" Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema: "lau hukufanya hivyo uso wako ungegusa (siku ya Kiama) moto" Amepokea Muslim katika " Jaami'i Sahih" (5/19) namba (9561).

**Hakuna kuteza nguvu katika dini:** Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alifikisha ujumbe wa Allah Mtukufu na akalingania kuabudiwa Allah Mtukufu peke yake na kutekeleza maamrisho na makatazo yake bila ya kutumia nguvu na kulazimisha watu. Na Qur-ani Tukufu imetilia mkazo kutowalazimisha watu kuacha dini zao kwa sababu haki iko wazi na batili iko wazi na imewahimiza watu kuzingatia ishara za ulimwengu kuhusiana na uwepo wa Allah Mtukufu na kukubali uwongofu wake kwa kufikiria na kukinai kinafsi.

> "Na kama angalitaka Mola wako (kuwalazimisha kwa nguvu kuamini) bila shaka wangaliamini wote waliomo katika ardhi (asibaki hata mmoja). (Lakini Allah hataki kuwalazimisha watu kwa nguvu) Basi je, wewe utawashurutisha (utawashurutiza) watu kwa nguvu hata wawe Waislamu?" Suratu-Yunus aya ya 99.

> "Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini. Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkataa shetani na akamwamini Allah, bila shaka yeye ameshika kishiko chenye nguvu kisichokuwa na kuvunjika. Na Allah ni mwenye kusikia mwenye kujua." Suratul-Baqarah aya ya 256.

## Usawa na kulinda haki katika Uislamu.

Mnamo mwaka 632AD Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alihiji na akahisi anawaaga watu na kwamba kifo chake kimekaribia, akawahutubia watu hotuba ikaitwa Hotuba ya kuaga. Hotuba ilikusanya misingi mingi aliyoiweka Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ili iwe misingi ya maisha inatofautiana na misingi ya wakati wa Ujahilia, na anachotakiwa Muislamu kukifanya mbele ya Allah Mtukufu na mbele ya Waislamu wenzake, basi katika aliyoyasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake):



"Enyi watu Mola wenu ni mmoja na baba yenu ni mmoja, nyote mnatokana na Adamu na Adamu anatokana na udongo, mbora wenu kwa Allah ni mchamungu, hapana ubora kwa Waarabu kwa wasiokuwa Waarabu isipokuwa kwa Uchamungu, je nimefikisha ujumbe? Ewe Mola shuhudia" (Masahaba) wakasema: Ndio (umefikisha), akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Basi aliyekuwepo amfikishie aliye mbali (hayupo)" Amepokea Ahmad katika "Musnad" (10/5586) namba (23972).



"Enyi watu hakika Waumini wote ni ndugu, si halali kwa mtu yeyote mali ya ndugu yake (kuichukuwa) ila kwa ruhusa yake, Je! Nimefikisha? Ewe mola shuhudia, msirejee baada yangu katika ukafiri mkapigana wenyewe kwa wenyewe, nimekuachieni vitu ikiwa mtashikamana navyo hamtopotea baada yake, kitabu cha Allah (Qur-ani tukufu) na Sunna za Mtume wake. Je! Nimefikisha? Ewe Allah shuhudia" Amepokea Al-Hakim katika "Mustadrak" (1/93) namba (317) na Bayhaqy katika "Sunanul-Kubra" (6/96) namba (11640) na Ahmad katika "Musnad" (9/4795) namba (21026).

## Msisitizo wa haki za Mwanamke

Katika hotuba ya kuaga Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alitilia mkazo kwa mara nyengine haki za mwanamke akasema: "Usianeni kuwafanyia wema Wanawake kwani hao kwenu ni wasaidizi hawamiliki chochote, na nyinyi mumewachukuwa kwa amana ya Allah Mtukufu mkahalalisha kustarehe nao kwa amri ya Allah mtukufu, basi muogopeni Allah kuhusu wanawake na Usianeni kuwafanyia kheri, Je! Nimefikisha? Ewe Allah shuhudia" Amepokea Bukhari katika "Jaami'i Sahih" (7/26) namba (5185) na Muslim katka "Jaami'i Sahih" (4/178) namba (1468).

## Kulinda haki za Yatima

Uislamu umesisitiza kwa njia ilowazi kumlea na kumtunza Yatima na kulinda haki zake mpaka akuwe, awe mwerevu na awe na uwezo wa kusimamia mambo yake mwenyewe. Na zimekuja aya za Qur-an zinazoamrisha kuhifadhi mali ya Yatima na kuonya na kuzigusa mali zake kwa dhulma na uadui.

> "Hakika wale ambao wanakula mali ya mayatima kwa dhuluma, bila shaka wanakula moto matumboni mwao; na wataungua katika huo Moto (wa Jahannam) uwakao" Suratu- Nnisai aya ya 10.

Kwa hakika Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amewahimiza Waislamu kuwalea Mayatima na kuwatunza mpaka wawe wakubwa. Akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake):



> **"Mimi na mwenye kumlea Yatima tutakuwa kama hivi Peponi" akaashiria kwa vidole vyake, cha shahada na cha kati kwa pamoja.** Amepokea Bukhari katika "Jaami'i Sahih" (7/53) namba (5304), (8/9) namba (6005).

## Kulinda haki za Warithi...Thuluthi na Thuluthi pia ni nyingi.

Uislamu umehifadhi haki za Warithi na Allah Mtukufu akampa kila mrithi awe mwanamme au mwanamke fungu maalumu katika mirathi kwa mujibu wa nafasi yake katika familia, na inazingatiwa nidhamu ya Mirathi katika Uislamu ni marejeo ya msingi ya Ulimwengu katika mifumo mingi iliyowekwa (na binaadamu), haukupatikana mfumo mwengine uliofafanua kwa undani Mirathi kama ambavyo imekuja katika Qur-ani.

Imesimuliwa na Sa'ad bin Abi Waqas (radhi za Allah ziwe juu yake) - na alikuwa tajiri, kwamba Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alimtembelea akiwa mgonjwa, Sahaba Sa'ad (radhi za Allah ziwe juu yake) akasema kumuuliza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Mimi ninayo mali nyingi na sina mrithi isipokuwa mtoto wangu wa

kike tu, Je! Nitowe sadaka thuluthi mbili ya mali yangu? Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema: “Hapana” akasema (Sa’ad): basi nusu? Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema: “Hapana” akasema: basi Thuluthi? (Mtume) akasema: “Thuluthi (sawa) na Thuluthi ni nyingi, kwani kuwaacha warithi wako na uwezo ni bora kwao kuliko ukawaacha wanaomba omba watu.” Amepokea Bukhari (2742) na Muslim (1628). (Maneno ya mapokezi yametofautiana lakini kisa ni kimoja).

### Kulinda haki za Mali, basi haifai kunyonya (watu) wala kulimbikiza mali”

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alilingania yale yanayojulikana katika zama zetu hizi “kuzungusha mali binafsi” na kutozibakisha au kuzizuwia watu wachache miongoni mwa Waislamu, akahimiza kufanya biashara na kushirikiana kibiashara katika mali, na akaharamisha Riba kama ilivyokuja katika Qur-ani Tukufu, na atakapokopa mtu kwa mwenzake hatostahiki mkopeshaji isipokuwa mtaji wake asidhulumu wala asidhulumiwe. Na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alisema katika hotuba ya kuaga:

“Hakika Riba ya kijahilia imekomeshwa lakini mnastahiki mtaji wenu msidhulumu na wala msidhulumiwe, ameamua Allah kwamba hapana muamala wa Riba, na hakika Riba ya mwanzo naanza nayo (kuikomesha) ni Riba ya ami yangu Al-Abass bin Abdul-Mutwalib.”

> “…bali Allah · ameihalalisha biashara na kaiharamisha riba…” “Allah huyafutia (baraka mali ya) riba: na huyatia baraka (mali yanayotolewa) sadaka. Na Allah hampendi kila kafiri (na) afanyae dhambi.” Suratul-Baqarah aya ya 275 - 276

### Ulazima wa kulipa Deni na kutekeleza Amana

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amesema katika hotuba ya kuaga” “Enyi watu, hakika damu zenu na heshima zenu ni haramu mpaka siku ya kiama, kama ilivyo haramu siku yenu hii na mwezi wenu huu na mji wenu huu, Je! Nimefikisha? Ewe Allah shuhudia, yeyote ambae ana amana ya watu basi airejeshe kwa mwenyewe” Amepokea Muslim katika “Jaami’i Sahih” (4/38) namba (1218).

> “Hakika Allah anakuamrisheni kuzirudisha amana kwa wenyewe (wanaozistahiki). Na mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa haki. Bila shaka mawaidha anayokutoleeni Allah ni mazuri sana. Hakika Allah ndiye Asikiaye (na) Aonaye. Suratul-Nnisai aya (58).

Ilisimuliwa kutoka kwa Salamah bin Akwa’a (radhi za Allah ziwe juu yake) amesema: “Tulikuwa tumekaa na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ghafla likaletwa jeneza, wakamwambia Mtume msalie, Mtume akauliza: “Je! anadaiwa? Wakasema: “Hadaiwi”, akauliza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): je ameacha kitu? Wakasema: “Hapana”, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamsalia. Kisha likaletwa jeneza jengine, Masahaba wakasema: “Ewe Mtume wa Allah msalie” Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akauliza: “Je, anadaiwa? Wakasema: “Anadaiwa dinari tatu”, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema: “msalieni mwezenu”, akasema Abuu Qatada: “Msalie Ewe Mtume wa Allah na mimi nitalipa deni lake, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamsalia.” Ameipokea Bukhari na Nasai.

## Watu wapo sawa mbele ya kanuni na kuhukumiwa.

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ametilia mkazo kwamba watu wote wapo sawa mbele ya sheria za Allah Mtukufu, na mwenye kufanya makosa ataadhibiwa pasi na kuangalia nasaba yake cheo chake na nafasi yake katika jamii, kwani katika kufanyia kazi kanuni ni kuhakikisha uadilifu baina ya watu na kupatikana amani. Na ametilia mkazo Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwamba hakuna mtu atakaekuwa juu ya sheria hata akiwa anatoka katika familia yake. Na ilitokezea Makureishi walishughulika sana kuhusu mwanamke aliyeiba wa kabila la Makhzuum, wakaona hakuna mtu anayeweza kumuombea kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) isipokuwa Sahaba Usama bin Zayd. Sahaba Usama (radhi za Allah ziwe juu yake) akazungumza



na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) nae Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema akiwa amekasirika: "Je unamuombea msamaha katika hukmu miongoni mwa hukmu za Allah?"

### Kisha Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasimama akawahutubia watu akasema:

"Enyi watu: Hakika wameangamia waliokuwa kabla yenu, walikuwa anapoiba mtukufu wanamwachia, na anapoiba aliyekuwa dhaifu, basi wanamsimamishia hukmu. Naapa kwa Allah, lau angeiba Fatma binti Muhammad ningeukata mkono wake." Amepokea Muslim namba (1688).

### Uadilifu wa Mahkama na Uadilifu katika maamuzi (hukmu)

**Kisa cha Tu'umah na Myahudi** Kulikuwa na mtu anaitwa Tu'umah bin Ubayriq, aliiba nguo ya vita, alipojua yule aliyeibiwa, Tu'umah alifanya haraka kwenda kuificha kwa rafiki yake Yahudi na aliapa Tu'umah kwamba hakuiba ile nguo, waliitafuta watu ile nguo wakaipata kwa Yahudi wakamtuhumu kuwa yeye ndiye mwizi wa ile nguo, lakini Yahudi alijitetea kutokana na tuhuma zile akasema kuwa Tu'umha ndie aliyempa ile nguo, watu wa Tu'umah (kabila la Bani Dhafar nao ni Waarabu) walimuomba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amfutie Tu'umah tuhuma za kuiba kwa sababu ile nguo ilipatikana katika nyumba ya Yahudi. Ukateremka Wahyi kwa ajili ya kuhakikisha uadilifu na kuidhihirisha haki ili iwe ni mfano na mazingatio kwa watu, Allah Mtukufu akadhihirisha kwamba Yahudi hakuiba na kwamba Tu'umah ndie aliyeiba." Amepokea Al-Hakim "Mustadrak" (4/385) namba (8256) na Tirmidhiy (Jaami'i" (5/128) namba (3036).

"Hakika tumekuteremshia Kitabu (hiki), hali ya kuwa kimeshikamana na haki ili upate kuhukumu baina ya watu kama alivyokufahamisha Allah; wala usiwe mwenye kuwatetea wale wafanyao khiyana" Suratu-Nnisai aya ya 105.

## Utukufu wa maisha ya binaadamu na heshima yake.

Hakika Allah pekee ndie aliyewapa viumbe vyote uhai na akawaumba kwa lengo maalumu, na Allah Mtukufu hakumuumba kiumbe hai kwa upuuzi tu pasi na lengo lolote, kila kiumbe katika hii dunia anatekeleza wajibu wake ambao Allah Mtukufu amemuumbia, na Allah mtukufu amemfanya binaadamu kuwa ni bwana wa viumbe wote na Kiongozi katika ardhi ili aimarishe dunia kwa mujibu wa mafundisho ya Allah Mtukufu. Hakika kuhifadhi maisha ya binaadamu kwa kumchukulia ni kiumbe na uumbaji mzuri wa Allah Mtukufu inajumuisha kiwango cha uchaMungu na unyenyekevu mbele ya Utukufu wa Allah Mtukufu. Ndio maana ikawa kumuua binaadamu pasi na haki ni uhalifu mkubwa kwa sababu huko ni kumfanyia uadui Bwana wa viumbe (yaani binaadamu) ambae Allah Mtukufu amemuumba hapa duniani. Na ameashiria Allah Mtukufu katika kitabu chake kitukufu (Qur-an) kosa la mwanzo lililofanywa katika ardhi, pale alipomuua Qaabil ndugu yake Haabil nao ni watoto wa Nabii Adam (amani iwe juu yake).

Amesema Allah Mtukufu:

"Kwa sababu ya hayo tukawaandikia wana wa Israili ya kwamba atakayemwua mtu bila ya yeye kuua mtu, au bila ya kufanya ufisadi katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote; na mwenye kumwacha mtu hai (kumsaidia kuishi) ni kama amewaacha hai watu wote. Na bila shaka Mitume wetu waliwajia na hoja zilizo wazi; kisha wengi katika wao baada ya haya walikuwa waharibifu sana katika nchi" Suratul-Maidah aya ya 32.

Hakuna haki kwa binadamu yeyote kumuua mwenziwe isipokuwa kwa idhni ya Allah Muumba na Sharia yake



## Kuua kwa kulipiza kisasi ni haramu katika Uislamu

Uislamu umeharamisha kuua kwa kulipiza kisasi, na ameweka wazi Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika hotuba ya kuaga, alisema "Na hakika damu za kijahiliya hazikubaliki, na damu ya mtu wa mwanzo ninayoanza (kubatilisha kisasi) ni ya A'amir bin Rabia bin A-Harith bin Abdul-Mutalib." Amepokea Tirmidhiy katika "Jaami'i" (5/167) namba (3087) na Ibnu Maajah katika "Sunan" (4/243) namba (3055). Na lililokuwa wazi ni kwamba A'amir bin Rabia anakutana kwa nasabu na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake ) bin Abdillah bin Abdil-Mutalib.

**Kuua kwa kukusudia na kuua pasi na kukusudia**

Hakika adhabu ya kuua kwa makusudi katika Uislamu inakuwa kwa kile kitendo chenyewe, maana yake anayeua na yeye huuliwa Ama ikiwa kuua huko ni kwa makosa au pasi na kukusudia, ni juu yake yule mtu alieua kutoa badali (diya) kwa wale watu wa yule aliyemuua. Adhabu ya kutoa diya katika kipindi cha Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) Ilikuwa ni ngamia mia moja, na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akaeleza kuwa kudai zaidi ya hicho huko ni kurudi zama za Kijahilia.



Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliweka misingi katika kulifundisha jeshi lake tabia na ubinaadamu katika kuamiliana na maadui na mateka, alikuwa akiwakumbusha siku zote kwamba Allah Mtukufu hawapendi watu wenye kufanya uadui.



Amesema Allah Mtukufu "…Na mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa haki…"

Kazi hii imeandikwa kwa khati za Thuluth katika kazi ya Mturuki Hassan Shalaby.

Na amepokea Abu Daud katika hadithi iliyokuwa sahihi kutoka kwa Anas bin Malik (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anapolituma Jeshi kwenda kupigana vita husema: "Nendeni kwa jina la Allah, msimuue mtu mzima wala mtoto mdogo wala mwanamke wala msichupe mipaka, na kusanyeni ngawira zenu na suluhishaneni na fanyeni wema, hakika ya Allah anawapenda wenye kufanya wema."

**Usimuue**

**Mwenye amani asiyepigana wala mwanamke**

**Usikate**

**Mtende Au mti wenye Matunda**

"Na piganeni katika njia ya Allah na wale wanaokupigeni, wala msipindukie mipaka (mkawapiga wasiokupigeni). Kwani Allah hawapendi warukao mipaka." Suratul- Baqarah aya ya 190.

## Kujiua ni kosa kubwa




Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ameweka wazi kwamba kujiuwa ni kosa kubwa, Allah Mtukufu anamuadhibu mwenye kulifanya kosa hilo adhabu iliyokuwa kali, Amesema:

"Mwenye kujiua menyewe kwa chuma basi chuma hicho hicho alichojiulia kinakuwepo mikononi mwake atajichoma katika tumbo lake katika moto wa Jahannamu milele, na mwenye kunywa sumu akajiua atakuwa anakunywa sumu hiyo katika moto wa Jahannamu, na mwenye kujitupa kutoka juu ya jabali na akafa nae atakuwa anajitupa katika moto wa Jahannam milele". Amepokea Bukhari na Muslim.



"Wala mbebaji habebi mzigo wa mwengine"
Ni kazi iliyofanywa na Iswam Abdul-Fattah

**Kataa vurugu**

## Hekima na Mawaidha mazuri

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alitofautiana na wengine kwa upole katika mazungumzo yake na katika kuamiliana na watu, na hakukhiyarishwa kuchagua moja ya mambo mawili isipokuwa huchagua lililo jepesi, na hakulingania watu Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwa kutumia nguvu katika kueneza dini bali alifuata maamrisho ya Allah Mtukufu, **“Na sema: "Huu ni ukweli uliotoka kwa Mola wenu, basi anayetaka na aamini na anayetaka na akufuru."** Suratul- Kahf aya ya 29. Na amesema Allah Mtukufu **“Waite (waite watu) katika njia ya Mola wako kwa hikima na mauidha mema”** Suratu-Nahli aya ya 125.

## Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake):

“Hakika ya upole haupatikani katika kitu isipokuwa utakipamba kile kitu, na hauondoshwi huo upole katika kitu isipokuwa kitapata aibu kitu hicho”. Na katika mapokezi mengine Amesema: “Hakika Allah ni mpole na anapenda upole na anatoa (ujira) kuulipa upole kwa asivyotoa (ujira) kwa kulipa vurugu na asivyotoa kwa vyengine.” Amepokea Muslim.





SURA

# 8

# MAZINGIRA





188

## Mafundisho ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika kuhifadhi Mazingira

Amefungamanisha Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) baina ya kumuamini Allah Mtukufu na kuhifadhi mazingira. Allah Mtukufu ndie mfalme wa wafalme ambae ameumba ulimwengu wote, na ardhi ni sehemu ya ufalme wake, na kila ambae anaishi humo ardhini atakufa na atamalizika, na Allah Mtukufu ndie atakae baki atairithi ardhi na vilivyokuwemo. Binaadamu ndie kiongozi katika ardhi na mwenye kuisimamia, basi, Itakuwaje afanye ufisadi katika ardhi? na asababishe madhara katika vitu

vya asli vya mazingira ambavyo ameviumba Allah (kama mchanga na mimea na wanyama na hewa na maji) au katika vyanzo vya asili.



Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ameweka misingi iliyokuwa madhubuti kwa ajili ya kuhifadhi mazingira, (Utakuja ubainifu wake katika somo hili) Na mwenye kufuatilia mafundisho ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) katika upande huu atapata ya kuwa imejumuisha misingi ya kielimu kwa ajili ya kuhifadhi mazingira, nayo ni:

1. Kutodhuru mazingira au kuharibu vyanzo vyake.

2. Na kutofanya israfu kwa kuangamiza vyanzo vya asili na kuviondosha vyanzo hivyo.

3. Kutoharibu mazingira na kutilia mkazo juu ya kuhifadhi usafi wake.

4. kutumia vizuri vyanzo vya kiasili vya Mazingira ambavyo vinanyanyua kule kujitosheleza katika matumizi yake na vinazidisha kupata faida ambazo zinatarajiwa.

5. Kuchukua hatua ya kuongezea maadili mazuri ya Mazingira na inakusanya hilo kuimarisha ardhi na kulima, na kupamba na kueneza kheri yake ardhi hiyo ili wafaidike kila wanaoishi kwenye ardhi hiyo.

Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): "Hakuna Muislamu ambae amepanda mti au akalima mazao wakawa wanakula ndege au binaadamu au wanyama isipokuwa kwa kufanya hivyo ataandikiwa ametoa sadaka". Amepokea Bukhari (2320) na Muslim (1188).

## Uasili upo katika kipimo kizuri daima

Allah Mtukufu ameumba vipengele vya Asili na akavijaalia vipo katika vipimo na ukamilifu wenye kuendelea na amekadiria katika ardhi vyakula na riziki zake, na yeye ndiye anaye viongoza kwa kuvumisha upepo na kunyeshesha mvua na kuisambaza katika ardhi na yale yanayozalikana kutokana na mvua katika kuotesha mimea. "…Ndiyo sanaa ya Allah, (matengenezo yake) aliyekitengeneza kila kitu…" Suratu-Naml aya ya 88. Na imekuja kwenye Qur-an Tukufu kawli ya Allah Mtukufu:

"Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kiasi (chake makhsusi)" Suratul-Qamar aya ya 49. "Na kila kitu kwake kwa kipimo (chake)." Suratul-Ra'ad aya ya 8.

## Watu wanashirikiana na vitu vinavyopatikana katika Asili

Hakika rasilimali ni zawadi kutoka kwa Allah kwa ajili ya watu wote na wala haifai kwa mtu kuzihodhi peke yake ikiwa hazitokuwa katika umiliki wake. Na amesisitiza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) wasinyimane watu maji, malisho na moto.

"Je! Mnayaona maji ambayo mnayanywa? (68) Je! Mumeyateremsha nyinyi mawinguni au Sisi ndio tunaoyateremsha? (69) Tungalitaka Tungaliyafanya ya chumvi, (makali). Basi mbona hamshukuru? (70) Je! Mnauona moto ambao mnauasha? (71) Je! Mti wake mumeuumba nyinyi au Sisi ndio tuliouumba? (72) " Suratul-Waqi'ah aya ya 68-72.

"Au Yule aliyeziumba mbingu na ardhi, na akakuteremshieni maji kutoka mawinguni (siye bora?). Na kwa hayo tukaziotesha bustani zenye kupendeza, (mashamba yenye kupendeza). Nyinyi hamna uweza wa kuiotesha miti yake hii. Je, yuko Mungu mwengine pamoja na Allah? Bali hao (makafiri) ni watu wenye kwenda upogo, (kwenda upande)." Suratu-Naml aya ya 60.






## Usiharibu Mazingira

### Usidhuru (kwa kuteleza) wala Usidhuru (kwa makusudi)

Ameweka Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kanuni kuu ya kutomdhuru mwengine, sawa ikiwa vitu visivyokua na uhai au mimea au wanyama, na wajibu wa kuondosha madhara ni sawa madhara hayo ni kwa kukusudia au bila ya kukusudia. Na kwa sababu sheria imejengeka katika kuleta maslahi na kuondosha uharibifu, kwa hivyo haifai kwa mtu kuwadhuru wengine, na vile vile haifai kudhuriwa yeye na wao.

Amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Usimdhuru mtu (bila ya kukusudia) wala usimdhuru (kwa kukusudia)." na katika mapokezi mengine: "Usimdhuru mtu (bila ya kukusudia) wala usimdhuru mtu (kwa kukusudia), mwenye kudhuru Allah Mtukufu atamdhuru, na mwenye kumletea mtu uzito na Allah Mtukufu atamtia uzito na yeye". Hadithi Sahihi kwa sharti ya Muslim, na amepokea Malik na Al-Hakim na Tabraaniy na wengineo

Na amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Imani ni daraja sabini na kitu, bora yao ni kauli ya "Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah" na ya chini yao ni kuondosha uchafu katika njia" Amepokea Bukhari "Jaami'i Sahih" (1/11) namba (9), na Muslim katika "Jami'i Sahih" (1/46) namba (35).

## Usifanye Ubadhirifu wala Israfu



Uislamu umekataza Israfu na Ubadhirifu kwa ujumla na umeamrisha kufanya tohara na usafi na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ametilia mkazo katika hadithi nyingi. Basi amekataza Israfu kwenye maji katika kila hali hata kama mtu akiwa anatawadha kwa ajili ya kuswali katika mto wenye kupita maji, kama alivyokataza kuchafua maji au kukojoa ndani ya maji hasa hasa maji yaliyotuwama, kwani maji ni msingi wa maisha na kuwa tohara kwake ni msingi wa usafi na ni kinga kutokana na maradhi. Amesema Allah Mtukufu:

"…Na tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai…"
Suratul-Anbiya aya ya 30.

"…na tunayateremsha kutoka mawinguni maji safi (kabisa)…" Suratul- Furqan aya ya 48.

"…na kuleni (vizuri) na kunyweni (vizuri). Lakini msipite kiasi tu. Hakika Yeye (Allah) hawapendi wapitao kiasi (wapindukiyao mipaka)." Suratul- A'araf aya ya a 31.

"Hakika watumiao kwa ubadhirifu ni ndugu - wa mashetani (wanamfuata Shetani). Na Shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake." Suratul- Israa aya ya 27.

## Athari chanya katika Mazingira

Hakika uelewa wa ibada katika Uislamu haupo tu katika Sala na ibada za kiroho bali imekusanya matendo na kuimarisha ardhi na muamala mzuri kwa viumbe na vilivyomo duniani kwa mujibu wa muongozo wa sheria za Allah Mtukufu. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amewahimiza Waislamu kuwa na muamala unaokubalika pamoja na yanayo wazunguka na mazingira yao, kwa hiyo kila hatua nzuri inayochukuliwa ni "Sadaka", basi kuondosha uchafu katika njia ni Sadaka na kuilima ardhi na kuiimarisha na kuiboresha pia ni Sadaka..





Hili ni neno "Muhammad" limechorwa kwa njia ya kisanii lidhihiri kama umbo la mimea (majani), ni katika kazi za Ustadhi Farid Al-'Aliy.



Hakika kutilia umuhimu usafi wa mazingira na kuipanda mimea na kuhifadhi rasili mali zake kuna athari kubwa hufaidika watu na wanyama na ndege. Na Allah Mtukufu anamlipa kila anayeimarisha vizuri ardhi na kuhifadhi rasili mali zake. Na ameashiria Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ufahamu "endelevu" katika matumizi mazuri na kuendelea kwa njia ya kudumu na akajaalia radhi za Allah Mtukufu na malipo yake ni vichocheo vya kuendeleza kufanya kheri na kutumia vizuri baina ya mtu na mazingira yake na baina ya mtu na watu. Na imepokewa katika hadithi Sahihi kwamba Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amesema:

**Ongeza thamani kwa Mazingira**

"Ikiwa kitasimama kiyama na katika mkono wa mmoja wenu ana mche basi ikiwa anaweza kuupanda (mche huo) kabla ya kusimama mpaka aupande mche huo basi afanye hivyo"
Amepokea Ahmad katika "Musnad" (5/2727) namba (13100), 95/2744) namba (13181).

"Na utafute kwa yale aliyokupa Allah - makazi mazuri ya akhera, wala usisahau sehemu yako ya dunia, na ufanye wema kama Allah alivyokufanyia, wala usitafute kufanya uflsadi katika nchi; bila shaka Allah hawapendi mafisadi."
Suratul-Qasas aya ya 77.

# Upole kwa Wanyama na kuamiliana nao Kistaarabu

## Wanyama na wadudu na ndege ni Umma kama sisi



Umma hujulikana kuwa ni mkusanyiko wa makundi ambayo yanaafikiana baina yao katika lugha na ada na desturi na wanakua wanamambo wanayo shirikiana kwayo. Na Elimu ya sasa imevumbua nidhamu ya ajabu na kanuni ngumu katika aina nyingi za viumbe kama vile sisimizi na nyuki na wegineo. Na Allah Mtukufu ameelezea kila kundi miongoni mwa makundi kuwa ni "Umma" mfano wetu, wanazo kanuni zao na lugha yao ambayo Allah Mtukufu amewawekea kuwa ni maumbile yao.

"Na hakuna mnyama katika ardhi wala ndege arukaye kwa mbawa zake mbili. ila ni umati kama nyinyi (tunadhibiti kila walifanyalo). Hatukupuza Kitabuni (mwetu) kitu chochote. Kisha watakusanywa kwa Mola wao (awalipe)"

Suratul-An'aam aya ya 38.

## Ufahamu wa nyama halali katika Uislamu




Uislamu umeharamisha kuuwa wanyama isipokuwa wale ambao ametoa ruhusa Allah Mtukufu kuchinjwa. Na kwa ruhusa kutoka kwa Allah na kwa jina la Allah Mtukufu unaweza kuchinja wale ambao amewahalalisha Allah Mtukufu kwa ajili ya kula mfano mbuzi, ngombe na ngamia vilevile kuku na ndege na wanyama ambao hawali nyama. Kwa ajili hiyo tunaona kwamba Waislamu hawachinji wanyama isipokuwa wale wanaokula majani, kwa kumtoa nguruwe, kwa mfano unaweza kula njiwa wala huwezi kula kipanga na unaweza kula mbuzi wala huwezi kula paka.





## Ufahamu wa Kistaarabu katika kichinjo halali

Na kichinjwa halali katika Uislamu hakipatikani isipokuwa kwa ufahamu wa “kuchinja kisheria” ambayo inatakiwa kutaja jina la Allah Mtukufu kwa mnyama ambae ni halali kuliwa, na iwe kwa kisu kikali au kitu kikali kinachoweza kukata mishipa miwili (mishipa miwili iliyoizunguka koo), na atamkata koo na mishipa kwa haraka itakayompa raha mnyama (kwa kufa haraka) wala haitomuadhibu na pia husaidia katika kutoka damu. Na miongoni mwa adabu za kuchinja kulokuwa halali asichinje mnyama pembezoni mwa mnyama mwengine au pahala atapomuona mwenziwe, na amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika msimamo wa kibinadamu wenye mafunzo makubwa kumwambia mtu ambae alikuwa amejiandaa kumchinja mbuzi pembezoni mwa mbuzi mwengine: “Je unataka kumuua mara nyingi?” yaani je unataka kumuua zaidi ya mara moja na yeye anamuona mwenzake anachinjwa mbele yake?

Na amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): “Hakika Allah Mtukufu amefaradhisha wema kwa kila kitu basi mtakapoua (kwenye Jihadi) basi ueni vizuri, na mtakapochinja kifanyeni uzuri kichinjo chenu na anoe mmoja wenu kisu chake na akipumzishe kichinjo chake” Amepokea Al-Hakim katika “Mustadrak” (4/231) namba (7658). (4/233) namba (7665).

Ama samaki katika Uislamu ni halali kuliwa kwa kuvuliwa na sio kwa kuchinjwa na amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kuhusu bahari na yaliyokuwemo ndani yake: “Ni tohara maji yake na halali maiti yake” Amepokea Bukhari na Muslim.







## Mafundisho ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ya kuwafanyia upole Wanyama



Allah Mtukufu ameumba wanyama na kuwafanya wengi miongoni mwao ni kwa ajili ya kutuhudumia sisi kama vile farasi na ngamia na ngombe na kondoo. Na hakika Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amekataza kuwaudhi na kuwafunga pasi na sababu kama alivyokataza kumpiga mnyama usoni au kumfanyisha kazi nzito, au kumchokesha kwa kazi au kumbebesha mizigo ambayo hana uwezo nayo au kumbebesha mizigo mizito asiyoiweza au kumuadhibu au kukata kiungo katika mwili wake naye akiwa hai au kumuua pasi na haki (kama ilivyokuwa ikijitokeza katika zama za ujinga). Mtume Muhammad (rehema na amai ziwe juu yake) alimuona ngamia amebebeshwa mizigo mizito sana naye akitoa sauti kutokana na uzito ule basi Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akataka kumpa somo mwenye ngamia yule la kuwafanyia wema wanyama na kuwafanyia upole, akamwambia: "Hakika ngamia wako amenishtakia mimi kwamba wewe unambebesha mizigo asiyoiweza" Amepokea Abu Dawd katika "Sunan" (2/328) namba (2549) na Ahmad katika "Musnad" (1/446) namba (1779).

## Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anatoa somo la vitendo katika kuwafanyia upole wanyama

Amepokea Sahaba Abdullahi bin Masoud (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba alikuwa yeye na kundi la Masahaba pamoja na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika safari, na walipopita kwenye mti, mmoja wao alivichukua vifaranga viwili vya ndege anayefanana na njiwa anayeitwa "Humrah", yule ndege akaanza kulia (kama kwamba anawaomba watoto wake) basi kutokana na kilio cha yule ndege kwa wanawe Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akamuarisha avirejeshe vifaranga kwa mama yao"

Amepokea Abuu Dawd katika "Sunan" (2/8) namba (2675), (4/539) namba (5268).

## Kuwafanyia wema wanyama ni jambo la Kistaarabu ambalo ndani yake kuna malipo kutoka kwa Allah Mtukufu

Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): "Wakati mtu alikuwa anatembea njiani kiu ilimzidi, alikuta kisima akashuka katika kisima kile na akanywa maji kisha alipotoka akamuona mbwa anahema kutokana na kiu, basi alisema yule mtu: "kwa hakika mbwa huyu amepatwa na kiu mfano wa kiu niliyoipata mimi," basi alishuka katika kisima na alijaza katika kiatu chake maji na akanywa mbwa maji yale na akamshukuru Mungu na akasamehewa dhambi zake mtu huyo" Amepokea Bukhari namba (2365) na Muslim namba (2242).

Na pia Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ametaja kisa cha mwanamke ambae ameingia motoni kwa sababu amemfunga paka mpaka akafa, basi yeye hakumpa chakula wala maji alipomfunga, wala hakumuacha akala wadudu wa ardhini."



(Muhammad ni Mtume wa Allah – kwa umbo la jani) Picha ni kazi ya mchoraji Mahmoud Al-Haji Yunus.



SURA

# 9

# MUUJIZA

“Na haiwezekani kuwa hii Qur-ani imetungwa, haitokani na Allah kama mnavyojidai). Bali (imetokana na Allah), inayasadikisha yaliyo mbele yake, na ni maelezo ya vitabu (vilivyopita). Haina shaka kuwa imetoka kwa Mola wa walimwengu (wote). (37) Je! Ndiyo wanasema ameitunga? Sema: "Hebu (tungeni na nyiye) mlete sura moja mfano wake na waiteni muwezao (kuwapata waje)- isipokuwa Allah- (wa kuwasaidieni) kama nyinyi mnasema kweli (kuwa haya ameyazua Muhammad)." (38)

Suratu-Yunus aya ya 37- 38



## Qur-ani ni Muujiza ambao Allah Mtukufu amemuunga mkono Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake)



Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) amekuja na ujumbe wa mbinguni kutoka kwa Mola wa watu kwa watu wote. Ujumbe huo ulikuwa ni aya zenye maneno ya kiarabu yalio wazi na ya fasaha ambayo Allah Mtukufu aliteremsha kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kupitia Jibril (amani iwe juu yake) ili kiwe kitabu cha milele, nacho si chenginye ni Qur-ani Tukufu. Wito wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ulikuwa wa Kilimwengu, hivyo alituma barua na wajumbe kwa Wafalme na wakuu wa dola na Wafalme wa nje ya Bara Arabu, kama vile Misri, Ethiopia, Fursi na Roma, akiwalingania kumuamini Allah Mtukufu na kuuamini Ujumbe wake kwa wanadamu. Wanadamu hao wanajumuisha mataifa na makabila ambayo huzungumza lugha tofauti na wanarudi katika Asili na Tamaduni na Ustaarabu mbali mbali.

Basi Je, nirahisi kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kuwakinaisha wasiokuwa Waarabu kuhusu Ujumbe wa Allah Mtukufu uliokuja kwa lugha ya kiarabu iliyonyooka?

> “Hawaizingatii nini hii Qur-ani? Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Allah bila shaka wangalikuta ndani yake khitilafu nyingi” Suratu-Nisaai aya ya 82.

## Kwa nini Qur-ani Tukufu inazingatiwa ni Muujiza wa milele?

Qur-ani tukufu ni Muujiza wa milele kwa sababu ndicho kitabu pekee cha mbinguni kilicho kusanya maneno ya Allah Mtukufu kwa maelezo ya Allah Mtukufu bila ya uundaji au usemi wa kibinadamu, haikuchanganyika na maneno ya binadamu, wala haikupotoshwa au kufupishwa, au kuongezwa na yeyote kati ya watu.





Qur-ani tukufu ni kitabu ambacho watu wanaweza kukisoma, kukigusa na kupokezana kizazi baada ya kizazi, ndani yake yamo maneno ya Allah Mtukufu na muongozo wake kwa watu wote.

Basi hakuna mtunzi wa Qur-ani Tukufu katika Wanaadamu kwa sababu ni Wahyi kutoka kwa Allah Mtukufu ambao Waislamu waliupokea kutoka kwenye kinywa cha Nabii Muhammad Mtume wa Allah Mtukufu katika kipindi cha miaka ishirini na tatu, wakaihifadhi na kuiandika kama ilivyo bila nyongeza wala kupunguza .

> “Sema "Hata wakijikusanya watu (wote) na majini ili kuleta mfano wa hii Qur-ani basi hawangaliweza kuleta mfano wake; hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao” Suratul-Israa aya ya 88.

## Muujiza Wa Kuhifadhiwa Qur-ani

Ijapokuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliwaweka waandishi wa Wahyi kama Sahaba Ali bin Abi Talib, (radhi za Allah ziwe juu yake) na Sahaba Ubay bin Ka'ab (radhi za Allah ziwe juu yake) na Sahaba Zaid bin Thabit (radhi za Allah ziwe juu yake) lakini Qur-ani haikukusanywa katika kitabu kimoja mpaka baada ya kufariki kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika zama za Khalifa Abu Bakar As-Siddiq (radhi za Allah ziwe juu yake) akihofia isije ikapotea baada ya kuuwawa kwa idadi ya waliohifadhi Qur-ani katika vita vya Al-Yamamah. Na baada ya kupanuka kwa dola ya Kislamu na kuingia kwa watu wengi wasiokuwa Waarabu katika Uislamu, Khalifa wa tatu Othmani bin Affan (radhi za Allah ziwe juu yake) aliamua kutoa nakala kadhaa za Misahafu ili aisambaze katika miji na akawatuma wasomaji katika sehemu hizo ili kuwafundisha watu maneno ya Allah Mtukufu.



Maandishi haya yaliyopambwa ni sehemu ya aya ya 60 ya Suratu-Ghafir katika Qur-ani Tukufu “Na Mola wenu anasema: "Niombeni nitakujibuni. Kwa hakika wale wajivunao kufanya ibada yangu, bila shaka wataingia Jahanamu, wadhalilike."

Maandishi ya Qur-ani yaliyopo kwa Waislamu wanalingana na yale yaliyoteremshwa kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kabla ya zaidi ya karne 14 zilizopita, bila ya shaka hata kidogo kutokana na mapokezi yake ya "Mutawatir" yaliyopokewa kutoka kwa kundi kubwa la Waliohifadhi kuwapa wengine na kupokewa na kizazi hadi kizazi bila kukatika katika masimulizi au tofauti au kugongana kati ya wasimuliaji. Hii ina maana kwamba haiwezekani kubadili au kutofautiana au kuacha neno au aya yoyote katika Qur-ani tukufu (iliyo mikononi mwetu sasa) na ile ambayo Allah Mtukufu aliyomshushia Mtume wake (rehema na amani ziwe juu yake).



### Kutofautisha Qur-an na Hadithi ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na tofauti kati ya Qur-ani na Sunna.



Hakika kauli za Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na mafundisho yake hayakuingiliana na Qur-ani Tukufu inayojumuisha maneno ya Allah Mtukufu, bila ya nyongeza, au maelezo au tafsiri ya mwanadamu. Na zilikusanywa kauli za Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na mafundisho yake katika kile kiitwacho "Hadithi za Mtume" au "Sunna ya maneno" pamoja na hayo yalikusanywa matendo yake ambayo walitusimulia Masahaba kama mfano utekelezaji wake wa Sala na muundo wake, nguzo za Hija na matendo yake yanayoitwa "Sunna za vitendo". Ama kunyamaza kwake Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika kitendo cha mtu au kukubali kwake matendo ya mtu Wanavyuoni wameziita "Sunna za Ikrari".




maneno ya Mtume na matendo na takriri zake kwa jina la "Sunna" na kitabu kilichokusanya maneno ya Allah peke yake kinaitwa Quran Tukufu.

## Ulinganisho baina ya Vitabu vya hadithi za Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na vitabu vya dini nyenginezo

Wapo watafiti wanaoamini kuwa vitabu vya hadithi za Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ni sawa na vitabu vitakatifu vya dini nyenginezo, kwa sababu vyote viwili vinatokana na maneno ya kibinadamu, basi vitabu vitakatifu kimsingi vinatokana na maandishi ya waliyotunga maandiko hayo ya kidini kwa maneno yao na Ibara zao na maelezo yao.

Kwa mfano, Injili nne za kanisa zinazojulikana kwa agano jipya zinahusishwa kwa waandishi wao Mathayo, Marko, Luka na Yohana. Ama agano la kale liliandikwa katika kipindi kati ya mwaka 1400 hadi 1800 AD na imeandikwa na waandishi takriban 40.

Alikuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akitofautisha kati ya maneno ya Allah Mtukufu yaliyoteremshwa kwake na maneno yake. Izingatiwe kuwa mzungumzaji katika Qur-ani ni Allah Mtukufu , kwa hivyo lugha ya Qur-ani ina sifa ya matumizi ya mara kwa mara ya kiwakilishi “Sisi” au “Hakika sisi” pamoja na kitenzi “Sema” ambacho kinamaanisha: waambie, ewe Muhammad.

## Muujiza wa kuchunga Hukmu za kusoma Qur-ani Tukufu



Usomaji wa Qur-ani unafungamanishwa na neno “Tajweed” ambayo ni sayansi inayochunguza jinsi ya kusoma Qur-ani Tukufu na kuboresha matamshi ya herufi na maneno yake kwa njia sahihi na thabiti. Ingawa Waislamu walikuwa na bidii ya kuisoma Qur-ani kama walivyojifundisha kutoka kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) lakini uandishi wa elimu ya Tajweed ulianza mwaka wa 154 Hijiria na ukaendelea hadi ikawa elimu inayojitegemea

katika karne ya nne Hijiria Kwa hivyo, elimu ya Tajweed imetangulia zaidi ya miaka 1000 kuliko elimu ya sauti na elimu ya mazungumzo katika lugha sita za Ulaya, ambazo zilitoka au ziliathiriwa na kilatini.

Elimu ya Tajweed inatofautishwa kwa kuunganishwa kwa riwaya zake katika zama tafauti kutoka kwa Jibril (amani iwe juu yake) ambaye aliteremsha Qur-ani kwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na kutoka kwake na kwenda kwa Masahaba zake na kisha kwa wapokezi waaminifu waliotoka kuwafundisha watu Qur-ani katika pande zote za dunia. Na hili liliendelea kutoka kizazi hadi kizazi mpaka leo, kwa hivyo utaona miongoni mwa wasomaji wa zama zetu hizi mwenye "Sanadi" aliyopokea kutoka kwa Wanachuoni waliotangulia. Sanadi au "Ijaza" zinashuhudia kwamba msomaji amekuwa na ujuzi wa kusoma Qur-ani kwa mujibu wa riwaya yenye kuaminika, na ameruhusiwa kuisoma na kuifundisha kwa watu

## "Kiarabu" ni lugha ya Qur-ani Tukufu, amabayo ni tajiri katika misamiati na maana zake

**Tajweed ni elimu inayotofautisha Qur-ani**

Qur-ani Tukufu imeteremshwa kwa lugha ya Kiarabu fasaha, na Waislamu wa jinsia zote na asili zao na lugha zao bado wanaendelea kujifunza na kuisoma Qur-ani Tukufu kwa ufasaha wa lugha ya Kiarabu ambayo imeteremshwa hadi leo na mpaka Allah Mtukufu achukue ardhi na vilivyo juu yake. Wasomi wengi wa lugha ya Kiarabu wanaamini kuwa lugha ya Kiarabu ni bora kuliko lugha nyinginezo kutokana na wingi wa misamiati yake, na maana zake za ndani, na ukunjufu wa sarufi zake, na uzuri wa maneno yake, na sauti yake ya kimziki.

Hakika mnyambuliko wa neno moja katika lugha ya Kiarabu wakati mwingine unaweza kufikia mpaka mia moja, na kila ongezeko katika mjengeko wa neno kwa herufi au mfano wa hayo inaongezeka maana. Wataalamu wa lugha wanakadiria kwamba misamiati ya lugha ya Kiarabu pamoja na minyambuliko yake yanafikia maneno milioni sita, idadi hii ni kubwa zaidi kuliko idadi ya misamiati ya lugha kuu za dunia na zilizoenea zaidi.

Lugha ya Kiarabu ina herufi ambazo hazipo katika lugha nyingine yoyote, kama vile “dhwadi”. Herufi za lugha ya Kiarabu na sanaa ya uandishi wake ni chanzo cha msukumo kwa wengi wa waandishi na wanasanaa na urembo ambao waliwasilisha michoro mizuri zaidi ya kisanii katika historia.



## UKWELI WA KISAYANSI NDANI YA QUR-AN TUKUFU



### Nadharia ya mlipuko mkubwa na uumbwaji wa ulimwengu



Katika zama za Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) hakuna aliyejuwa chochote kuhusu kuanza kwa ulimwengu, au nyendo za sayari, au ikiwa dunia ni duwara au tambarare. Waislamu wanaamini kwamba Allah Mtukufu ndiye muumba wa ulimwengu, na yeye peke yake ndiye anaejuwa jinsi ya ardhi ilivyoumbwa. Na Sayansi ya leo imeelezea kuumbwa kwa ulimwengu kulikuja kama matokeo ya mlipuko mkubwa. Ulimwengu wote ulikuwa pande moja ukatokezea mlipuko mkubwa ulimwenguni ambao ulisababisha kuundwa kwa Nyota, Sayari, na Galaksi za ulimwengu ambazo zina mawingu ya Volkana yenye asili ya gesi.

### Kupanuka kwa Ulimwengu

Mnamo mwaka wa 1925 mtaalamu wa nyota wa Marekani Edwin Hubble aliwasilisha ushahidi wa kisanyansi unaonesha kwamba nyota zinatembea mbali kutoka kwa kila moja, jambo ambalo linaonesha Galaksi na ulimwengu mzima uko katika hali ya kutanuka daima. Pia alitoa uthibitisho wa kisayansi kwamba Sayari husogea kwa namna ya duaradufu

kuzunguka jua na kwamba zinazunguka kwa wakati mmoja kwenye mhimili wake. Wana Sayansi wa mambo ya Asili huthibitisha nadharia zao kupitia uchunguzi na matokeo ya miongo kadhaa iliopita. Na mtu anaweza kushangazwa na mfanano uliopo kati ya uvumbuzi wa kisayansi wa kisasa na yale yaliyotajwa katika Qur-ani Tukufu ambayo Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliyasema zaidi ya karne kumi na nne zilizopita na bado yamehifadhiwa hadi sasa. Qur-ani Tukufu ilitaja kwa namna ya kustaajabisha kisa cha uumbaji wa ulimwengu, na mwendo wa jua na mwezi, na mzunguko wa dunia, na kupatikana mchana na usiku. (Angalia aya katika ukurasa unaofuata).

“Je! hawakuona wale waliokufuru ya kwamba mbingu na ardhi vilikuwa vimeambatana, kisha tukaviambua, (tukavipambanua): Na tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai. Basi jee hawaamini?”

Suratul-Anbiyaa aya ya 30.

“Kisha akazielekea mbingu na zilikuwa moshi, basi, akaziambia (mbingu) na ardhi: "Njooni, mkipenda msipende.Vyote viwili vikasema: "Tumekuja, bali ya kuwa wenye utiifu."

Suratu-Saaffat aya ya 11.



“Na yeye ndiye aliyeumba usiku na mchana . na jua na mwezi; vyote vinaogelea katika duara (zao).”

Suratul-Anbiyaa aya ya 33

“Na mbingu Tumezifanya kwa kudra (yetu); na hakika Sisi ndio wenye uweza (wa kila kitu). (47) Na ardhi Tumeitandaza; basi Watandazaji Wazuri walioje Sisi! ” (48)

Suratu-Dhaariyaat aya ya 47-48.



## Kuumbwa binaadamu na kukua kwake katika fuko la Uzazi

Qur-ani Tukufu imetaja mambo ya ajabu na ufafanuzi wa kina kuhusu kuumbwa kwa binaadamu na kukua kwake tumboni, na haipingiki kuwa maelezo hayo hayakuwa yakijulikana kabla ya miaka 1400, na elimu ya mtoto tumboni haikuwepo wakati huo kwa mfano wa hayo, sehemu ya aya ya 6 ya Suratu-Zumar inayozungumzia kuwepo kwa viza vitatu katika tumbo la mama:

> "...Hukuumbeni matumboni mwa mama zenu- umbo baada ya umbo - katika viza vitatu. Huyu ndiye Allah Mola wenu: Ufalme ni wake; hakuna aabudiwaye kwa haki ila yeye. Basi nyinyi mnageuzwa wapi?" Suratu-Zumar aya ya 6.

Na inashangaza kwamba Sayansi ya kisasa imegundua kuwepo kwa tabaka tatu zinazounda mbawa za giza zinazozunguka Fetusi katika Uterasi na kuunda mfuko wa Fetasi wenye nguvu ili kuilinda. Tabaka hizi tatu ni ukuta wa tumbo, ukuta wa Uterasi, na Membrane ya Placenta







**Na imekuja katika Qur-ani Tukufu wasifu wa kimiujiza juu ya kuumbwa kwa binaadamu na kukua kwa kichanga , Amesema Allah Mtukufu**




"Na kwa yakini tulimuumba mwanadamu kwa udongo ulio safi. (12) Kisha tukamuumba kwa tone la manii, (mbegu ya uzazi) lililowekwa katika makao yaliyohifadhika. (13) Kisha tukalifanya tone hilo kuwa pande la damu, na tukalifanya pande la damu hilo kuwa pande la nyama, kisha tukalifanya pande la nyama hilo kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama, kisha tukamfanya kiumbe kingine. Basi ametukuka Allah Mbora wa waumbaji. (14)"

Suratul-Muminun aya ya 12- 14

Na jambo la kushangaza kuwa ugunduzi wa Sayansi ya kisasa umekuja sambamba na kukua kwa kichanga tumboni kama yalivyotajwa katika aya hii, na hii inatujulisha wazi kwamba aliezungumzia haya ima atakuwa ndie aliyeumba hicho kichanga tumboni na akapanga ukuaji wake au ambae aliona kwa macho kuumbwa kwa hicho kichanga tumboni na kukua kwake kisha akatoa wasifu wake kwetu sisi. Na ilivyokuwa hali ya pili haiwezekani kielimu kutokezea katika zama za Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) basi aya hii inajuulisha kwamba maneno haya ni ya kimiujiza ya Allah Mtukufu ambaye ndie amemuumba kichanga (binaadamu) na akaeleza namna ya ukuaji na haiwezakani kwa mtu yeyote kujua mambo hayo kiundani kabisa isipokuwa kwa kutumia vifaa vya kisasa vilivyowawezesha wanasayansi kujua ukuaji wa mtoto tumboni.

Na miongoni mwa mambo ya kweli na ya ajabu yaliyotajwa katika Qur-ani Tukufu kuelezewa mifupa kwamba inaundika kabla ya nyama.

Na kutajwa kiungo cha hisia ya usikivu kabla ya hisia ya uoni, na hiki ndicho walichokigundua wasomi wakileo, kwani mifupa ya kichanga inaundwa kabla ya nyama zake, na hisia ya usikivu inakuwepo kabla ya hisia ya uoni. (angalia aya zifuatazo):

"...Basi ametukuka Allah Mbora wa waumbaji." Suratul-Muuminun aya ya 14.

"Kisha Akamtengeneza na Akampulizia roho Yake, na Akakupeni masikio na macho na nyoyo; ni kidogo tu shukrani yenu" Suratu-Sajda aya ya 9.

" Hakika s1s1 tumemuongoa, (tumembainishia) njia (zote mbili hizi; kuwa hii ndiyo ya kheri na hii ndiyo ya shari). Basi (mwenyewe tena) atakuwa mwenye shukurani au awe mwenye kukufuru, (kukanusha)." Suratul-Insaan aya ya 3.

"Na Yeye ndiye aliyekuumbieni masikio na macho na nyoyo; ni machache mnayoyashukuru" Suratul-Muuminun aya ya 78.

## Viashirio vya Kisayansi kwa baadhi ya nambari katika Qur-an Tukufu

309 Qur-ani Tukufu imetaja kisa cha watu wa pangoni, nao ni kundi la vijana walio muamini Allah Mtukufu, ambao walikimbia kwa ajili ya dini yao, na kukimbilia kwenye pango wakalala humo, basi Allah Mtukufu akawafisha kwa muda wa karne tatu takriban kisha akawafufua. Na jambo la Muujiza katika kisa hiki ni kwamba aya ya 25 katika Suratul-Kahfi imetaja muda waliokaa vijana hao katika pango lakini kwa mtindo wa kimiujiza:

"Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu, na wakazidisha (miaka) tisa" Suratul-Kahfi aya ya 25

Wakati Qur-ani Tukufu inashuka kalenda ya jua (Gregorian) haikuwa ikijulikana kwa Waarabu, na kalenda kuu iliyoenea ni kalenda ya mwezi ambayo kalenda hiyo kwa mwaka inapunguwa ukilinganisha na mwaka wa jua kwa siku 11 kwa hivyo miaka 300 ya miaka ya jua inawiyana na miaka 309 ya miaka ya mwezi mwandamo na huwenda ikawa ndio makusudio ya aya "miaka 300 na wakazidisha siku tisa"

## Matukio ya baadae na ishara za kisayansi katika Qur-an Tukufu

" Alif Lam Mym. (1) Warumi wameshindwa (2) Katika nchi iliyo karibu (na nchi ya Bara Arabu. Nayo ni Shamu); nao baada ya kushindwa kwao, watashinda (3) Katika miaka michache; Amri ni ya Allah kabla (yake) na baada (yake); na siku hiyo Waislamu watafurahi. (4) Kwa nusura ya Allah (atakayowapa wao. Nayo ni kuwashinda Makureshi siku hiyo). (Allah) humnusuru Amtakaye; naye ni Mwenye nguvu (na) Mwenye rehema. (5) " Suratu-Ruum aya ya 1-5.



Qur-ani Tukufu imekusanya aya nyingi zinazozungumzia kwa namna ya kimiujiza kuhusu mambo yatakayotokea baadae, aya za mwanzo za Suratul-Ruum zimezungumzia kuhusu kushindwa kwa utawala wa Roma katika vita vyake dhidi ya utawala wa Fursi, wakati ambao ulikuwa ni vigumu kwa Waarabu wakiwa ni makabila duni kuweza kufahamu ukuaji wa migogoro itakayotokea baina Madola mawili yenye nguvu.



Uhalisia wa kitarekhe unasema ufalme wa ki-Fursi uliwashinda Roma –Bizintiya – katika vita ambavyo vimepatikana Palestina na wakaitawala Qudsi, na Waroma wakarudisha ushindi wao kutoka kwa Waroma kwa muda mchache baadae katika vita vilivyo piganwa karibu na Naynawa huko Iraq.

Neno "Adna" kwa Kiarabu lina maana ya karibu, na pia lina maana ya chini, na vilipigwana vita katika sehemu ambayo ni ya karibu na mji wa Shamu kwenye Bara Arabu ndani yake kuna bahari inayoitwa bahari ya MAITI, ambayo inatazama Palestina, nayo ni katika miji ardhi yake ipo chini sana ulimwenguni (mita 422 takribani usawa wa bahari)

---

Kwa maelezo zaidi kuhusu miujiza ya kisayansi katika Qur-ani tizama tovuti ya chombo cha kimataifa cha Miujiza ya Sayansi katika Qur-an na Sunna, www.eajaz.org.

### Mazingatio

• Idadi ya kurasa za Qur-ani Tukufu = 604 kwa makisio ya machapisho mengi. Idadi ya Sura za Qur-ani Tukufu = 144. Idadi ya aya za Qur-ani Tukufu = 6348. Sura refu katika Qur-ani Tukufu ni Suratul-Baqara na idadi ya aya zake = 286. Sura fupi katika Qur-ani Tukufu ni Suratul-Kawthar na idada ya aya zake ni = 3.

> "Na hakika wewe unafundishwa Qur-ani inayotokana kwa (Allah) Mwenye hikima, Mjuzi"
> Suratu-Naml aya ya 6.

Picha hii imechukuliwa katika eneo la tukio la watu wa Pangoni, ambalo limegunduliwa katika eneo la mashariki mwa Jodan - Abu 'Alanda -, na inadhaniwa kuwa ndilo pango ambalo limetajwa katika Qur-ani Tukufu katika Suratul-Kahfi na inaonekana sehemu ya kuingilia Pangoni (baada ya kuwekwa mlango) na ndani yake yapo Makaburi ya vijana ambao wametajwa katika Qur-ani tukufu kuwa wamekaa humo kwa miaka 309.



SURA

10

# HADITHI ZA MTUME

## (rehema na amani ziwe juu yake)



“Amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): “Muumini kwa Muumini mwenzie ni kama jengo, wanashikamana kwa pamoja, na akaviunganisha vidole vyake.”Amepokea

Bukhari (481) na Muslim (2585).




Kutoka kwa Anas bin Malik (radhi za Allah ziwe juu yake) amesema: “Amechora Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) mstari na akasema “huyu ni binadamu” na akachora pembeni yake mstari na akasema “haya ni mauti yake” na akachora mchoro mwingine upo mbali na ule uliopita na akasema: ”haya ndio matarajio” akiwa katika hali hiyo ya matarajio, mara yanamjia mauti” Amepokea Bukhari (6417) na Muslim (1671)


212

## HADITHI ZA MTUME

Qur-ani Tukufu imesifia maneno ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kuwa ni Wahyi anaoshushiwa Mtume basi hazungumzi kitu kilicho batili au chenye kupinga maneno ya Allah Mtukufu.

> "Naapa kwa nyota zinapoanguka. (zinapokuchwa) (1) Kwamba mtu wenu (huyu Nabii Muhammad) hakupotea (kwa ujinga) wala hakukosa, (na hali ya kuwa anajua); (2) Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake). (3) Hayakuwa haya (anayosema) ila ni Wahyi (ufunuo), uliofunuliwa (kwake)" (4) Suratu-Najmi aya ya 1-4.

Wanavyuoni wa hadithi wamekusanya maneno ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na mafundisho yake na wakayahakiki na wakathibitisha wapokezi wake "Sanad" na katika maelezo yake (Matini) kisha wakazipanga kwa mfumo uliokusanya mambo ya dini kama vile Imani, na Tohara, na Sala, na mfumo wa mambo ya dunia kama miamala ya kijamii na kibiashara na mengineo.

Katoka kwa Abdullah bin Abbas (radhi za Allah ziwe juu yake), Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema kumwambia mtu hali ya kumpa mawaidha': "Patiliza mambo matano kabla ya matano: ujana wako kabla ya uzee wako, na afya yako kabla ya maradhi yako, na utajiri wako kabla ya umaskini wako, na wakati wako kabla ya kushugulika kwako, na uhai wako kabla ya kufa kwako." Amepokea Al-Hakim kwenye "Mustadrak" namba (7847) 4/341, akasema Hii hadithi Sahihi kwa sharti ya Bukhari na Muslim na wao hawakuipokea na akasahihisha Albani katika 'Sahihul-Jaami'i" namba (1077) na katika "Sahih Tarhib wa Tarhibu" namba (3355).

Kutoka kwa Anas bin Malik (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba Mtume (rehema na amani ziwe yake) amesema: "Hatoamini mmoja wenu mpaka ampendelee ndugu yake lile analolipenda ndani ya nafsi yake" Amepokea Bukhari (13) na Muslim (45).

Kutoka kwa Abdallah bin Amr bin Al-'Aas (radhi za Allah ziwe juu yake) amesema: "Hakuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) mchafu wa tabia, wala hakuwafanyia watu ubaya, na alikua akisema: "Mbora wenu ni yule mwenye tabia njema". Amepokea Bukhari "Jaami'i Sahih" (4/189) namba (3559), (5/28) namba (3759), (8/12) namba (6029), (8/13) namba (6035) na Muslim katika "Jaami'i Sahih" (7/78) namba (2321).

Kutoka kwa Abdallah bin Abas (radhi za Allah ziwe juu yao), amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Neema mbili wanahadaika nazo watu wengi (nazo ni) Siha na Faragha" Amepokea Bukhari (6049)

Kutoka kwa Abdallah bin Masoud (radhi za Allah ziwe juu yake), Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "hapana kuhusudiana isipokuwa katika mambo mawili: Mtu ambaye Allah Mtukufu amempa elimu na akaitumia kuhukumia vizuri na kuifundisha, na mtu ambaye Allah Mtukufu amempa mali na akaitumia katika mambo ya haki." Amepokea Bukhari (4737) na Muslim (815).

Kutoka kwa Anas bin Malik amesema: amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) "Fanyeni wepesi wala msifanye uzito, na bashirianeni mema wala msifukuzane katika mema." Amepokea Bukhari (4867) na Muslim (1734).

Kutoka kwa Hakiim bin Hizaam (radhi za Allah ziwe juu yake ) kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Wanaouziana wana hiyari ikiwa hawajatengana, au amesema : mpaka watengane, basi wakiwa wakweli katika kuuziana na wakawekeana uwazi (kile wanachouziana), basi watabarikiwa katika mauziano yao, na ikiwa watafichana na wakadanganyana (katika mauziano yao), basi huenda wapate faida, na wataikosa baraka ya walicho uziana, kiapo cha uongo kinafanya bidhaa iuzike na kinaondoa baraka katika kipato.

Amepokea Bukhari (2079)

Kutoka kwa Abu Musa Al-Ash-ary (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Kila Muislamu analazimika kutoa sadaka, (Masahaba) wakasema! "Unaonaje ikiwa hakupata?" akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake)": "Afanye kazi kwa mikono yake ili ajinufaishe yeye na atoe sadaka, pakasemwa: "Unaonaje ikiwa hawezi je? Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema: "Amsaidie mwenye haja" akasema (mpokezi) akaambiwa Mtume: "Unaonaje ikiwa hawezi je?" akasema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Aamrishe mema au mambo ya kheri" akasema (Sahaba): "Unaonaje ikiwa hakufanya? Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akasema: "Ajizuwie na shari kwani hilo ni Sadaka"

Amepokea Bukhari (4562) na Muslim (1008).

Kutoka kwa Abu Huraira (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Atakapo kufa mwanadamu amali zake zinakatika isipokuwa mambo matatu, sadaka inayoendelea , au elimu yenye manufaa kwa watu , au mtoto mwema anaemuombea dua."

Amepokea Muslim ( 1635).

Kutoka kwa Abu Dharri Al-Ghaffary (radhi za Allah ziwe juu yake ), amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Muogope Allah Mtukufu popote ulipo na fuwatisha ovu kwa (kufanya) jema, litafuta ovu, na ishi na watu kwa tabia njema ". Amepokea Tirmidhiy (1987)

Kutoka kwa Nuwas bin Sam'aan (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba amemuuliza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kuhusu wema na ubaya, Akasema: "Wema ni tabia njema, na ubaya ni ule unaokupa shaka katika kifua chako, na ukahofia kuonekana na watu."
Amepokea Muslim (4760).

Kutoka kwa Abu Huraira (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Kuwa na nguvu sio kwa kupigana mieleka, bali mwenye nguvu ni yule mwenye kuidhibiti nafsi yake wakati wa hasira." Amepokea Bukhari (5785) na Muslim (4853).

Kutoka kwa Abu Huraira (radhi za Allah ziwe juu yake) kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: "Yule anaemuamini Allah na siku ya mwisho basi asimuudhi jirani yake, na yule anaemuamini Allah na siku ya mwisho basi amkirimu mgeni wake, na yule anaemumini Allah na siku ya mwisho basi aseme yaliyomema au anyamaze."
Amepokea Bukhari (6018) na Muslim (660).

## UKWELI KUHUSU MATIBABU NA LISHE



### Kinga ni bora kuliko Tiba.

Pamoja ya kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) hakuwa ni daktari, lakini hadithi zake zimefungamana sana na yanayohusiana na lishe pamoja na ada za afya na lishe yanayojulikana kwa sasa kuwa ni Tiba za miti shamba na tiba mbadala. Hakika hadithi hizi hujulikana kwa Waislamu kuwa "Tiba za Mtume". Na alikua Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akiwahimiza Masahaba zake kuwa na kiasi katika vyakula na vinywaji, na wajiepushe na unene, na wachunge shughuli zao (wachunge mfumo wa maisha kiafya kulingana na ufahamu wa kisasa)

Ameashiria Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika matukio tofauti kuwa tumbo ni nyumba ya ugonjwa, na alikuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) akichukia kujaza tumbo kwa chakula, na alikuwa akipendelea mtu ale mlo mdogo kwa siku, ili kuupa mwili unachohitaji kama nguvu na uchangamfu.

Amesema Mtume (rehema na amani zwe juu yake): "Hajajaza mwanadamu katika chombo kitu kibaya kuliko kujaza tumbo lake, kinamtosheleza binadamu chakula kitachoweza kusimamisha mgongo wake, na ikiwa hapana budi ya kula, basi ale kwa kuligawa tumbo lake mara tatu, thuluthi moja kwa ajili ya chakula, na thuluthi nyengine iwe kwa ajili ya vinywaji, thuluthi nyingine kwa ajili ya kupumua".

Amepokea Al-Hakim katika "Mustadrak" (4/121) Namba (7232), (4/331) namba (8040) na Tirmidhy katika "Jaami'i" (4/188) namba (2380) na Ibnu Maajah katika "Sunan" (4/448) namba (3349) na Ahmad katika "Musnad" (7/3819) namba (17459)

**Tumbo lako ni chombo kibaya unachokijaza**

1/3 Chakula
\+
1/3 Kinywaji
\+
1/3 Nafasi ya Pumzi



### Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) anakula Shairi na anausia kuitumia

Zinaashiria tafiti za zama hizi kuwepo kwa faida nyingi za kiafya katika Shairi ambayo inahisabiwa kuwa ni chakula kamili chenye mkusanyiko wa: vimeng'enya (Enzymes), na asidi (Acid), na vitamin (Vitamins) na maadini kama chuma (Iron), na fosforasi (Phosphorus), na Kalsiam (Calcium) na Patasiamu (Potassium) na (Chromium).

Shairi inasaidia kufanya kazi mwilini katika kupunguza kiwango cha lehemu (cholesterol) katika damu na inaweka vizuri kiwango cha sukari kwenye damu na inazuwia kuganda damu na hayo ni kwa kule kukusanya ndani yake nyuzinyuzi (Fiber) zinazokubali kuyayuka katika maji kama ambavyo inayo nyuzinyuzi zisizokubali kuyayuka (zipo kwenye pumba za shairi) zenye athari kubwa katika kuchangamsha utendaji wa utumbo mdogo na kupunguza nafasi ya kudhihiri uvimbe na kubakia visababisha vya Saratani.

Na Shairi imepunguza uwezekano wa kupata maradhi ya kutetemeka mwili na shida ya kupata usingizi kwa kukusanya madini ya "Melatonin" nayo ni mada ya homoni (hormones) inayotoka kwenye maeneo ya ubongo na inapunguwa utokaji wake kila umri ukizidi. Vile vile Shairi imekusanya ndani yake Vitamini A na E, nazo ni "Antioxiodants" inayolinda mwili kutokana na Radikali huru ambazo zinaharibu utando wa seli na kusababisha Saratani.

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anakula mkate uliotengenezwa kwa unga wa Shairi na pumba zake mara kwa mara na alikuwa akitumia zaidi mkate huo kuliko mkate wa unga wa ngano. Na amepokea Bukhari kutoka kwa Salamah bin Diinaar kwamba Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa anakula Shairi isiyokobolewa na walikuwa wanaisaga na kuisafisha.



## "Talbina" ni mapishi ya Kinabii kwa kila mwenye huzuni

Na miongoni mwa Miujiza na Sayansi katika maneno ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ni kwamba alikuwa akiusia chakula kiitwacho "Talbina" kwa ajili ya kupunguza huzuni na msongo wa mawazo kwa mgonjwa au wafiwa. Na Talbina ni Uji wa unga wa Shairi na pumba zake. Amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake):

"Talbina inaliwaza moyo wa mgonjwa na inaondoa baadhi ya huzuni" Amepokea Bukhari (5365) na Muslim (2316).

Zimegundua tafiti za tiba ya kileo kuwa upungufu wa kiwango cha 'Neurotransmitter" katika ubongo wenye jukumu la kuweka sawa hali (mood) ya mwanaadamu husababisha msongo wa mawazo.



Na dawa za kupambana na msongo wa mawazo zinafanya kazi ya kuzidisha kiwango cha (Neurotransmitter) au kuzirejesha katika hali yake ya kawaida ili kuondokana na msongo wa mawazo.



Na miongoni mwa vitu vyenye uwezo wa kusaidia kusambaza ujasiri katika ambavyo vinaathiri hali ya mtu (mood) ni "Sirotanin" na "Norepinefrin" na "Dopamine". Wataalamu wamegundua kuwa Shairi hufanya kazi hiyo ya kuathiri "Sirotanin" kwa kiwango kikubwa ambacho kinapunguza hali ya msongo wa mawazo. Shairi inayo virutubisho vya "Amino Acid Tryptophan" ambayo inachangia kutengeneza vimelea vya "Sirotanin" kama ilivyokusanya sehemu ya "Potassium" na vitamini B ambazo zikipungua mwilini zinasababisha hisia za dhiki na msongo. Hakika hadithi ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kabla ya miaka 1400 ameelezea Talbina (nayo ni Shairi) kwamba inakupunguza baadhi ya huzuni (na sio huzuni yote) ni kielelezo cha kutangulia kwa matibabu (katika Uislamu) na ugunduzi sahihi wa Kisayansi.

## Hadithi ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kuhusu maji ya Zamzam

Zamzam ni maji ya maadini yanayochipuka karibu na Al-Ka'aba Tukufu katika Msikiti mtukufu wa Makka. Waislamu wanaitakidi kuwa maji haya yanaendelea kutoka (chemchem) kwa namna ya Miujiza tangu maelfu ya miaka iliyopita.

Habari za Zamzam zinarejea kwa Nabii Ibrahimu (amani iwe juu yake) wakati alipomuacha mkewe bibi Hajar na mtoto wake Nabii Ismail (amani iwe juu yake) katika eneo la Makka kwa amri ya Allah Mtukufu. Wakati Nabii Ismail (amani iwe juu yake)) alipopatwa na kiu (wakati huu ni mtoto mchanga) Bibi Hajar alichukua juhudi ya kutafuta maji kwa kuenda na kurudi (Swafaa na Marwa) baada ya kipindi alipiga mtoto wake ardhi kwa miguu yake na yakatoka maji chini yake. Bibi Hajra akawa anayazingia yale maji kwa mchanga ili yahifadhike huku akisema zam zam zam zam yaani (jikusanye, jikusanye) kwa lugha ya Siryani. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) aliyasifu maji ya Zamzam kwamba ni maji yenye baraka akasema:

wake ni madhubuti Yaani kunywa

> "Maji ya Zamzam ni chakula cha kuliwa na ponyo la maradhi" Amepokea Tabrany na wapokezi

maji yake ni sawa sawa na kula mlo wa chakula kinachoshibisha, kama yalivyo kuwa yanaponesha maradhi. Maji huitwa ya maadini ikiwa maadini yaliyomo (ndani yake) yanafika au yanazidi Miligram 250 kwa lita moja.

Kwa mujibu wa Uchunguzi wa Kimaabara uliofanyiwa maji ya ZamZam kimepatikana kiwango cha maadini ndani yake baina ya Miligram 800-1000 kwa lita moja, kwa hivyo ni chakula cha kushibisha kutokana na maadini ambayo mwili unayahitajia.

Kama ilivyobainika kwamba maji ya Zamzam yanaendana na vipimo vya Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa kitengo maalumu cha maji ya kunywa na kwamba yamejaa Maadini muhimu kama "Calcium" ambayo mwili unayahitaji kujenga mifupa na meno na kwa kazi za virutubisho muhimu vinavyohusiana na moyo, misuli na mishipa, vile vile imo "Bicarbonate" ambayo inasaidia kusaga chakula, na "Fluoride" ambayo mwili unahitaji kwa ajili ya kuhifadhi siha ya meno.

Na inavyojulikana ni kwamba maji ya maadini yana faida nyingi za kiafya na kwamba pia yanasaidia kupunguza na kutibu uvimbe wa misuli na viungo.

Inazingatiwa maji ya Zamzam ni tajiri sana wa Maadini ya "Calcium", yanayo ndani yake "Calcium" Miligramu 190-200 kwa lita moja ukilinganisha na maji ya "Evian" ambayo yana "Calcium" milligram 78-80 kwa lita moja takriban, na maji ya "Perrier" ambayo yana "Calcium" Miligramu 147-150 kwa lita moja takriban.



Watoto wa miaka 4-8 wanahitaji Miligramu 800 ya "Calcium" kwa kila siku, na mjamzito na

mnyonyeshaji wanahitaji Miligramu 1300 ya "Calcium" kwa kila siku ambayo anaweza kuipata kutoka vyakula tofauti na zaidi kwenye maziwa, lakini maji ya Zamzam peke yake hupatikana baina ya asilimia 15-20 ya "Calcium" inayohitajia mwili kwa kila siku.





Hili ni neno "Rasulu-llah" limechorwa kwa muundo wa tone la maji ni katika kazi za Ustadh Faridi Al -'Aliy.

## Uyoga "Kam-ah" ni dawa ya Macho

Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake):



"Uyoga unatokana na Manna na maji yake ni tiba ya jicho"
Amepokea Bukhari (5708) na Muslim (5244).



"Kam-ah" ni aina ya Uyoga ambao huota kwa vikundi chini ya ardhi kwa kina cha sentimita 2-50 katika sehemu za jangwa lenye rutuba. Kam-ah hauna majani wala mizizi, na ina harufu ya kipekee na rangi yake inakuwa nyeupe au nyeusi au kahawa. (inaitwa hii "Kam-ah" katika baadhi ya mataifa ya Ghuba ya Kiarabu "Faq'a"). Uchambuzi wa Kemikali unaonesha kuwa maji yanapatikana kwa asilimia 77% katika "Kam-ah" (uyoga) na kwamba sehemu nyengine iliyobaki ni Protini na Mafuta na baadhi ya "Carbohydrete" na maadini, lakini uvumbuzi wa hivi karibuni ulionesha kuwa maji ya Uyoga ni tiba kubwa kwa magonjwa mengi ya macho hasa "Trakoma" ambayo ni magonjwa ya kuambukiza na yanasababisha uharibifu wa seli za "Cornea" ya jicho.

Angalizo:

"Manna" ni chakula alichoteremsha Allah Mtukufu kutoka mbinguni kwa watu wa Banii Israili.



## Tende ni Afya na Nishati

> Amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Nyumba ambayo hakuna tende ndani yake watu wake ni wenye njaa" Amepokea Muslim (2046).
>
> Na amesema Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Atakaekula asubuhi tende saba za Ajwa haitompata siku hiyo sumu wala uchawi". Amepokea Bukhari (5769) na Muslim (5241).

Uchambuzi wa kimaabara unaonesha kuwa tende zina mchanganyiko wa asilimia 6.70% ya "Carbohydrete" inayoharakisha kusaga chakula, na idadi kubwa ya maadini kama chuma na fosforasi na "Potassium" na "Magnesium" na "Calcium". Punje chache za tende zinakupa hisia ya kushiba haraka na uchangamfu wa kiwiliwili na akili. Hayo ni kwa sababu tende inayo (Glycemic Index) inayo karibia mia moja na hicho ni kiwango kikubwa sana kinachojulisha uharaka wa usagaji wa chakula na kufyonzwa kwa njia ambayo huongeza viwango vya sukari kwenye damu kwa muda mfupi baada ya kula. Basi sukari ya tende hufikia tishu na seli za ubongo na misuli kwa ufanisi mkubwa, kuzipa nguvu na uchangamfu kwa namna ambayo ni bora kuliko vinywaji vya nishati ambavyo vimeenea katika wakati wetu huu. Na Tende huimarisha misuli na mishipa, na huchelewesha kuzeeka, hupambana na kuwa na wasiwasi, huamsha tezi, hulinda upungufu wa damu na hulainisha mishipa ya damu, hulainisha matumbo na hunusuru uvimbe ndani yake. Pia tende ukila kabla ya kula kitu chochote asubuhi zinauwa minyoo na tende zilizorowekwa zinasaidia (kuponesha) kikohozi na mivimbe ya koo, wakati nyuzinyuzi zake zinapambana na tatizo la kuziba choo, na chumvi yake inaweka sawa Asidi ya damu ambayo husababisha vijiwe kwenye figo na kibofu cha nyongo na "Gout" na Bawasiri. Na tende imekusanya makundi ya vitamini lakini zilizo muhimu zaidi ni vitamin A ambayo inasaidia ukuaji na kuikinga ngozi na inakinga maradhi ya upofu wa usiku. Na vitamini B ambayo inalinda usalama wa mfumo wa neva "Nervous system" na hukinga mvutano wa neva na huzuwia kuziba kwa hamu ya kula.Tende inayo "Tannin" nyingi nayo ni dawa ya kuzuwia uvimbe na yenye ufanisi katika kusafisha mwili, pia inayo dawa inayotuliza Fuko la uzazi inayofanana na "Oxytocin" ambayo husaidia kutoka (kuzaliwa) mtoto na kupunguza damu baada ya kuzaa.

## Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) anausia kutumia mafuta ya Zaituni



Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) ameyasifu mafuta ya Zaituni ya kuwa yanatokana na mti wenye baraka na akasema: "Kuleni mafuta ya Zaituni na mjipake kwani hakika inatokana na mti uliobarikiwa" Amepokea Tirmidhiy (1851).

Unathibitisha uvumbuzi wa kisasa wa Matibabu kuwa mafuta ya Zaituni yamejaa faida za kiafya, na kwamba Asidi nyingi za mafuta ndani yake hazijajaa na hii inawakilisha asilimia 75- 85% wakati ambao Asidi za mafuta uliojaa ni asilimia 10-20% ya jumla ya Asidi ya mafuta iliyojumuishwa katika muundo wa mafuta ya Zaituni. Na tafiti zinaonesha kuwa mafuta ya Zaituni ni kinga ya maradhi ya moyo kwa kuchangia kuidhibiti "Cholesterol" inayodhuru, na kuipandisha "Cholesterol" yenye faida. Mafuta ya Zaituni yanatuliza tumbo, yanayo uwezo wa kukinga na kusaidia kutibu vidonda vya tumbo na uvimbe wa utando wa "Mucosa' ya tumbo "Mucous membrane". Ama kuhusu mafuta ya biashara yajulikanayo kuwa ni mafuta ya Zaituni bikira, yanayo asilimia kubwa ya "Antioxidant". hasa hasa vitamini E na "Phenol" kwa sababu yametolewa kwa njia ya uasili ya hali ya joto linalofaa. Yanatumika mafuta ya Zaituni kutibu matatizo ya ngozi pamoja na kuwa ni yenye vitu vinavyorutubisha ngozi kwa hali ya juu. Wanashauriwa wagonjwa wa kisukari na waliokaribu kupata ugonjwa huo kuongeza mafuta ya Zaituni kwenye lishe ambayo inayo sehemu kubwa ya Uwanga.



Natafiti zinathibitisha kuwa mchanganyiko wa uwanga "Carbohydrate" na mafuta ya Zaituni yanauwezo mkubwa wa kudhibiti sukari kwenye damu ikilinganishwa na vyakula vyenye mafuta kidogo.



"Allah ni nuru ya mbingu na ardhi; mfano wa nuru Yake (anayoongozea waja wake) ni kama shubaka (lenye kuwekwa) ndani yake taa: taa (ile imo) katika tungi, (chemni): tungi (lile ni) kama nyota ing'arayo, inayowashwa (taa hiyo kwa mafuta yanayotoka) katika mti uliobarikiwa wa mzeituni, usio (upande) wa mashariki wala wa magharibi, · (ukawa unapigwa na jua sana linapopinduka na linapotoka); yanakaribia mafuta yake kung'aa (wenyewe) ingawa moto haujayagusa-Nuru juu ya nuru-Allah humuongoza katika nuru Yake Amtakaye, na Allah Hupiga mifano kwa watu; na Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

Suratu-Nuur aya ya 35.

SURA

# 11

# MWISHO



Msikiti Mtukufu wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) ndani ya Mji Mtukufu wa Madina

## MUHAMMAD MJUMBE WA ALLAH
(rehema na amani ziwe juu yake)

### Kisa cha Suraqa Al-Kinani: Utabiri unathibitika baada ya miaka 20

Katika mwaka wa 622AD Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alihama Makka kuelekea Madina pamoja na rafiki yake Sahaba Abu Bakar kwa amri aliyopewa na Allah Mtukufu, na viongozi wa Kikuraishi walitangaza zawadi ya ngamia mia moja kwa yeyote atakaye mpeleka Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) akiwa hai au amekufa. Hilo lilimsukuma mmoja kati ya mashujaa wa Kiarabu nae ni Suraqa bin Malik kumtafuta Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na rafiki yake.

Alijulikana Suraqa kuwa ni mpiganaji mwenye kujua kuzifuata athari za nyayo, na mwenye kuhimili misukosuko ya safari njiani. Basi alianza kuzifuata athari za safari ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) na rafiki yake. Na baada ya utafutaji mkubwa Suraqa aliwapata Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na rafiki yake Abu Bakar (radhi za Allah ziwe juu yake), lakini wakati alipowaona na kutaka kuwafikia Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alimuomba Mola wake amuondoshee shari zake, na kwa uwezo wa Allah Mtukufu Farasi wake (Suraqa) akajikwaa kwenye mchanga na akaanguka chini, na ajabu zaidi alipojaribu kusimama na kwenda kwa mara nyengine ilididimia miguu ya Farasi katika mchanga, na tukio hili la kudidimia kwa Farasi lilijirudia zaidi ya mara moja. Na Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alimtaka Suraqa arejee Makka na asimuachie yeyote kumfuata Mtume, na Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alimuelezea kwa kujiamini na kwa kumuamini Allah Mtukufu kwamba dini ya Allah Mtukufu itaenea katika ardhi yote, na kwamba ipo siku (Suraqa) atavaa bangili (mapambo) za Mfalme Kisra Mfalme wa Fursi kuonesha kua Waislamu watakuwa na nguvu na kunusuriwa kwa kuwashinda Wafursi miaka ijayo, na jambo hilo litakua ni kheri kwake kuliko zawadi kutoka kwa Makureishi. (na zimetaja baadhi ya riwaya kuwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alimuandikia juu ya hilo).



**Amesema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake): "Utajisikiaje ewe Suraqa pindi utakapovaa bangili za Kisra?"** Amepokea Al-Bayhaqy katika "Sunanul-Kubra" (6/357) namba (13156).

Alijua Suraqa kuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alikua mkweli basi aliurejesha msimamo wake na akakubaliana na ombi la Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na wakakamilisha Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) yeye na Abubakar (radhi za Allah ziwe juu yake) safari yao mpaka wakafika Madina Munawwarah. Ilipita miaka akafariki Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kisha baada ya miaka miwili alifariki Khalifa Abubakar (radhi za Allah ziwe juu yake), na Khalifa Omar bin Khatwab akawa kiongozi wa Waislamu (radhi za Allah ziwe juu yake) na mipaka ya dola ya Kiislamu ilitanuka katika zama zake hadi kufikia Waislamu kuifungua miji ya Fursi mwaka 642 AD. Na zikaanguka hazina za Kisra bin Hurmuz mfalme wa Fursi zikawa mikononi mwa Khalifa Omar bin Khatwab (radhi za Allah ziwe juu yake). Akakumbuka Khalifa Omar bin Khatwab kisa cha Suraqa ambae kwa wakati huo amekuwa mzee sana, Khalifa Omar alimuita Suraqa Msikitini, na baada ya Sala alisimama Khalifa Omar (radhi za Allah ziwe juu yake) mbele ya Waislamu na kuwakumbusha ahadi ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwa Suraqa, basi alimvisha nguo ya Kisra na akaweka taji lake juu ya kichwa chake na akamvisha bangili zake. Kwa hakika lilikua ni tukio lenye kusisimua sana lililopelekea Suraqa kulia na watu wengine waliokua wakisali pembeni yake walipoona ahadi ya Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) imetimia baada ya miaka kumi tangu kufariki kwake, (ni miaka ishirini tangu kutokezea tukio la Suraqa).



Mchoro katika kazi za mwandishi mchoraji wa Misri Isaam Abdul-Fattah



## Kisa cha funguo ya Al-Ka'aba – amana hadi hii leo

Katika mwaka wa 630 AD Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alipata ushindi dhidi ya viongozi wa Kikureishi na kufanikiwa kuingia Makka kwa salama bila ya vita, na hakurudi Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) katika mji wake wa Makka ili amalize maisha yake yaliyobakia lakini alirudi ili kuisafisha Al-Ka'aba kutokana na ibada za Masanamu na iwe ni nyumba ya ibada ya Allah Mtukufu mmoja aliye mpweke anakusudiwa yeye tu na watu kutoka kila sehemu , na kwa hilo lilirejeshwa lile lengo ambalo Nabii Ibrahim (amani iwe juu yake) aliijenga Al-Ka'aba hio kwa amri ya Allah Mtukufu. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) aliyaondosha Masanamu yote yaliyokua pembeni ya Al-Ka'aba, na akamtaka Sahaba wake Bilali (radhi za Allah ziwe juu yake) apande juu ya Al-Ka'aba na aseme "Allah ni mkubwa Allah ni mkubwa, ninashuhudia kua hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokua Allah, ninashuhudia kuwa Mtume Muhammad ni mjumbe wa Allah."

Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alitaka ufunguo wa Al-Ka'aba., Akamwita Bwana Othman bin Talha Shaibaniy ambae alikuwa ndie msimamizi wa Al-Ka'aba kwa kurithi tangu kabla ya Uislamu, na kabla ya kusilimu kwake aliwahi kumzuwia Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) kusali ndani ya Al-Ka'aba lakini alisilimu kabla ya kutekwa mji wa Makka. Imesemwa kuwa wakati alipotawala Qusayyi Makka nae ni babu yake wa tano Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alimchagua mtoto wake mkubwa awe msimamizi wa Al-Ka'aba, na baada ya hapo watoto wake walimrithi mpaka usimamizi ukafikia kwa Bwana Othman bin Talha.








Bwana Othman bin Talha (radhi za Allah ziwe juu yake) hakuwa na namna isipokua kumpa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) funguo ya Al-Ka'aba, na kumepelekea kuikosa ile hadhi ya kusimamia Al-Ka'aba, na maelfu ya Waislamu walikuwa wakisubiri ili kujua nani atapata utukufu wa kusimamia Al-Ka'aba baada yake. Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alinyamaza kwa kipindi, kisha alifungua mlango wa Al-Ka'aba na akaingia ndani ili kuisafisha kutokana na Masanamu yaliyokuwemo humo, kisha alitoka na kumwambia Bwana Othman bin Talha:

> "Leo ni siku ya kufanya wema na kutimiza ahadi, chukueni funguo ya Al-Ka'aba enyi watu wa Talha muwe nao daima, wala hakupokonyeni mtu yoyote isipokuwa dhalimu."
>
> Amepokea Twabrany katika "Al-Kabir" (11/120) namba (11234)



## Wema na kutimiza ahadi yanaendelea hadi leo



Ufunguo wa Al-Ka'aba umeendelea kuwepo katika himaya ya Bani Shaibah kwa zaidi ya miaka 1,400 hadi hii leo, wanapokezana usimamizi wa Al-Ka'aba na kuihudumia kutimiza amana ya Allah Mtukufu, kizazi baada ya kizazi pasi na kujitokeza yoyote anayezozana nao ili asijekua dhalimu kama alivyosema Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake). Na katika zama zetu hizi Ufalme wa Saudi Arabia ndio unasimamia usafishaji wa Al-Ka'aba kila mwaka na humuita mtu kutoka ukoo wa Bani Shaibah ili afungue mlango wa Al-Ka'aba ili isafishwe kwa maji ya Zamzam na maji ya mawaridi na mengineo katika manukato, na kupakwa kuta zake za ndani kwa mafuta mazuri ya Uud. Ni wema ulioje huu? heshima iliyoje? Kwa maneno ya kiongozi ambayo wanajilazimisha nayo wafuasi wake baada ya kufa kwake kama anaishi nao?



SURA

# 11

# SANAA YA USANIFU NA KHATI ZA KIISLAMU



▲ Picha ya Msikiti wa Mfalme Qabus katika mji wa Muscat-Oman. Picha imepigwa na Peter Gould



**Peter Gould - Australia**

Amefanikiwa msanii na mbunifu kutoka Australia Peter Gould kwa kudhihirisha uzuri wa Usanifu wa Kiislamu kupitia utaalamu wa Kidigitali na zikawa safari zake katika nchi tofauti hasa hasa nchi za Kiislamu ndio chimbuko la utambuzi na ubunifu wake, na ikawa michoro yake ya picha ndio mlango wa mchanganyiko wa kitamaduni na Ustaarabu na inaonesha ushawishi wa Usanifu wa Kiislamu juu ya miundo ya usanifu na mapambo ya duniani.



## Peter Sanders – Uingereza

Ni mpiga picha wa Kiingereza mtaalamu, ana mkusanyiko wa picha za "Photograph" za kitaalamu zinazozidi picha laki tano, alizikusanya kipindi cha upigaji picha wake wa Ustaarabu na Tamaduni kutoka nchi arobaini.

Peter amependa Usanifu wa Kiislamu akaelekea nchi za mashariki na akajihusisha kwa kupiga picha za Usanifu na mapambo ya Kiislamu, ana kitabu cha picha kinachoitwa "Kwenye kivuli cha mti" ameonesha kwa njia ya kipekee aina mbali mbali za Ustaarabu wa Kiislamu uliostawi katika maeneo mbali mbali ulimwenguni zimetofautiana asili yake na utamaduni wake lakini zimeathirika kwa njia ya wazi kabisa na Ustaarabu wa Kiislamu.

Serikali ya Morocco imempa Peter Sanders jukumu la upigaji picha na kuweka kumbukumbu za Misikiti ya kitarekhe na Usanifu na mapambo ya Kiislamu katika Ufalme wa Morocco.















### Hassan Shalaby – Uturuki

Anazingatiwa Hassan Shalaby ni mmoja ya watu maarufu wataalamu wa Sanaa ya khati za Kiislamu katika ulimwengu, tangu alipoanza kusomesha khati za Kiislamu katika mwaka 1976 AD amewapa ijaza zaidi ya wanafunzi 44 katika nchi tofauti ulimwenguni. Kama alivyokuwa amechora michoro kipekee ya khati za Kiislamu kwenye Msikiti wa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na Msikiti Qubaa uliopo katka mji wa Madina, na Msikiti wa Sultan Ahmad ulipo Istanbul na Msikiti wa Al-Fatih katika mji wa Pforzheim uliopo Ujerumani, na msikiti wa Ijumaa uliopo Johannesburg Afrika ya Kusini na vile vile katika kituo cha afya cha Kiislamu kilichopo Kuwait.







**Muhammad Zakariya – Marekani**

Muhammad Zakariya anazingatiwa ni balozi wa khati za Kiislamu katika nchi ya Marekani. Amezipenda khati za Kiarabu na sanaa za Kiislamu tangu udogoni mwake na pale alipofikia umri wa miaka 19 alisafiri kujifunza khati za Kiislamu katika nchi ya Morocco na Uturuki.



Muhammad Zakariya ni Muamerika wa mwanzo kupata Ijaza katika Sanaa ya khati za Kiislamu kutoka Uturuki. Ana kazi nyingi za kipekee na miongoni mwa hizo zilizokuwa maarufu ni muundo wa Stempu ambayo ilitoleshwa na Serikali ya Marekani inayobeba neno la pongezi ya Idi njema ya Waislamu katika siku kuu yao "Eid Mubarak".










Mchoro unaonesha Sanaa ya khati za Kiislamu kwa aya tukufu "Hakuna malipo ya ihsani ila kulipa ihsani (vile vile)"









### Nuria Garcia Masip - Hispania

Nuria amezaliwa na akaishi katika mji wa Ibiza uliokuwepo Hispania kisha akahamia Marekani kwa kusoma masomo ya Fasihi na Sanaa katika chuo cha George Washington kilichopo Marekani.

Baada ya kukamilisha masomo yake ya chuo akajikhusisha Nuria katika Sanaa za khati za Kiislamu na akapata Ijaza ya mwanzo katika khati za Kiislamu kutoka Uturuki mwaka 2007.

Nuria ameshiriki maonesho ya kimataifa na zikapwekeka kazi zake kwa mandhari nzuri pamoja na kudumisha michoro ya asili ya khati za Kiislamu.



**Haji Nurdiin Juang Jiang - China**

Mwalimu wa somo la khati Haji Nurdiin amezaliwa mwaka 1963AD katika jimbo la "Shangdong" nchini China na yeye ni miongoni mwa watu maarufu wanaochonga Khati ambao walioleta kiunganishi cha kipekee baina ya Sanaa ya khati katika lugha mbili ya Kiarabu na Kichina.






Hizi picha mbili zinawakilisha michoro miwili ya kisanaa yenye neno la "La Ilaha Illa Allah" na "Muhammad Rasulu-llaah"

Ama Quba lililochorwa sehemu ya chini ya picha limepangwa kwa ibara "Muhammad Rasulul-llah" limerejewa mara mia.





(سل عن الرفيق قبل الطريق،
وعن الجار قبل الدار)

(Uliza kuhusu Rafiki kabla ya njia, na Uliza Jirani kabla ya nyumba)

**Nobuko Sagawa – Japan**

Nobuko Sagawa anazingatiwa kuwa ni miongoni mwa Wajapani wa mwanzo ambao wamebobea katika Sanaa za khati za Kiarabu. Baada ya kumaliza masomo yake katika kitivu cha Sanaa mjini alielekea mji wa Damascus kujifunza khati za Kiarabu mpaka akawa hodari wa khati za “Kufiy” na khati za “Thuluth” ameshiriki katika maonesho mengi ya kimataifa, na akaweza kukusanya maandiko ya kabila la “Kana” lililokuwepo Japan na “Kanji” lililokuwepo China na herufi za Kiarabu.



Mchoro unaonesha khati za Kiislamu za “Thuluth” kwa aya “Na Hatukukutuma (hatukukuleta) ila kwa watu wote.”



**Farid Al-Aliy – Kuwait**



Farid Al-Aliy ni mkuu wa kituo cha Sanaa za Kiislamu kilichokuwepo Kuwait, na mwenye kitabu kinachoitwa "Muhammadiyyaat" ambacho amekusanya ndani yake michoro ya neno la "Muhammad" na kinaonesha kitabu michoro mia tano ya kisanaa ikagaiwa michoro hiyo makundi kumi na moja ya kiufundi. Ukakamilika mjengeko wake wa neno "Muhammad" kwa michoro inayovutia, miongoni ya michoro hiyo amefananisha na jani la mti, mengine amefananisha na tone la maji, na mengine inaonesha mfano wa Quba kwenye usanifu wa Kiislamu. Na Ustadh Farid amefanya kazi nyengine za kisanii zinazovutia, kazi muhimu zaidi ni umbile la kisanaa la kiufundi kwa neno la "Allah".





**Muhammad Al-Mandy – Emirate**

Limekuwa jina la Muhammad Al-Mandy maarufu katika nchi ya Emirate baada ya kufanikiwa kufanikisha mkusanyiko wa michoro ya Kisanaa, kwa kupamba paspoti na pesa za karatasi za nchi ya Emirate, pamoja na michango yake ya kipekee katika khati za Kiislamu ambazo zilipamba Msikiti mkubwa wa Sheikh Zaid uliokuwepo Abu Dhabi ambao umekuwa jengo na alama inayoonesha michoro mizuri ya Usanifu wa Kiislamu wa kisasa katika ulimwengu.



Huu mchoro wa kisanaa wa kipekee wa neno "Muhammad" kwa herufi za Kiarabu uliotenganika, nao ni kiungo kikuu cha picha aliyoichora msanii Muhammad Al-Mandy ambao umekusanya maneno mawili "Muhammad" kwa Kiingereza na Kiarabu. Hii kazi ya kisanaa inaonesha mchanganyiko baina ya herufi nne za Kiarabu na herufi nane za Kiingereza kwa umbile lililokuwa zuri mno.





**Msikiti mkubwa – Nchini Kuweit.**

Ni Msikiti mkubwa katika nchi ya Kuweit , upo katikati ya mji mkuu , na unatosheleza kiasi cha watu elfu thalathini. Hivi karibuni umefanyiwa ukarabati upya ndani na kupambwa kwa mapambo yenye kupendeza ya Kiislamu.







Picha hii imepigwa katika usiku wa mwezi 27 mwezi Mtukufu wa Ramadhan, na kama inavyojulikana kuwa Waislamu wanafunga mwezi wa Ramadhani kuanzia alfajiri mpaka kuzama kwa jua, na wanatekeleza ibada ya Sala ya Tarawehe baada ya Sala ya Isha na Sala ya Tahajjud katika kumi la mwisho la mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Picha na Ahmad Al-Umayry.








244

**Msikiti mkubwa wa Sheikh Zayed – uliopo Abu Dhabi – UAE.**

Nao ni Msikiti mkubwa zaid nchini Emirates, ni wa nane miongoni mwa Misikiti mikubwa zaidi duniani, kiasi ambacho unafikia ukubwa wake sawa na viwanja vitano vya kuchezea mpira wa miguu, na unatosheleza zaidi ya watu 40,000.

Umekusanya Msikiti huu Maquba 82 na minara 4 yenye urefu kila mmoja mita 107, na ndani ya Msikiti kuna zulia kubwa Zaidi ulimwengni, linafika ukubwa wake mita za mraba 5627 na kuna shada la taa kubwa zaidi duniani linalofikia urefu wake mita 15 na upana wa duara lake ni mita 10 na inazingatiwa ni moja ya sehemu muhimu za kitalii katika nchi ya Imarati.





**Msikiti mkubwa wa Imam Muhammad bin Abdul-Wahab – Qatar.**

Umefunguliwa mwaka 2011 nao ni Msikiti mkubwa zaidi nchini Qatar ambao umetengenezwa kwa njia inayoakisi Sanaa ya Usanifu wa Kiislamu na umechukuwa mtindo wa ujenzi wa nchini Qatar. Na Msikiti huo una Maquba 28 na mnara mmoja mkubwa wenye urefu wa mita 65 na unatosheleza karibia watu elfu kumi na mbili, na ulijengwa kwa jumla ya eneo la mita za mraba 175,000.



**Makumbusho ya Sanaa ya Kiislamu. nchini Qatar.**

Imefunguliwa sehemu hii ya makumbusho kwa watu wote mwaka 2008. Yaliyomo ndani ya jumba la makumbusho ni vitu vya zamani vinaonesha utofauti wa kisanii katika ulimwengu wa Kiislamu. Amelibuni jengo hili la Makumbusho mbunifu wa Marekani Leoh Ming Pei. Anaejulikanwa kiufupi kwa jina la I.M. Pei nae ni mbunifu wa Piramidi ya Louvre, Paris. Jengo la vigae na chuma.













**Msikiti Saleh – Sanaa – Yemen.**

Nao ni Msikiti mkubwa zaidi nchini Yemen, umefunguliwa mwaka 2008AD, Jumla ya eneo lake linafikia mita za mraba 224,000, na unatosheleza kiasi cha watu 40,000. Na umejengwa Msikiti huo kwa mtindo wa kisanifu wa Yemen. Msikiti una milango kumi na tano ya mbao na minara sita mikubwa





**Msikiti mkubwa wa Sultan Qabus – Mascut Oman.**

Nao ni Msikiti mkubwa zaidi katika Falme ya Omani, umefunguliwa mwaka 2001, una zulia na shada la taa kubwa zaidi yaliyotengenezwa kwa mkono, linafikia eneo la Ujumla la Msikiti mita za mraba 416,000, wakati eneo la Msikiti linafika mita za mraba 40,000.







**Msikiti Jumeira –uliopo Dubai – nchini Emirates.**

Ni mmoja kati ya Misikiti mizuri zaidi nchini Dubai , na unaakisi sanaa ya kisasa katika usanifu wa Kiislamu, na unatembelewa na idadi kubwa ya watalii wa kigeni.



**Msikiti wa Mfalme Hussein – Amman – Ufalme wa Jordan.**

Umefunguliwa mwaka 2005, nao ni Msikiti mkubwa zaidi nchini Jordan ambao unawakilisha fani ya kisasa katika Usanifu wa Kiislamu, Msikiti unaangalia mji wa Amman na minara yake 4, na ulijengwa kwenye kilima kilichonyanyuka takriban mita 1000 juu ya usawa wa bahari.



**Msikiti wa Ahmad Fatih – Ufalme wa Bahrein.**

Aliufungua kiongozi wa nchi ya Bahrain aliefariki Shekh Issa bin Salman Al-Khalifa mwaka 1988,eneo lake ni mita za mraba 6500, na unatosha kusali watu 7000, Msikiti huo unaakisi mchanganyiko wa Sanaa ya Usanifu wa Kiislamu na utamaduni wa wenyeji.







Quba la Mwamba - Quds

**Msikiti wa Aqsa - Quds – Palestina.**

Waislamu wanaitakidi kuwa Msikiti Aqsa ni Msikiti wa pili kujengwa duniani baada ya Msikiti mtukufu wa Makka kwa ajili ya kuabudiwa Allah mmoja , nao ni Msikiti unaotukuzwa na Waislamu na ulikua ndio qibla chao cha mwanzo katika sala zao kabla ya kuwaamrisha Allah Mtukufu kuelekea upande wa Msikiti mtukufu wa Makka (Al-bait Al-'Atiiq) ambayo aliijenga Mtume Ibrahimu na mwanae Nabii Ismail (juu yao amani) katika mji wa Makka.







**Msikiti Aqsaa-Quds**

Unafikia eleo lake mita za mraba 144,000, na unajumuisha ukuta (uzio) wa Msikiti Aqsa Msikiti wa Al-qibly na Msikiti wa Qubbat Sakhrah ambao aliujenga Khalifa wa Umawiyy Abdul-Malik bin Marwan katika kipindi cha baina ya mwaka 688 na 692 juu ya mwamba ambao inaaminika kuwa Mtume Muhammad (rehema na amani ziwe juu yake) alipaa kupitia hapo kuelekea mbinguni safari ya Miiraj, nalo ni jengo la thamani lilowekwa juu yake Qubbah lilopambwa kwa dhahabu kiasi cha mita 29.4.









**Msikiti Umawiyy – Damascus-Syria.**

Ulijengwa Msikiti huu mwaka 86 Hijriya – 706 AD. Katika utawala wa Khalifa wa Umawiyya Waliid bin Abdul-Malik. Nao ni miongoni mwa Misikiti mikubwa na Msikiti wa zamani katika ulimwengu. na umepambika kwa Sanaa ya Usanifu ulio muhimu na mtukufu. Unafikia eneo lake kilo mita za mraba 4000. Imeelezwa kuwa Salahuddinil-Ayyubiyy aliyefariki mwaka 1193 AD amezikwa upande wa kusini wa Msikiti Amawy.



**Msikiti Mkuu – Saamurai – Iraq.**

Ameujenga Khalifa wa Abbasiyy Al-Mutawakkil Samurrai-Allah katika mwaka 234 Hijria – 851AD.. Msikiti Samurrai ulikuwa ndio Msikiti mkubwa wao ulimwenguni unasifika kwa mnara wake uliojipinda ambao unafikia urefu wake mita 52 na upana wake mita 33 na umejengwa kwa mtindo wa Piramidi za babilioni. katika Msikiti huu zipo sehemu za kutembea 17 zilizopambwa kwa Mozaik ya vigaye bluu iliokoza.



**Msikiti Sultan Ahmad – Istanbul – Uturuki.**

Unajulikana kwa jina la Al-Masjidil – Azraq (Blue Mosque). Nao ni Msikiti pekee Uturuki wenye minara sita na muunganiko wa MaQuba. Aliamrisha Sultan Ahmad ambae alikuwa ni Khalifa wa Othmaniya aliamrisha kujengwa katika mwaka 1609AD. Unazingatiwa Msikiti  Sultan Ahmad (Masjidul Azraq) ni sehemu muhimu ya kitalii katika mji wa Istanbul, wanautembelea maelfu kwa maelfu ya watalii kutoka pande mbali mbali za ulimwengu kwa mwaka mzima.





**Makumbusho ya Ayasufiya – Istanbul – Uturuki**

Lilikuwa ni Kanisa la Bizantiya zamani. Halafu ukawa ni Msikiti wa Othmaniyya kwa kipindi cha takriban miaka 481, na kwa zama za sasa lilibadilishwa jengo hili la kihistoria na kuwa ni makumbusho na maelekeo ya watalii mwaka 1935 AD, unatembelewa na maelfu ya Watalii wa kigeni kwa mwaka mzima.









**Taj Mahal - Agra – India.**

Taj Mahal inazingatiwa kuwa ni sehemu ya makumbusho ya Kiusanifu wa kipekee mpaka hivi sasa, ameujenga Mfalme wa Mangoli Shah Jahan katika kipindi cha baina ya mwaka (1632-1653) AD. na inakusanya sehemu hii ya Taj Mahal Msikiti mkubwa, na jengo la Taj Mahal ambalo limepambwa kwa sura kamili kutoka karika Qur-an Tukufu na limo katika sehemu hiyo kaburi la Mumtaz Mahal mke wa Sultan na kaburi lake vilevile lipo pembeni ya kaburi la mke wake.



▲ Msikiti wa Mfalme Faisal - Islamabad – Pakistan.

▼ Ngome ya Lahore - Pakistan





▲ Msikiti Mkuu wa Ijumaa –New Delhi-India. Ni Misikiti mkubwa katika nchi ya India, umekamilika ujenzi wake mwaka 1656 AD.

▼ Ngome nyekundu New Delhi-India Red Fort – New Delhi- India





▲ Msikiti wa Nyota -Daaka-Bangladesh.

▼ Msikiti Orbon Galiboly – Sydney – Australia





▲ Msikiti wa Istiqlaal-Jakarta-Indonesia

▼ Msikiti Uliopo Patani -Tailand.







▲ Msikiti Sultan Omar Saifud-Diin - Bruney




▲ Msikiti Sultan -Singapore.



▲ Msikiti wa Tokyo-Japan. (Umejengwa kwa mtindo wa Othmaniya



▲ **Msikiti wa Karistalia – Kuala Terengganu - Malaysia**

Umefunguliwa katika mwaka wa 2008 AD. Kristal ndio kifaa cha msingi katika ujenzi wa Msikiti huu uliopo katika bustani ya athari za Kiislam katika kisiwa cha Wan Man

▼Msikiti wa Butrajaya nchini Malaysia





▲ Msikiti wa Kuwantan -Malaysia

▼Msikiti wa mji wa Bairak -Malaysia.





**Jaamiul- Azhar-Cairo - Misri**

Umejengwa katika mwaka 971 Hijriya na ukafunguliwa mwaka 988 Hijriya. Msikiti huu umeorodheshwa miongoni mwa Msikiti ya zamani katika ulimwengu.



**Msikiti wa Ahmad bin Tuuluun- Cairo-Misri**

Umekamilika kujengwa mwaka 879 Hijriya nao mmoja katika Misikiti mikubwa ulimwenguni ambao eneo lake ni mita za mraba 26,318, na umepata umaarufu kwa Usanifu wake mzuri na mnara wake wa kipekee.













**Msikiti Mkuu wa Qurtuba - Spain**

Ameamrisha kujengwa kwake Abdu-Rahman A-Dakhil mnamo mwaka 92 Hijriya 785 AD katika mji wa Qurtuba Mji mkuu wa Utawala wa Kiislamu wa Hispania. Umetanuliwa mara nyingi ndani ya kipindi cha Ukhalifa wa Kiislamu. Ulibadilishwa kuwa Kanisa la Kathedral “Cathedral” baada ya kuanguka utawala wa Qurtuba, na kwa sasa unajulikana kwa jina “Cathedral of our lady Assumption” na huitwa pia kwa jina “Mezquita” maana yake ni “Msikiti” kwa lugha ya Hispania.





Msikiti Mkuu wa Qurtuba kwa mtazamo wa ndani



**Kasri Jekungu– Greneda –Spain:**

Ni sehemu muhimu ya kitalii nchini Spain na ulimwenguni. lilijengwa Qasri hili wakati wa kipindi cha utawala wa Kiislamu Garnada (1353-1391) AD, jengo lake lina akisi ujenzi bora wa kiufundi wa Usanifu wa Kiislamu Uhispania. Na imejengwa ndani ya Qasri Jekundu Kasri la Wafalme wa Kirumi Charles wa Tano katika mwaka 1527 AD.













**Msikiti Wa Hassan wa Pili – Casablanca - Morocco**

Aliamrisha kujengwa Msikiti huu Mfalme Al-Hasan wa Pili Mfalme wa Morocco katika mwaka 1993AD. Na akasimamia kuweka michoro yake injinia wa kifaransa aitwae Michel Pinseau, unazingatiwa mnara wake ndio mrefu kubwa zaidi katika nchi ya Morocco bali ndio mnara mrefu zaidi ulimwengu mzima una mita 210. Na juu ya mnara huo kuna taa ya Laser yenye mwangaza mkubwa usiku humurika kuelekea Msikiti Mtukufu wa Makka. Na unaingia katika Msikiti huu watu 25,000.



**Msikiti wa Qairawan- Fes- Morocco**

Ulianzishwa mnamo mwaka 987 AD ni Msikiti wa pili kwa ukubwa katika nchi ya Morocco baada ya Msikiti wa Mfalme Hassan wa Pili. Pia Msikiti huu ni mmoja wa Misikiti ya Ijumaa ya zamani zaidi katika ulimwengu pia kati ya moja ya majengo ya kale ya Kiislamu katika mji wa Fes.







▲ Msikiti wa Kaibatishak ▼ Msikiti wa Azadiy Ishqi Abad -Turkmanistan





▲ Msikiti wa Shir Dor Madrasah, Samarqand - Uzbakistan.

▼ Msikiti wa Bukhara - Uzbakistan.





▲ Msikiti wa Kali Sharif –Qazan - Urusi.



▲ Msikiti Mkubwa wa Moscow - Urusi.



**Msikiti Mkuu wa Paris - Ufaransa**

Ni Msikiti mkubwa zaidi nchini Ufaransa, Umejengwa baada ya vita vya kwanza vya dunia na kufunguliwa tarehe 15/7/1926 AD.



الله أكبر..الله أكبر..

أشهد أن لا إله إلا الله..

أشهد أن محمداً رسول الله..

حي على الصلاة..

حي على الفلاح..

الله أكبر..الله أكبر..

لا إله إلا الله

Waislamu wanasali Sala tano kwa siku, na hunadiwa Sala juu ya Minara kila unapoingia wakati wa Sala. Na wito huo unaitwa Adhana.

Adhana ni wito kwa Muislamu ili awache kazi zake na shughuli zake kwa muda mfupi ili kutekeleza amri ya Allah kwa kusali. Na katika Adhana ni wito wenye kuleta mafungamano na Allah Mtukufu ndani ya wakati maalumu katika siku, ni jambo kubwa sana na lenye umuhimu mkubwa kuliko mtu kushughulikia mambo yake binafsi ya kidunia. Maandishi ya Adhana yamenakishiwa na kuchongwa katika mnara huu kwa muundo mzuri wa kisanaa ya kipekee nayo:



**Msikiti wa Bainazbirgh - Ujerumani.**

Mnara wa Msikiti umepambwa kwa maneno ya Adhana ambayo yamebuniwa na mchoraji mbunifu Muhammad Mandiy kutoka Emarete.




Msikiti Mkuu Jiyan - China



▲ Msikiti mkuu - Indonesia. ▼ Msikiti wa Huwei - Naingazy - China





▼ Msikiti wa mfalme Faisal - Conakriy - Guinea ▲ Msikiti mkuu - Tuba - Senegal.





▼ Msikiti Djenne - Mali. ▲ Msikiti wa Bubuduyulaso – Burkina Faso.



Katika mji wa Djenne ndio Msikiti mkubwa duniani uliojengwa kwa udongo, kila mkaazi wa mji huu mara mbili kwa mwaka wanaleta gari la mzigo wa udongo wa mto Bani uliojirani na kusaidiana katika kukarabati kuta za Msikiti huu.

الصلابي، علي محمد ٢٠٠٨. السيرة النبوية عرض وقائع وتحليل أحداث، مكتبة دار السلام، المملكة العربية السعودية.

عبد الغني، إلياس ٢٠٠٣. تاريخ المدينة المنورة، رشيد للنشر، المملكة العربية السعودية.

العبد المنعم, عبدالله ٢٠١٠. نهضة الحضارة الإسلامية، دار إقرأ للنشر – دولة الكويت

الغزالي، محمد ٢٠٠٨. فقه السيرة – مراجعة وتعليق الشيخ محمد ناصر الدين الألباني، دار الدعوة للنشر، مصر

العودة، سلمان بن فهد ٢٠٠٨. هذا رسول الله، المؤتمر العالمي الثاني لمنظمة النصرة العالمية، وزارة الأوقاف، دولة الكويت

المباركفوري، صفي الرحمن ١٩٩٥. روضة الأنوار في سيرة النبي المختار، دار السلام، الرياض – المملكة العربية السعودية

المصلح، عبدالله بن عبد العزيز ٢٠٠٦. أنه الحق، إصدارات الهيئة العالمية للإعجاز العلمي في القرآن والسنة، المملكة العربية السعودية

المطوع، جاسم ٢٠٠١. زوجات النبي في واقعنا المعاصر. دولة الكويت

المغلوث، سامي ٢٠٠٨. الأطلس التاريخي لسيرة الرسول ص ، العبيكان للأبحاث والتطوير، المملكة العربية السعودية

هارت، مايكل ١٩٩٢. المئة: تصنيف لأكثر الشخصيات تأثيرا في التاريخ، مجموعة كارول للنشر، نيوجيرزي، الولايات المتحدة.

# المراجع


أدير، جون ٢٠١١. قيادة محمد ص ، ترجمة رامي كلاوي، إصدارات التراث للنشر، الإمارات العربية المتحدة

أرمسترونج، كارين ٢٠٠٢. الإسلام تاريخ موجز "Islam, a short history" هاربر كولينز، نيويورك

أرمسترونج، كارين ٢٠٠٧. محمد نبي لزماننا "Muhammad, a prophet for our time" هاربر كولينز، نيويورك

إسلام، يوسف ١٩٩٥. حياة آخر نبي، دار السلام، المملكة العربية السعودية

الإمام النووي، يحيى ٢٠٠٣. رياض الصالحين، القاهرة، مصر

البخاري، محمد بن إسماعيل الإمام أبو عبد الله ١٩٩٧. صحيح البخاري، دار الأفكار الدولية – عمان – الأردن

الحاج أحمد، يوسف ٢٠١٠. معجزات القرآن ، دار السلام, الرياض، المملكة العربية السعودية

حماد، أحمد زكي ٢٠٠٧. القرآن الكريم، ترجمة وتفسير بالإنجليزية، Lucent Interpretations، إلينويز، الولايات المتحدة.

دي لامارتين، ألفونس ٢٠٠٦. حياة محمد، مختارات مترجمة للعربية للدكتور محمد قوبعة، مؤسسة جائزة عبدالعزيز سعود البابطين للإبداع الشعري – دولة الكويت

رضا، صالح أحمد ٢٠٠٠. الإعجاز العلمي في السنة النبوية، العبيكان للأبحاث والتطوير، المملكة العربية السعودية

رضا، صالح أحمد ٢٠١٠. إنها النبوة: بصائر وعبر من سيرة خير البشر، دار الخيل للنشر والتوزيع، الإمارات العربية المتحدة

رمضان، طارق ٢٠٠٧. على خطى النبي "In the footsteps of the prophet" أوكسفورد – بريطانيا

الزايد، سميرة ١٩٩٥. مختصر الجامع في السيرة النبوية، الطبعة الأولى ، دمشق – الجمهورية العربية السورية

# NOTES

Mwongozo wa kina na uliokunjuliwa ambao ni rahisi kuusoma na kuufahamu

# MWONGOZO WA MFUKONI KUHUSU MUHAMMAD ﷺ



"Hakika uchaguzi wangu wa Muhammad kuwa wa mwanzo miongoni mwa watu wakubwa zaidi kuathiri Ulimwenguni kunaweza kuwashangaza baadhi ya wasomaji na wengine watakuwa na masuala, Lakini yeye ni Mtu pekee miongoni mwa hao watu wakubwa ambaye amefaulu zaidi kwa upande wa dini na dunia"

**Michael Hart**

*Mtunzi wa kitabu "Mia moja, Watu watukufu zaidi kuathiri katika Tarekhe"*

1 Ushahidi wa Wasomi
2 Sifa zake na Wasifu wake
3 Maisha yake na Sira yake
4 Utume na Ujumbe
5 Maadili na Ustaarabu
6 Mwanamke
7 Haki za Binaadamu
8 Mazingira
9 Muujiza
10 Hadithi za Mtume
11 Sanaa ya Khati za Kiislamu
12 Usanifu wa Kiislamu

*Nyongeza ya picha za Sanaa ya Khati na Usanifu wa Kiislamu na Misikiti muhimu na sehemu za Historia za Kitalii katika nchi za Ulimwenguni*

ISBN 978-0-9807277-6-0

9 780980 727760